AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

UNIÓN AFRICANA

Addis Ababa, Ethiopia P. O. Box 3243 Telephone: 5517 700 Fax: 5517844
**Website: www.au.int**

**MKUTANO MKUU WA UMOJA WA AFRIKA**
**Mkutano wa Thelathini na Nane wa Kawaida**
**15 - 16 Februari 2025**
**Addis Ababa (ETHIOPIA)**

**Assembly/AU/Dec. 903-941(XXXVIII)**
**Assembly/AU/Decl.1-6(XXXVIII)**
**Assembly/AU/Res.1-2(XXXVIII)**
**Assembly/AU/Motion(XXXVIII)**

# MAAMUZI, MAAZIMIO NA MAAZIMIO

**UAMUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KAULIMBIU YA MWAKA 2025 : "HAKI KWA WAAFRIKA NA WATU WENYE ASILI YA AFRIKA KUPITIA FIDIA." Doc.EX.CL/1569(XLVI)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Dec.884(XXXVII), wa Februari 2024 ambao uliteua Kaulimbiu ya Mwaka 2025 kuwa "Haki kwa Wafrika na Watu wa Asili ya Afrika Kupitia Fidia;"

2. **UNAREJELEA PIA** uamuzi EX.CL/Dec.1267(XLV) wa Julai 2024 kuhusu kupitishwa kwa Andiko la Mpango wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025, ambalo lilisisitiza utekelezaji wa uamuzi Assembly/AU/Dec.884(XXXVII); **UNASISITIZA** kwamba ni hatua muhimu kuelekea kutafuta haki na uponyaji kwa Waafrika na Watu wenye Asili ya Afrika na kutaka uwajibikaji kwa uhalifu wa kutisha uliofanywa dhidi ya Waafrika na wanadiaspora ya Afrika wakati wa biashara ya utumwa iliyovuka Atlantiki, ukoloni na ubaguzi wa rangi, mauaji ya kimbari na ukoloni mamboleoikijumuisha kufukuzwa, mauaji ya halaiki, kuwekwa kizuizini kiholela, matumizi ya unyanyasaji, na uporaji wa maliasili, na majaribio ya nyuklia, ambayo yalipelekea majang aya kimazingira wakati wa enzi ya ukoloni ;

3. **UNAKARIBISHA** Ripoti ya Maendeleo ya Kamisheni kuhusu Utekelezaji wa uamuzi Assembly/AU/Dec. 884(XXXVII) na uamuzi Ex.CL/Dec.1267(XLV), ikijumuisha Mpango Mkuu [Rev 1]; **UNAPITISHA** Ripoti ya Maendeleo ya Kamisheni; na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kutoa fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji madhubuti wa shughuli zilizobainishwa katika ripoti hiyo.

4. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kutekeleza Kaulimbiu ya Mwaka 2025 katika nchi zao; na pia **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutoa rasilimali za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa kaulimbiu ya mwaka katika ngazi ya kitaifa.

5. **UNAPITISHA** pendekezo la Mhe.. Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa kuanzisha Siku ya Afrika ya kuwaenzi mashujaa wa Afrika na waathirika wa biashara ya utumwa iliyovuka Atlantiki, ukoloni na ubaguzi wa rangi; na **UNAIOMBA** Kamisheni kuanzisha mashauriano na Nchi Wanachama ili kupanga tarehe hii;

6. **UNAKARIBISHA** pendekezo la Algeria la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa la Uhalifu unaohusiana na ukoloni, kwa uratibu wa pamoja na Kamisheni;

7. **UNAIOMBA** Kamisheni, kwa ushirikiano wa karibu na Nchi Wanachama za AU, Vyombo na Taasisi za AU na RECs; Asasi za Kiraia za Afrika, pamoja na vyuo vikuu vya Afrika, taasisi za kidini, asasi zisizo za serikali; wadau muhimu katika Diaspora ya Afrika, ikiwamo CARICOM; vyombo husika vya Umoja wa Mataifa na wadau

wengine muhimu wa kimataifa, kuratibu utekelezaji wa Kaulimbiu ya Mwaka 2025; na kufuatilia maendeleo yake na kuwasilisha ripoti ya maendeleo katika Mkutano wa 7 wa Uratibu wa Nusumwaka unaotarajiwa kufanyika Juni/Julai 2025, na pia katika Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali utakaofanyika Februari 2026.

**UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO YA MALARIA AFRIKA**
**Doc. EX.CL/1571(XLVI)A**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA** "Ripoti ya Maendeleo ya Malaria Afrika 2024" iliyowasilishwa na Mh. Umaro Sissoco Embaló, Rais wa Guinea-Bissau na Mwenyekiti wa Muungano wa malaria wa Viongozi wa Afrika (*African Leaders Malaria Alliance*);

2. **UNAREJELEA** Mfumo wa Kichocheo wa Umoja wa Afrika wa Kutokomeza UKIMWI, Kifua Kikuu na Kutokomeza Malaria Barani Afrika ifikapo 2030 na maamuzi na maazimio ya siku za nyuma yanayozitaka Nchi Wanachama kuchukua hatua madhubuti ili kufikia malengo hayo. **UNAUPONGEZA** Umoja wa Afrika kwa Mwongozo mpya wa kuharakisha juhudi za kutokomeza malaria, UKIMWI na TB barani Afrika ifikapo mwaka 2030;

3. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Jamhuri ya Cabo Verde kwa kupata ithbati ya Shirika la Afya Ulimwenguni ya kutokomeza Malaria;

4. **UNAELEZEA WASIWASI WAKE** kwamba malaria inasalia kuwa chanzo kikuu cha magonjwa na vifo, hasa miongoni mwa watu walio katika hatari kubwa zaidi, na kikwazo cha kufikia Mkakati wa Afya wa Afrika (2016-2030) na vipaumbele vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi vilivyoainishwa katika "Ajenda 2063: Afrika Tunayoitaka";

5. **UNAELEZEA WASIWASI PIA** kuhusu tishio linaloongezeka la ukinzani wa kibayolojia, upungufu wa rasilimali, dharura za kibinadamu, na mabadiliko ya Tabianchi ili kudumisha maendeleo ambayo yamefikiwa dhidi ya malaria;

6. **UNATAMBUA** kwamba kutokomeza malaria kunahitaji masuluhisho ya haraka, jumuishi na ya kiubunifu ambayo yanahusisha serikali nzima na jamii nzima;

7. **PIA UNATAMBUA** jukumu la The Global Fund katika kufadhili afua muhimu za kuokoa maisha dhidi ya malaria na umuhimu wa kufufua mfuko huu mwaka huu;

8. **UNATAMBUA ZAIDI** umuhimu wa Vipimo vya Uwajibikaji na Utekelezaji vya ALMA, vipimo vya utekelezaji vya kikanda na kitaifa na zana zingine zenye ushahidi katika kubaini vikwazo na kuendeleza uwajibikaji na hatua za mapambano dhidi ya malaria;

9. **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda na Wadau wa Maendeleo kutoa msukumo mkubwa ili kuharakisha maendeleo ya vita dhidi ya malaria, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua muhimu zifuatazo; kuunda mfumo wa kichocheo wa mapitio ya katikati ya muhula na Mwongozo wa AU ili kushughulikia magonjwa makubwa zaidi barani, kuandaa mipango ya

kuongeza kasi ya nchi yenye gharama na kufuatilia maendeleo ili kuendelea na juhudi za kutokomeza malaria;

a. Kuendeleza ajenda ya uhamasishaji wa rasilimali za ndani kupitia uanzishaji wa Mabaraza na Mifuko ya Kutokomeza Malaria;
b. Kuharakisha Ufadhili wa Afya Jumuishi ikiwa ni pamoja na mradi wa IDA wa Benki ya Dunia wa dola bilioni 5, kuomba na mbinu muhimu za afya duniani kutoa rasilimali za ziada ili kusaidia kuongeza afua za Malaria na Magonjwa ya Kitropiki Yaliyopuuzwa na kuharakisha maendeleo dhidi ya malaria;
c. Kuimarisha matumizi ya zana za vipimo vya utekelezaji wa mapambano dhidi ya malaria ili kuendesha utetezi wa sekta mbalimbali, hatua na uwajibikaji;
d. Kujumuisha zaidi malaria katika uhusiano mpana wa afya na maendeleo, ikiwa ni pamoja na kupanua nguvu kazi ya afya ya jamii, kuunganisha mabadiliko ya tabianchi, na majibu ya mabadiliko ya kijinsia na afua zinazohakikisha upatikanaji wa huduma bora na za gharama nafuu;
e. Kuwekeza katika Kinga, teknolojia ya kidijitali na zana mpya zinazojumuisha uwekaji maalum wa bidhaa za kizazi kijacho za malaria, upatikanaji wa dawa za bei nafuu ikiwa ni pamoja na kuimarisha uzalishaji wa ndani na upatanishi wa udhibiti na kuwekeza katika utafiti na uvumbuzi.

**10.** **UNATOA WITO ZAIDI** kwa jumuiya ya kimataifa kuufufua kikamilifu Mfuko wa Kimataifa wa kutokomeza UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

## UAMUZI
## KUHUSU RIPOTI YA KINARA WA UFADHILI WA NDANI WA AFYA
**Doc. EX.CL/1571(XLVI)B**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** Azimio la Mkutano wa Umoja wa Afrika Assembly/AU/Decl.4(XXXII) kuhusu "Ahadi ya Addis Ababa kuelekea Uwajibikaji wa Pamoja na Mshikamano wa Kimataifa wa Azimio la Kuongeza Ugharimiaji wa sekta ya Afya," ambalo lilimteua Mheshimiwa Rais Paul Kagame kama Kiongozi wa Ufadhili wa Ndani wa Sekta ya Afya;

2. **UNATAMBUA** maendeleo yaliyopatikana katika ripoti ya maendeleo ya utekelezaji ya Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) kuhusu Uwekezaji katika Afya na mapendekezo yaliyomo ndani yake ;

3. **UNAMPONGEZA** Mheshimiwa Rais Paul Kagame, Kinara wa Umoja wa Afrika wa Ufadhili wa Ndani wa Sekta ya Afya, kwa uongozi wake mzuri ambao umekuwa chanzo cha mwongozo wa kimkakati na chachu ya kusukuma mbele ajenda ya ugharimiaji wa sekta ya afya barani Afrika ;

4. **PIA, UNAIPONGEZA** Kamisheni, AUDA-NEPAD, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, Ofisi ya Kinara wa AU wa Ufadhiili wa Ndani wa Sekta ya Afya, na washirika kwa jitihada za pamoja katika utekelezaji wa Mkutano wa Viongozi wa Afrika – Uwekezaji katika Afya, na **UNARIDHISHWA** na maendeleo yaliyopatikana hadi sasa ;

5. **UNATAMBUA** maendeleo yaliyofikiwa na AUDA-NEPAD katika kuanzisha Vituo vya Kikanda vya Ugharimiaji wa Sekta ya Afya (RHFHs) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, na Shirika la Afya la Afrika Magharibi ; na **UNATOA WITO** kwa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda zilizosalia kuharakisha uanzishwaji wa RHFHs ili kuhakikisha hakuna Nchi Mwanachama inayoachwa nyuma katika kufanikisha mifumo ya afya endelevu na yenye usawa ;

6. **UNAPONGEZA** juhudi za Nchi Wanachama, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda, AUDA-NEPAD, na Washirika wa Maendeleo katika kuimarisha ugharimiaji wa ndani wa sekta ya afya kupitia **Majadiliano ya Kitaifa ya Ugharimiaji wa Sekta ya Afya**, ambayo yamefanikiwa kufanyika katika Nchi Wanachama Tisa (9), zikiwamo **Malawi, Zambia, Msumbiji, Kenya, Mauritius, Rwanda, Burundi, Tanzania, na Zimbabwe**; na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kujumuisha matokeo ya Vituo vya Kikanda vya Ugharimiaji wa Sekta ya Afya katika mikakati yao ya kitaifa ili kufanikisha Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) na matokeo endelevu ya afya ;

7. **UNAREJELEA** Azimio Assembly/AU/20(XXXII) kuhusu Ripoti ya Maendeleo ya *AIDS Watch Africa (AWA):* Matokeo ya Mkutano wa Viongozi wa Ngazi ya Juu kuhusu Mfuko wa Ugharimiaji wa Sekta ya Afya, lililotoa wito wa kuongeza ufadhili ili kuimarisha mifumo ya afya na kufanikisha utoaji Huduma ya Afya kwa Wote (UHC).

8. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kuwasilisha kwa Kamisheni, taarifa za maendeleo, mafunzo, na mbinu bora katika kufanikisha Huduma ya Afya kwa Wote, kwa mujibu wa Lengo la Kwanza la Mkakati wa Afya wa Afrika : Kufikia Huduma ya Afya kwa Wote ifikapo 2030 kwa kutimiza ahadi za kimataifa na za bara zilizopo, ambazo zinaimarisha mifumo ya afya na kuboresha viashiria vya kijamii vya afya barani Afrika.

9. **UNAIAGIZA** AUDA-NEPAD kuimarisha Vituo vya Kikanda vya Ugharimiaji wa Sekta ya Afya (RHFH) kwa kubadilishana maarifa na kutanua wigo wa mbinu bora za mageuzi ya ugharimiaji wa ndani wa sekta ya afya.

10. **UNAREJELEA** azimio Assembly/AU/Decl.4(XXXII) ambalo linasisitiza kukuza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuimarisha mifumo endelevu ya ugharimiaji wa sekta ya afya; **UNAMPONGEZA** Mheshimiwa Rais William Ruto kwa uzinduzi wa Programu ya AUDA-NEPAD ya Uwekezaji na Ugharimiaji katika Sekta ya Afya Afrika (PIFAH), na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama zinazotekeleza ahadi za Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) kutumia mfumo huu kwa ajili ya kuendeleza na kutekeleza miradi ya kipaumbele ya uwekezaji katika afya ili kubadilisha Uchumi wa sekta ya Afya Afrika.

11. **UNAKARIBISHA** kupitishwa kwa Hadidu za Rejea za Kikosikazi cha UA kuhusu Ugharimiaji wa Sekta ya Afya na Kikao cha Kawaida cha Tano cha Kamati Maalum ya Kitaalamu kuhusu Afya, Idadi ya Watu, Lishe na Udhibiti wa Dawa kilichomalizika tarehe 9 Agosti 2024, na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kuunga mkono kuanzishwa na utekelezaji wa kikosi kazi hicho.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA *AIDS WATCH AFRICA* (AWA)
## Doc. EX.CL/1571(XLVI)B

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA**

(i)Ripoti ya *AIDS Watch Africa* (AWA) ya mwaka 2023 na mapendekezo yaliyomo;
(ii)Maendeleo ya utekelezaji wa Ripoti ya Uwekezaji katika Maendeleo ya Afya ya Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) na mapendekezo yaliyomo;
(iii) Andiko dhana kuhusu Mkutano mkuu maalumu na muhtasari wa Mwongozo kuhusu: “Kudumisha mwitikio wa UKIMWIo (Kifua kikuu na Malaria), kuhakikisha mifumo inaimarishwa na usalama wa afya kwa maendeleo ya Afrika;
(iv)Kadi ya alama za Kifua Kikuu (TB) ya 2022 na Azimio la Ngazi ya Juu la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (HLM) la mwaka 2023 kuhusu TB.

**2.** **UNAIPONGEZA** Kamisheni, AUDA-NEPAD, Ofisi ya Kinara wa Ufadhili wa Ndani wa Afya, Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Mfuko wa Dunia na kusaidia washirika wa midahalo ya kitaifa ya ufadhili wa afya na **UNAHIMIZA** Jumuiya nyingine za Kiuchumi za Kikanda za Afrika kuzindua midahalo ya kitaifa ya ufadhili wa afya kwa kuendana na Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) kuhusu Uwekezaji katika Azimio la Afya;

3. **UNAREJEA** uamuzi Assembly/AU/Dec.649(XXIX) uliodhamiria “kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika mapambano dhidi ya Malaria na kufuatilia ukinzani wa dawa dhidi ya malaria na ukinzani wa viuadudu”, **UNATAMBUA** umuhimu na mafanikio yaliyofikiwa ya udhibiti wa vijidudu katika kutokomeza malaria na magonjwa mengine yanayoenezwa na wadudu ndani na nje ya bara la Afrika; **UNASHUKURU k**ukamilika kwa mkakati wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa Kukabiliana na Kudhibiti Vekta Duniani 2017-2030, ambao unasisitizia kurekebisha upya programu za udhibiti wa vekta, kuongeza uwezo wa kiufundi, kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, na kuhamasisha jamii na sekta binafsi kama vichocheo muhimu vya kuimarisha udhibiti wa vekta;

4. **UNAIOMBA** Kamisheni, Kituo cha Afrika cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Africa CDC), na AUDA-NEPAD kwa ushirikiano na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanada Afrika zinazotambuliwa na AU na WHO kuendelea kusaidia Nchi Wanachama kuimarisha mifumo ya udhibiti na ufuatiliaji wa usalama kwa bidhaa zilizopo na zinazoibukia za kudhibiti vekta, zana na teknolojia, na kufanya kazi kwa karibu na wizara na wadau wengine wanaohusika katika bara;

5. **UNAPITISHA** rasimu ya Azimio la ‘Kuendeleza Mapambano Dhidi ya UKIMWI, (TB na Malaria), Kuhakikisha Mifumo imara na Usalama wa Afya Barani Afrika'; **UNAIOMBA** Kamisheni, AUDA-NEPAD, Africa CDC; Nchi Wanachama, na washirika kusaidia utekelezaji wake;

6. **UNAIDHINISHA** Hadidu za rejea (TORs) za Kamati ya kudumu ya Wataalamu wa AWA, Hadidu za rejea (TORs) za Mwenyekiti wa AWA, na hadidu za rejea za Kinara wa Afya ya Jamii barani Afrika na **UNAIOMBA** Kamisheni, AUDA-NEPAD, na Africa CDC kusaidia utekelezaji wake ikiwa ni pamoja na lakini sio tu kwa mipango ya utekelezaji iliyoainishwa;

7. **AIDHA UNAIDHINISHA** Mpango wa Afrika wa Kutokomeza Maambukizi ya Wima ya Maambukizi mapya ya VVU, Kaswende na Hepatitis B kwa Watoto ifikapo mwaka 2030 na kuwaweka hai mama zao na **UNAIOMBA** Kamisheni kupitia AIDS Watch Africa, Africa CDC, AUDA-NEPAD kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mpango kwa msaada wa RECS na washirika;

8. **UNATOA WITO KWA** Kamati ya Wataalamu wa AWA kupitia na kupitisha rasimu ya Mwongozo wa gharama kamili wa "Kuendeleza Mapamabano ya UKIMWI (TB na Malaria), Kuhakikisha Mifumo imara na Usalama wa Afya Barani Afrika";

**UAMUZI**

**KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO YA KUANZISHWA NA UENDESHAJI WA TAASISI YA UDHIBITI WA DAWA AFRIKA (AMA)**
**EX.CL/1571(XLVI)C**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Ripoti ya Maendeleo ya Kamishenikuhusu utekelezaji wa Taasisi ya Udhibiti wa Dawa Afrika (AMA) na mapendekezo yaliyomo ndani yake;

2. **PIA, UNAZINGATIA** changamoto zinazohusiana na mrejesho kutoka kwa Nchi Wanachama, na Mashirika ya Afya ya Kikanda (RHOs) ambazo Kamisheniilikabiliana nazo katika kuanzisha Bodi ya Usimamizi ya Taasisi ya Udhibiti wa Dawa Afrika;

3. **UNATOA WITO** kwa Kanda ya Afrika Kaskazini na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS) kukamilisha mashauriano na kuwasilisha majina ya wagombea kwa Kamishenikwa ajili ya kujadiliwa wakati wa kuunda Bodi ya Usimamizi ya AMA;

4. **UNAKARIBISHA** kusainiwa na kuridhiwa kwa Mkataba wa Makao Makuu ya AMA kati ya Kamishenina Serikali ya Rwanda, na Mkutano wa Nchi za Wanachama kupitisha Maelezo ya Kazi ya Mkurugenzi Mkuu wa AMA kwenye Mkataba wa AMA;

5. **VILEVILE, UNAKARIBISHA**, uteuzi wa Bodi ya Usimamizi ya AMA wakati wa Kikao cha Dharura cha Tatu cha Mkutano wa Nchi Wanachama, tarehe 22 Aprili 2024. Wanachama wa sasa wa Bodi wanawakilisha kanda ya Kati, Kusini, Mashariki, na Magharibi pamoja na Shirika la Afya la Afrika Magharibi (WAHO), Jumuiya ya Nchi za Sahel–Sahara (CEN-SAD), na Kamisheniya Umoja wa Afrika;

6. **UNAIPONGEZA** Kamishenikwa kuzindua Makao Makuu ya AMA tarehe 1 Novemba 2024 huko Kigali, kuanzishwa kwa Sekretarieti ya muda, na kuendelea kwa mchakato wa kuajiri Mkurugenzi Mkuu wa AMA ulioanza Septemba 2024, na UNAOMBA kwamba mchakato huu uendane na sheria zinazoanzisha AMA. **UNAIPONGEZA ZAIDI** Serikali ya Rwanda kwa kujitolea kwake na uongozi wake katika utekelezaji wa Mkataba wa Nchi Mwenyeji wa AMA.

7. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ishirini na nane (28) zilizoridhia Mkataba wa AMA na **UNAZITAKA** Nchi Wanachama zilizosalia kuridhia na kujiunga na AMA.

8. **UNATAMBUA** changamoto za kifedha zinazoikabili AMA na **INAZIOMBA** Nchi Wanachama kukusanya rasilimali za ndani na kugharimia mahitaji ya AMA, ikiwa ni pamoja na, lakini siyo tu, mshahara wa Mkurugenzi Mkuu atakayechaguliwa na

nafasi muhimu zinazohitajika katika awamu ya awali ya utekelezaji wa AMA, hii ikiwa ni kulingana na kiwango cha tathmini ya Umoja wa Afrika katika nafasi za kufanya kazi kwa muda.

9. **UNASISITIZA** kuwa AMA ni taasisi maalum la Umoja wa Afrika inayotokana na mkataba ambapo uanachama unategemea kuridhiwa kwa Mkataba wa Kuanzisha AMA.

# UAMUZI WA MKUTANO MAALUMU WA WAKUU WA NCHI WA KUTEKELEZA MPANGO WA KUTOKOMEZA UKIMWI IFIKAPO MWAKA 2030, MPANGO WA UMOJA WA AFRIKA WA KUSHUGHULIKIA VIFO VYA WAJAWAZITO, MAGONJWA YA KUAMBUKIZA NA YASIYO YA KUAMBUKIZA KATIKA BARA LA AFRIKA, NA KUIMARISHA MIFUMO YA AFYA KWA AJILI YA MAENDELEO YA AFRIKA - EX.CL/1571(XLVI)D

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/Dec.852(XXXVI)kuhusu Mpango wa mwaka 2030 wa Kudumisha Ushughulikiaji wa UKIMWI, Kuhakikisha Uimarishaji wa Mifumo na Usalama wa Afya kwa maendeleo na kufanyika kwa Mkutano wa Dharura wa kutokomeza UKIMWI, na **UNAZINGATIA** kwamba Kamishenihaikuweza kuitisha Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi hadi kufikia Julai 2024, na **PIA UNAZINGATIA** kwamba kiasi cha Dola za Marekani Milioni Moja na Laki Saba (**US$1,700,000**) kwa ajili ya kuandaa Mkutano Maalumu kilichoahidiwa na USAID sasa kimesitishwa kufuatia mabadiliko ya hivi karibuni ya serikali ya Marekani.

2. **UNAAMUA** kwamba Mkutano wa Dharura ambao awali uliopangwa kufanyika mwaka 2024 ufanyike mwaka 2025.

3. **UNAIDHINISHA** Mpango Kamili wa kuelekea 2030 na Baadaye: "Kudumisha Ushughulikiaji wa UKIMWI, Kuhakikisha Uimarishaji wa Mifumo na Usalama wa Afya kwa Maendeleo ya Afrika" kama mfumo mkuu wa sera kwa Bara, na andikodhana kwa ajili ya Mkutano wa Dharura wa Nchi Wanachama kuhusu Kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030, na Kushughulikia Vifo vya Wajawazito vinavyoepukika, Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza Barani Afrika, na Kuimarisha Mifumo ya Afya ifikapo 2030.

# UAMUZI KUHUSU UENDESHAJI WA SHIRIKA LA MSAADA WA KIBINADAMU LA AFRIKA
# Doc. EX.CL/1572(XLVI)B

**MKUTANO MKUU:**

1. **UNAZINGATIA** Uamuzi EX.CL/Dec.1269(XLV) uliopitishwa Julai 2024, mjini Accra, Ghana kuhusu Ripoti ya Timu Huru ya Kiufundi ya AU kuhusu Kuwa Mwenyeji wa Shirika la Msaada wa Kibinadamu Afrika (AfHA);

2. **UNAAMUA** kwamba AfHA litakuwa na makao makuu yake katika Jamhuri ya Uganda na unaiomba Serikali ya Uganda na Kamisheni kuchukua hatua zote muhimu, ikiwa ni pamoja na makubaliano ya nchi mwenyeji, ili kuhakikisha kuwa Shirika hilo linafanya kazi haraka. iwezekanavyo.

3. **UNAZIOMBA** Nchi zote Wanachama, wabia wa huduma za kibinadamu na maendeleo, na wadau wa sekta binafsi kutoa msaada kamili kwa ajili ya utendaji kazi kamili wa AfHA ili kutekeleza mamlaka yake;

4. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama, Mashirika ya Kibinadamu na Wabia wa Maendeleo kutimiza ahadi zao walizotoa wakati wa Mkutano Maalumu kuhusu huduma za Kibinadamu wa mwaka 2022 mjini Malabo.

**UAMUZI**
**KUHUSU UTEKELEZAJI WA MATOKEO YA MKUTANO WA DHARURA WA 15 WA MASUALA YA KIBINADAMU NA MKUTANO WA AHADI**
**Doc. EX.CL/1572(XLVI)C**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** ripoti ya utekelezaji wa matokeo ya Mkutano wa Dharura wa 15 wa Masuala ya Kibinadamu na Mkutano wa Ahadi, uliofanyika tarehe 27 Mei 2022, huko Malabo, Equatorial Guinea na **UNAIPONGEZA** Kamishenikwa kazi iliyofanyika hadi sasa.

2. **UNAIOMBA** Kamisheni kuendelea kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Malabo wa Miaka 10 na kushirikiana na Nchi Wanachama na washirika kutimiza ahadi zao.

3. **UNAZIPONGEZA** nchi amabzo zimetekeleza ahadi zao na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama na Washirika ambao hawajatimiza ahadi zao hadi sasa kufanya hivyo haraka iwezekanavyo.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO JUU YA ENEO HURU LA BIASHARA LA BARA LA AFRIKA (AFCFTA), YA MHE. MAHAMADOU ISSOUFOU, RAIS WA ZAMANI WA JAMHURI YA NIGER NA KIONGOZI WA AfCFTA – Doc. Assembly/AU/9(XXXVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPOKEA** na kupongeza Ripoti ya Mheshimiwa Bw. Issoufou Mahamadou, Kinara wa AfCFTA na Rais wa zamani wa Jamhuri ya Niger, na KUPITISHA mapendekezo yaliyomo.

2. **UNAREJEA** Maamuzi Assembly/AU/Dec.854(XXXVI) na Assembly/AU/Dec.902(XXXVII) yanayopitisha Protokali za Uwekezaji, Haki Miliki, Sera ya Ushindani, Biashara ya Kidijitali na Wanawake na Vijana katika Biashara na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama zinazotakiwa kufanya hivyo na mifumo yao ya kisheria kuziridhia na Nchi Wanachama zote ziingize Protokali hizi ili kuwezesha utekelezaji wake kikamilifu.

3. **UNAWAPONGEZA** washirika wa maendeleo, Jamhuri ya Korea ya Kusini, EU-TAF, China, Uturuki na Benki ya Dunia kwa kuendelea kuunga mkono Sekretarieti.

4. **UNAPONGEZA NA KUSHUKURU kwa** msaada mkubwa unaotolewa na Afreximbank, AfDB na BADEA. **UNAZINGATIA** ushirikiano muhimu unaoendelea kati ya Sekretarieti ya AfCFTA na taasisi hizi muhimu za fedha za maendeleo.

5. **UNAITAKA** Afreximbank na Sekretarieti ya AfCFTA kuharakisha utekelezaji wa Mfuko wa Maboresho ya AfCFTA na kuanza kwa haraka utoaji wa fedha chini ya Mfuko huo.

6. **UNAIAGIZA** Afreximbank na AfDB kutoa vifaa na usaidizi wa kifedha kwa Makampuni ya Biashara ya AfCFTA.

7. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kukamilisha mazungumzo ya Viambatisho na Kanuni kuhusu Protokali za Hakimiliki Bunifu, Sera ya Ushindani na Wanawake na Vijana katika Biashara ifikapo Oktoba 2025 na kuzipendekeza kupitishwa na Mkutano wetu wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwaka 2026.

8. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kuhakikisha kuwa wanawake na vijana katika biashara wanapewa mapendeleo yenye maana ya kupata soko chini ya utaratibu wa kibiashara wa AfCFTA na kuhitimisha mazungumzo kuhusu Udhibiti wa Mawaziri kuhusu Upatikanaji wa Soko la Upendeleo kwa Wanawake na Vijana, ifikapo mwisho wa 2025.

9. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kuhitimisha mazungumzo kuhusu Kiambatisho cha Kanuni na Taratibu za Kuzuia, Usimamizi na Utatuzi wa Migogoro ya Protokali ya Uwekezaji na kuwasilisha Kiambatisho kilichokamilishwa kwenye Mkutano Mkuu Februari 2026.

10. **UNAPITISHA** Ratiba za Ahadi Maalum za Jamhuri ya Botswana na Muungano wa Comoro na **UNAIPONGEZA** Ethiopia kwa kuwasilisha maofisa wao watano katika sekta tano (5) za kipaumbele.

11. **UNAZITAKA** Nchi wanachama:
    i. kuwasilisha ratiba zao za ahadi mahususi katika sekta tano za kipaumbele ifikapo Oktoba 2025, kwa kuzingatia haja ya kuhitimisha mazungumzo katika sekta tano za kipaumbele na kuanza mazungumzo kuhusu sekta zilizosalia za huduma;

    ii. Kuhitimisha kwa haraka mazungumzo kuhusu mifumo ya udhibiti ya Huduma za Mawasiliano, Fedha, Utalii na Usafiri, na kuhakikisha kwamba zinakamilisha kikamilifu ratiba zilizopitishwa za ahadi mahususi.

12. **UNALIPONGEZA** Baraza la Mawaziri wanaohusika na biashara kwa kuhitimisha mazungumzo kuhusu Viambatisho vya Protokali kuhusu Biashara ya Kidijitali na **KUPITISHA** Viambatisho vinane (8) vya protokali ya AfCFT kuhusu Biashara ya Kidijitali vifuatavyo:
    i. Kiambatisho cha Kanuni za Uasili;
    ii. Kiambatisho cha Vitambulisho vya Kidijiti;
    iii. Kiambatisho cha Malipo ya kidijiti ya kuvuka Mipaka;
    iv. Kiambatisho cha Uhamishaji data wa kuvuka mipaka
    v. Kiambatisho cha Vigezo vya Kuamua Sababu Halali na za Kisheria za Ufichuzi wa Msimbo;
    vi. Kiambatisho cha Usalama na Ulinzi Mtandaoni;
    vii. Kiambatisho cha Teknolojia Zinazochipukia na Zilizostawi; na
    viii. Kiambatisho cha Teknolojia ya Kifedha.

13. **UNAREJELEA** Uamuzi Mkutano Mkuu/Dec./Dec.831(XXXV) ambalo ulianzisha Mfuko wa Marekebisho wa AfCFTA, na **UNAIELEKEZA** Sekretarieti ya AfCFTA na Afreximbank kuanzisha Mfuko wa Biashara wa Kidijitali chini ya Mfuko wa Marekebisho wa AfCFTA, ili kusaidia utekelezaji wa Protokali ya Biahara ya Kidijitali.

14. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri wanaohusika na Biashara kuharakisha utekelezaji wa Viambatisho vyote vya Protokali ya Biashara ya Kidijitali ikiwa ni pamoja na Utambulisho wa Kidijitali wa AfCFTA ulioanzishwa na Protokali ya Biashara ya Kidijitali na kuripoti maendeleo katika Mkutano ujao wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali;

15. **UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Des.902(XXXVII) ulioiidhinisha Kenya na Afrika Kusini kuwa washindi wenzi wa Biashara ya Kidijitali na **KUAMUA** kumteua Mhe. Bola Ahmed Tinubu Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Nigeria kama Protokali ya AfCFTA kuhusu Kinara wa Biashara ya Kidijitali ili kuhamasisha utekelezaji wake na kutoa uongozi wa hali ya juu katika kuwezesha mipango ya kuvuka mpaka kuhusu utekelezaji wa Protokali;

16. **UNAIAGIZA** Sekretarieti ya AfCFTA kutoa msaada wa kiufundi na kujenga uwezo kwa Nchi Wanachama ili kuwezesha na kuharakisha utekelezaji wa Protokali ya AfCFTA ya Biashara ya Kidijitali na Viambatisho vyake.

17. **UNATHIBITISHA** Soko la Sarafu la Afrika la Mfumo wa Kuwezesha Malipo Barani Afrika kama chombo cha kuwezesha biashara kwa sarafu za Kiafrika bila kutegemea sarafu ya tatu na **UNAZISIHI** Benki Kuu zote za Afrika kuunga mkono uwekaji na upitishaji wa sheria hiyo, ikijumuisha na benki za kibiashara.

18. **UNAPOKEA TAARIFA KWA MASIKITIKO** kuhusiana na kutokutekelezwa kwa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika kuhusu kuajiri wafanyakazi wa Awamu ya II na **UNAIAGIZA** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kutoa dola milioni 2.9 kutoka kwenye mfuko wa akiba, kama ilivyoidhinishwa na Uamuzi EX.CL/Dec.1143(XL) wa Februari 2022, na uamuzi AU/17(XXWVII)_E wa Februari 2024 na EX.CL/Draft/Dec.1(XLV)Rev.1 wa Julai 2024 na kuzitoa kutoka kwenye mfuko wa akiba.

19. **UNATAMBUA** umuhimu wa AfCFTA kama moja ya miradi mikuu ya Ajenda 2063: Afrika Tunayoitaka na **UNAZIPONGEZA**:

    i. Angola, Msumbiji na Zimbabwe kwa kuwasilisha ofa za ushuru, **UNAIDHINISHA** upitishwaji wa ofa zao zilizothibitishwa kitaalamu;

    ii. Nchi zilizoridhia kumi na tisa (19) ambazo zimeingiza ofa za ushuru kwa mujibu wa Maagizo ya Mawaziri yaliyowekwa na **UNAZITAKA** Nchi zilizoridhia zilizosalia kuharakisha michakato yao husika ya kitaifa ili kuharakisha utekelezaji wa Mkataba; na

    **iii.** Nchi Wanachama zinazoshiriki katika Mpango wa majaribio wa Biashara Elekezi (GTI) na Katibu Mkuu wa Sekretarieti ya AfCFTA kwa maendeleo yaliyofikiwa chini ya majaribio haya ishara ya biashara ambayo inaweza kufanyika kwa mujibu wa kanuni za mbele za AfCFTA.

20. **UNAZITAKA** Nchi Wanachama:

i. kuwasilisha Ratiba zao kamili za Makubaliano ya Ushuru aina ya A, B na C kufikia mwisho wa Oktoba 2025, kwa kuzingatia hitaji la kuhitimisha kwa haraka mazungumzo kuhusu Kanuni za Uasili ambazo bado hazijakamilika; na
ii. Kuongeza juhudi zinazolenga kuongeza biashara ya ndani ya Afrika chini ya mfumo wa kisheria wa Mkataba wa AfCFTA na kuhimiza sekta binafsi kutumia fursa za biashara chini ya mfumo wa Kampuni za Biashara za AfCFTA (ATCs).

21. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kuchunguza chaguzi zinazolenga kurahisisha, kufuatilia kwa haraka na kuboresha mbinu za kufikia masoko na kuwasilisha ripoti ya maendeleo ya utekelezaji wake katika Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

22. **UNAIDHINISHA** nyongeza ya mwisho ya muda wa kumalizika kwa mazungumzo juu ya Kanuni za Uasili ambazo hazijakamilika kuwa Oktoba 2025, **UNALIELEKEZA** Baraza la Mawaziri kuwasilisha kanuni zozote za uasili ambazo hazijakamilika chini ya mazungumzo yenye uhalali wa kisera kwa ajili ya azimio la mwisho la Mkutano Mkuu na **KUZISIHI** Nchi Wanachama kufanya mashauriano zaidi ya kitaifa juu ya Kanuni za Uasili ambazo bado hazijakamilika kwakusisitiza uhitimishaji wake mnamo Oktoba 2025.

23. **UNAIDHINISHA** Kiambatisho Na. IV juu ya Kanuni za Uasili za toleo lililobadilishwa kuwa HS2022.

24. **UNAIDHINISHA** Utaratibu wa Mapitio ya Kiambatisho Na. 2 na Kiambatisho Na. IV kuhusu Kanuni za Uasili.

25. **UNAIDHINISHA** kuongezwa kwa tarehe ya mwisho kwa miaka mitatu ya ziada kwa vichwa vikuu na vidogo vinavyotegemea ukaguzi wa lazima mwaka 2024 kwa kuwa na mabadiliko katika kanuni baada ya mapitio halisi.

26. **UNAIDHINISHA** kanuni za HS 2301 na 2309.

27. **UNAIDHINISHA** Mwongozo wa utekelezaji wa Kiambatisho Na. 9 cha Protokali ya Biashara ya Bidhaa katika Suluhu za Kibiashara.

28. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kuandaa programu za kuongeza mwonekano na kupitisha mfumo wa AfCFTA wa Kuripoti kwa njia ya mtandao na sekta binafsi.

29. **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kuweka kipaumbele kukamilishwa kwa Mkataba wa Kutambuana kwa AfCFTA (MRA).

30. **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyofikiwa katika majadiliano ya rasimu ya kanuni za utekelezaji wa Protokali ya Mkataba wa kuanzisha Sera ya Ushindani ya

AfCFTA na **UNALIAGIZA** Baraza la Mawaziri kukamilisha kanuni na kuziwasilisha kwa ajili ya kupitishwa katika Mkutano wa Kawaida ujao.

**31.** UNAREJELEA Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly/AU/Des.902(XXXVII) uliopitishwa Februari 2024 kuhusu kuanzishwa kwa Kamati Ndogo ya Mkutano Mkuu kuhusu AfCFTA, na kumteua Mhe. Rais William Ruto wa Kenya kama mwenyekiti wake na UNAMUOMBA Katibu Mkuu kuchukua hatua stahiki ili kuifanya Kamati Ndogo ifanye kazi, ambayo itaundwa na Wakuu wa Nchi kumi, yenye wawakilishi wawili kwa kila kanda, na itaripoti moja kwa moja kwenye Mkutano Mkuu.

**32.** **UNAIDHINISHA** mapendekezo ya Baraza la Mawaziri Wanaohusika na Biashara la kugawa upya mgawanyo wa Biashara ya Kidijitali, Uwekezaji na Haki Miliki, ndani ya bajeti iliyoidhinishwa na muundo wa Sekretarieti ya AfCFTA ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Sekretarieti ya AfCFTA.

**33.** **UNAMUOMBA** Kinara wa AfCFTA, Mhe. Mahamadou Issoufou, kuwasilisha kuwasilisha ripoti ya maendeleo kuhusu hali ya utekelezaji wa AfCFTA kwenye Mkutano wa 7 wa nusu mwaka wa uratibu Julai 2025.

**UAMUZI**
**KUHUSU KAULIMBIU YA UMOJA WA AFRIKA YA MWAKA 2026**
***"KUHAKIKISHA UPATIKANAJI ENDELEVU WA MAJI NA MIFUMO SALAMA YA USAFI WA MAZINGIRA ILI KUFIKIA MALENGO YA AJENDA 2063"***

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** uamuzi EX.CL/Dec.1234(XLIV) inayoidhinisha pendekezo la kupitisha "*Kuhakikisha Upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo ya Usafi wa Mazingira Ili Kufikia Malengo ya Ajenda 2063*" kama Kaulimbiu ya AU ya mwaka 2026.

2. **UNAREJELEA ZAIDI** Uamuzi EX.CL/Dec.1234(XLIV) unaoitaka Kamisheni kutengeneza Sera ya Maji ya Afrika ambayo inatoa mfumo wa kimkakati kuelekea usalama wa maji jumuishi na unaostahimili tabianchi katika bara baada ya 2025.

3. **UNAKARIBISHA** andiko dhana pamoja na mfumo wa utekelezaji na **UNAPITISHA** "Kuhakikisha Upatikanaji Endelevu wa Maji na Mifumo ya Usafi wa Mazingira Ili Kufikia Malengo ya Ajenda 2063" kama Kaulimbiu ya AU kwa mwaka 2026 ili kuimarisha usalama wa maji kuelekea kufikia matarajio ya Afrika ya kupanua fursa za kiuchumi; na kupunguza sababu zinazosababisha ukosefu wa ajira, uhamaji, kupoteza makazi na ukosefu wa usalama.

4. **UNASISITIZA** kuwa Kaulimbiu ya AU ya 2026 inapongeza mipango mingine mikubwa ili kuhamasisha hatua za kufikia Ajenda 2063 ya AU ya "uchumi na jumuiya zinazostahimili mazingira na zinazostahimili tabianchi".

5. **UNAZINGATIA** fursa inayotolewa kwa uhusiano wa kiwima kati ya mfumo wa utekelezaji wa Kaulimbiu ya AU ya mwaka 2026 na Mkutano wa Maji wa Umoja wa Mataifa wa 2026 ili kuharakisha utekelezaji wa SDG 6, maji safi na usafi wa mazingira. Kutumia fursa hiyo kutaweka msimamo wa pamoja wa Afrika kwa Mkutano wa maji wa Umoja wa Mataifa wa 2026 katika hatua ya katikati ya mijadala ya kimataifa kuhusu nini kifanyike ili kuongeza msukumo mpya katika kutekeleza ahadi za Afrika kuhusu maji na usafi wa mazingira.

6. **UNAELEKEZA** Baraza la Mawaziri wa Afrika kuhusu Sekretarieti ya Maji na Kamisheni kuunga mkono utekelezaji na ufuatiliaji wa mfumo wa utekelezaji, kuhakikisha ushirikiano na upatanishi wa wima katika mipango ya utekelezaji ya Kaulimbiu ya AU ya 2026 na Mkutano wa Maji wa UN wa 2026.

**7.** **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama na Vyombo husika vya AU, RECs, Taasisi, Wawakilishi wa Kudumu, Ofisi Maalumu za Kiufundi na Benki ya Maendeleo ya Afrika kusaidia utekelezaji wa mfumo wa utekelezaji wa kaulimbiu katika ngazi zote.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MAENDELEO YA TOGO NA KAMISHENI KUHUSU UTEKELEZAJI WA UAMUZI ASSEMBLY/AU/DEC/848(XXXVI) KUHUSU UANDAAJI WA MKUTANO WA 9 WA AFRIKA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly Decision/AU/Dec. 807(XXXIV) uliopitishwa katika Mkutano Mkuu wa Kawaida wa Thelathini na nne (34), uliofanyika tarehe 6 na 7 Februari 2021, ukiutangaza muongo wa 2021-2031 kama **"Muongo wa Mizizi ya Afrika na Diaspora";**

2. **PIA, UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano Mkuu Assembly Decision /AU/Dec. 848 (XXXVI) uliopitishwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa nNchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika tarehe 18 na 19 Februari 2023, ukiidhinisha pendekezo la Jamhuri ya Togo la kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 9 wa Afrika kwa mwaka 2024 chini ya kaulimbiu. **"*Kufufua Umajumui wa Afrika na Kazi ya Afrika katika mageuzi ya taasisi za kimataifa: Kukusanya Rasilimali na Kujiwekeza upya kwa ajili ya Kuchukua hatua*",** kama sehemu ya shughuli za **"Muongo wa 2021-2031 wa Mizizi ya Afrika na Diaspora";**

3. **UNAZINGATIA** taarifa ya maendeleo ya Kamati Kuu kuhusu utekelezaji wa Uamuzi Assembly Decision /AU/Dec. 848 (XXXIV) ;

4. **UNAKARIBISHA** kuandaliwa kwa mafanikio kwa mikutano sita (6) ya kikanda ya maandalizi kwa ajili ya Mkutano wa 9 wa Afrika ambao awali ulipangwa kufanyika mwaka 2024 mjini Lome, Togo ;

5. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Togo, Kamati Kuu, nchi wenyeji na Kamisheni kwa kazi nzuri iliyofanyika wakati wa mikutano ya kikanda iliyofanyika katika kanda sita (6) za Bara la Afrika, ikiwemo Diaspora kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano wa 9 wa Afrika mjini Lome, Togo;

6. **UNAZINGATIA** kuahirishwa hadi tarehe nyingine uandaaji wa Mkutano wa 9 wa Afrika;

7. **UNAZINGATIA PIA** pendekezo la Jamhuri ya Togo na Kamisheni kuandaa Mkutano wa 9 wa Afrika mwaka 2025 kwa ushiriki wa Nchi zote Wanachama na wawakilishi wa Diaspora;

8. **UNAAMUA** kwamba Mkutano wa 9 wa Afrika utafanyika mwaka 2025 katika Jamhuri ya Togo chini ya kaulimbiu : **"*Kufufua Umajumui wa Afrika na Kazi ya Afrika katika mageuzi ya taasisi za kimataifa : Kukusanya Rasilimali na Kujiwekeza upya kwa ajili ya Kuchukua hatua*";**

9. **UNAIOMBA** Kamisheni na Serikali ya Togo kuendeleza ushirikiano wao ili kuhakikisha maandalizi yanaenda vizuri, uandaaji mzuri na mafanikio ya Mkutano wa 9 wa Afrika;

10. **UNAIOMBA** Kamisheni kutoa msaada kwa ajili ya uandaaji wa Mkutano wa 9 wa Afrika ;

11. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama, wabia wa AU na Diaspora na jamii za watu wenye asili ya Afrika duniani kote kuunga mkono uandaaji wa Mkutano wa 9 wa Afrika na matokeo yake yenye mafanikio;

12. **UNAIOMBA** Jamhuri ya Togo na Kamisheni kutoa ripoti kwa Mkutano Mkuu mwaka 2026 kuhusu matokeo ya Mkutano wa 9 wa Afrika;

13. **UNAAMUA** kushughulikia na suala hilo**.**

**UAMUZI**
**KUHUSU UCHAGUZI NA UTEUZI WA MWENYEKITI NA MAKAMU MWENYEKITI WA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Ripoti za Kamishenikuhusu Uchaguzi na Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamisheniya Umoja wa Afrika mtawalia.

2. **UNAWACHAGUA** na **KUWATEUA** wafuatao kwa kipindi cha miaka minne (4):

| Na. | JINA | JINSI | NCHI | KANDA | WADHIFA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mhe. Mahmoud Ali Youssouf | Mwanaume | Djibouti | Mashariki | Mwenyekiti |
| 2 | Mhe. Balozi Salma Malika Haddadi | Mwanamke | Algeria | Kaskazini | Naibu Mwenyekiti |

3. **UNAWAPONGEZA** Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti waliochaguliwa, unawatakia mafanikio mema katika kutekeleza majukumu yao, na **UNAWAHAKIKISHIA** kuwapa msaada unaohitajika.

# UCHAGUZI WA UONGOZI WA MKUTANO MKUU WA UMOJA WA AFRIKA KWA MWAKA 2025

**Mkutano Mkuu**

**1.** **UNACHAGUA** Uongozi wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika kwa mwaka 2025, kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| i) | Mwenyekiti | Jamhuri ya Angola |
| ii) | Makamu Mwenyekiti wa Kwanza | Jamhuri ya Burundi |
| iii) | Makamu Mwenyekiti wa Pili | Jamhuri ya Ghana |
| iv) | Makamu Mwenyekiti wa Tatu | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| v) | Katibu | Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania |

**UAMUZI KUHUSU**
**RIPOTI YA SHUGHULI ZA BARAZA LA AMANI NA USALAMA (PSC) NA HALI YA AMANI NA USALAMA BARANI AFRIKA –**
**Doc.ASSEMBLY/AU/3 (XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNALIPONGEZA** Baraza la Amani na Usalama (PSC) kwa juhudi zake zinazoendelea katika kushughulikia changamoto za amani na usalama zinazolikabili Bara la Afrika na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama na washirika wote kuheshimu na kuunga mkono utekelezaji wa maamuzi ya PSC.

2. **UNATHIBITISHA** kuwa Mkataba wa Amani, Usalama na Ushirikiano (PSCF) kwa ajili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Kanda, ni chombo madhubuti cha kuwezesha DRC na nchi za Ukanda huu kupata amani na utulivu; **UNATHIBITISHA** dhamira endelevu ya AU, kama mmoja wa wadhamini wa Mkataba huo, kuunga mkono juhudi zinazoendelea za kuhuisha Mkataba huo; **UNAZIPONGEZA** juhudi za Mchakato wa Luanda, chini ya mwamvuli wa Msuluhishi, Mhe. Joao Lourenco, Rais wa Jamhuri ya Angola; na Mchakato wa Nairobi unaoongozwa na EAC chini ya uongozi wa Mhe. Uhuru Kenyatta, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Kenya; **UNAUNGA MKONO** kikamilifu juhudi za Majeshi ya DRC (FADRC), kwa msaada wa Jeshi la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) nchini DRC (SAMIDRC), sio tu kutetea uhuru na heshima ya ardhi ya DRC, lakini pia kuweka mazingira salama na kulinda raia ili kuchangia utulivu, na kufanikisha juhudi za kikanda za kuleta amani nchi DRC; **UNATOA SHUKRANI** kwa Mhe. Felix Tshisekedi, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na Mhe. Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, kwa kujitolea kwao katika utekelezaji wa Mchakato wa Luanda; **UNAELEZEA WASIWASI WAKE KUHUSU** kuzuka upya kwa mashambulizi ya M23, ADF na makundi mengine yenye silaha dhidi ya FADRC; **UNALAANI** ukiukwaji wa haki za binadamu na mashambulizi yanayofanywa na makundi haya yenye silaha na kigaidi dhidi ya kambi za Wakimbizi wa Ndani (IDP), shule na miundombinu ya utawala; **UNASISITIZA HAJA** ya kuimarishwa kwa uratibu wa juhudi ndani ya Mpango wa Pande nne (EAC, SADC, ECCAS na ICGLR); **UNAKARIBISHA WITO** kutoka kwa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutumia mkakati uliyoratibiwa na uimarishaji wa mipango mbalimbali ya utatuzi wa mgogoro wa mashariki mwa DRC; **UNATHIBITISHA** Taarifa rasmi ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC uliofanyika tarehe 8 Februari 2025 jijini Dar es Salaam, Tanzania; Taarifa ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika tarehe 31 Januari 2025; na Taarifa ya Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu matukio ya hivi karibuni katika Eneo la Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo uliofanyika tarehe 29 Januari 2025 na **UNAZISIHI** pande husika kuhakikisha utekelezaji kamili wa maamuzi haya;**UNATHIBITISHA HAJA** ya pande zote

kuheshimu na kutekeleza maamuzi yote yaliyokubaliwa katika mikutano ya awali ya Wakuu wa Nchi, ikiwa ni pamoja na mkutano wa kwanza wa Pande nne uliofanyika Luanda, Juni 2023 na mkutano wa tarehe 17 Februari 2023, uliofanyika Addis Ababa ili kushughulikia hali ya Mashariki mwa DRC.

3. **UNALAANI** uvunaji haramu wa maliasili unaofanywa na vikundi vilivyo na silaha na kigaidi mashariki mwa DRC na **KUTOA WITO** kwa vikundi vyote vinavyohusika kukomesha tabia hii na kuimarisha mifumo iliyopo ya udhibiti na **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU na washirika wote kuunga mkono DRC katika mpango wake mpya wa Uondoaji Silaha na Uunganishaji upya, na mpango wa kurejesha jamii; **PIA UNALAANI** msaada wa kijeshi wa kigeni unaotolewa kwa M23 na kundi lingine lolote linalofanya kazi mashariki mwa DRC na **UNATAKA** kusitishwa mara moja kwa msaada huo na kuondoka mara moja bila masharti kwa wahusika wa nje kutoka kwa eneo lote la Congo.

4. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano katika mapambano dhidi ya ugaidi na makundi yenye silaha mashariki mwa DRC na Afrika, kwa ujumla, kuweka mkazo katika upashanaji habari, ufuatiliaji wa mpakani, na kwa kuwezesha mazungumzo kati ya jamii za mpakani na **UNAKARIBISHA** kuanzishwa upya tarehe 20 Mei 2024, kwa Mkataba wa Operesheni za Pamoja za Uganda (Uganda) na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Uganda iliyopewa jina la “Operesheni Shuja”, ili kukomesha makundi ya kigaidi ya ADF na MTN yanayofanya kazi Lubelo na katika sehemu ya eneo la Irumu; **UNAMPONGEZA** Mhe. Felix Antoinne Tshisekedi Tshilombo, Rais wa DRC, na Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, kwa kujitolea kwao na juhudi zao za kujitolea katika mapambano dhidi ya ugaidi kati ya nchi hizo mbili na UNAIOMBA Kamisheni ya AU na washirika wa kimataifa kuhamasisha uungaji mkono unaohitajika kwa nchi hizo mbili katika juhudi zao za pamoja za kukomesha shughuli za makundi hayo ya kigaidi (MTN na ADF), yenye mafungamano na Dola ya Kiislamu Afrika Mashariki; UNATOA POLE kwa askari wa kulinda amani wa MONUSCO na SADC (Malawi, Afrika Kusini, na Tanzania) Burundi na Uganda wanaoendelea kupambana na makundi yenye silaha na kigaidi mashariki mwa DRC; **UNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa utaratibu wa pamoja wa ufuatiliaji uitwao "Mkakati uliyoimarishwa wa Uhakiki Maalumu" ili kufikia amani ya kudumu Mashariki mwa DRC, kuzihimiza pande husika kutimiza ahadi zao, na kuhakikisha utekelezaji wake kikamilifu na **UNAIOMBA** Kamisheni kutoa msaada wa kutosha kwa Mkakati uliyoimarishwa wa Uhakiki Maalumu na kupeleka afisa uhusiano mjini Goma kuratibu msaada huo.

5. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) kwa maendeleo thabiti yaliyopatikana katika mchakato wa amani na maridhiano kupitia mafanikio katika utekelezaji wa Mkataba wa Kisiasa wa Amani na Maridhiano katika Jamhuri ya Afrika ya Kati (PPR-CAR) na kuihimiza Serikali na watu wa CAR kuendeleza juhudi za kufikia kikamilifu malengo ya DDR; **UNATOA WITO** kwa Kamisheni ya AU kama mratibu mkuu wa Makubaliano ya Amani kutumia taratibu zote zilizopo kwa kuitisha ipasavyo mchakato wa upatanisho na utekelezaji wa PAPPR-CAR, kwa kuwapatanisha na kuwaunganisha wahusika wote kwa mbinu ya pamoja na iliyoratibiwa katika kuisaidia CAR kupata amani ya kudumu; **UNALIPONGEZA** Baraza la Usalama la Umoja wa

Mataifa kuhusiana na kuondolewa kwa vikwazo vya silaha kwa CAR, kuitikia wito wa Uamuzi wa Mkutano Mkuu wa 37 wa kuondolewa kikamilifu kwa vikwazo vya silaha ili kuruhusu CAR kujibu ipasavyo changamoto zake za usalama na kukuza usalama wa taifa; **UNAIPONGEZA** MINUSCA na wanajeshi/polisi wote kutoka nchi zinazochangia kwa kujitolea kwao katika kudumisha amani na utulivu, pamoja na ulinzi wa raia nchini CAR; **PIA UNAPONGEZA** msaada kwa CAR kutoka kwa Kamisheniya Umoja wa Mataifa ya Kujenga Amani katika kuhamasisha msaada wa kimataifa ili kuchochea amani endelevu na ukuaji wa kijamii na kiuchumi nchini CAR; **UNATOA WITO** kwa Kamisheni ya AU kushirikisha Nchi Wanachama zote zilizo katika nafasi ya kufanya hivyo na washirika wa maendeleo kukusanya rasilimali ili kusaidia kitaalamu na kifedha CAR katika kuandaa uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na mkuu utakaofanyika Aprili na Desemba 2025, mtawalia; na UNAIHIMIZA Serikali ya CAR kuendelea kuwashirikisha viongozi wote wa kisiasa nchini kuhusu maandalizi ya uchaguzi wa 2025, ili kuhakikisha ushirikishwaji, ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wanawake na vijana.

6. **UNAWAPONGEZA** waliotia saini Mkataba wa Kukomesha Uhasama wa tarehe 2 Novemba 2022 (COHA) kwa juhudi zao kamili za kusitisha mapigano katika eneo la Tigray, na kuendeleza mazungumzo na maridhiano ya kitaifa; **UNALITAKA** Jopo la Ngazi ya Juu la AU kuhusu mchakato wa amani wa Ethiopia, kuendelea kushirikiana na Wanachama, wadau, na washirika wa kimkakati ili kutoa uungaji mkono mkubwa kwa mchakato wa utekelezaji wa COHA, hasa, upokonyaji wa silaha, uondoaji wa silaha na ujumuishaji upya (DDR), huku kuwezesha mazungumzo ya kisiasa kuhusu masuala yaliyosalia; **UNAELEZEA MSHIKAMANO** na watu wa Ethiopia, na **UNAWAHIMIZA** wadau wote kuendeleza mchakato wa mazungumzo ya kitaifa kama chombo cha kukuza umoja, amani na upatanisho wa kitaifa; **UNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa Kamisheniya Kitaifa ya Ushirikiano na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia na, katika suala hili, **UNAMWOMBA** Mwakilishi Mkuu wa AU katika Pembe ya Afrika na wajumbe wa Jopo la Ngazi ya Juu la AU kushawishi uungwaji mkono wa washirika wa kimataifa na sekta ya binafsi ya Afrika kuunga mkono DDRiti inayoongozwa kitaifa na kuwarejesha IDPs katika IDPs. Mkutano Mkuu **UNAUPONGEZA** Ujumbe wa AU (MVCM) wa Ufuatiliaji, Uthibitishaji na Uzingatiaji uliotumwa katika eneo la Tigray tangu Januari 2023 kwa kujitolea kwa hali ya juu kuhusiana na wajibu wa kutumika kama chombo chanya cha Mkataba wa Pretoria na unakaribisha upanuzi wa MVCM na waliotia saini kwenye Mkataba wake wa Pretoria, **UNAIHIMIZA** Jumuiya ya Kimataifa kuharakisha kuunga mkono; na **UNAWAPONGEZA** wadau wa kikanda, kimataifa, na wa nchi mbili, hasa IGAD, UN, AfDB, Marekani, Norway, Uingereza, Ireland, Denmark, Ujerumani, na Japan, kwa kusaidia utekelezaji wa mchakato wa amani katika eneo la Tigray.

7. **UNAKARIBISHA** maendeleo yaliyofikiwa na Serikali ya Shirikisho la Somalia (FGS) katika nyanja za kisiasa na kijamii na kiuchumi, ikionyesha hatua kubwa kuelekea ujenzi mpya na maendeleo baada ya vita kwa ajili ya kudumu kwa amani na usalama; **UNAWATAKA** wahusika wa kisiasa kusuluhisha kwa pamoja mizozo inayokua kati ya FGS na Nchi Wanachama wa Shirikisho (FMS), na kushiriki katika mazungumzo, mshikamano na upatanisho; **UNASISITIZA UMUHIMU** wa juhudi zaidi za kupatanisha koo zinazohasimiana na kuzuia Al-Shabaab kutumia vibaya malalamiko ya jamii;

**UNAELEZEA WASIWASI** kuhusu hali ya usalama na kuongezeka kwa mashambulizi ya hivi karibuni ya Al-Shabaab dhidi ya kambi za AU/UN na kiraia, na kusisitiza ulazima wa kuepuka ombwe lolote la usalama wakati wa kipindi cha mpito kati ya ATMIS na Ujumbe wa Kusaidia na Kuimarisha Udhibiti wa Umoja wa Afrika nchini Somalia (AUSSOM); **UNATOA WITO** kwa jumuiya ya kimataifa kwa ajili ya kuendelea kujitolea kuunga mkono ipasavyo kasi ya Somalia ya amani, usalama na utulivu, hasa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Somalia katika kujenga uwezo wa vikosi vya usalama vya Somalia (SSF), hasa katika masuala ya vifaa, mafunzo, na vifaa, ili kuhakikisha kwamba ATMIS inatoka kwa urahisi.

8. **UNAKARIBISHA** Azimio 2767 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2024), linaloidhinisha AUSSOM, kufuatia kupitishwa, na PSC, kwa Dhana ya Kimkakati ya Uendeshaji (CONOPs) kwa Ujumbe wa Kusaidia na Kuimarisha Udhibiti wa Umoja wa Afrika nchini Somalia (AUSSOM) katika taarifa yake [PSC/PR/COMM] 21 Agosti 2024; **UNASISITIZA** kauli ya kuhakikisha ufadhili wa uhakika, unaotabirika na endelevu wa AUSSOM; **UNASISITIZA** umuhimu wa kuanzisha utaratibu maalum wa ufadhili, kupitia michango iliyotathminiwa na Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa Azimio nambari 2719 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2023) kama njia inayofaa zaidi ya kutoa ufadhili wa kutosha, unaotabirika na endelevu ili kuepusha changamoto za kudumu za kifedha zinazokabili ujumbe wa awali. **UNAKARIBISHA** Azimio 2767(2024) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, linaloidhinisha AUSSOM na **UNATOA WITO** wa utekelezaji wake hasa inapohusu kipengele cha ufadhili kwa kutumia mfumo azimio 2719 (2023); **UNAMWOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kufanya kazi kwa karibu na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika kutimiza wajibu wa kuripoti katika aya ya 43 na 44 ya Azimio 2767 (20240) na kulitaka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutoa uthibitisho unaohitajika ili kuruhusu utekelezaji wa 2719 kuanzia tarehe 1 Julai 2025; **PIA UNATOA OMBI** jingine kwa Umoja wa Umoja wa Mataifa, EU, na washirika wengine wa kimkakati na wafadhili wapya, ili kuhakikisha ufadhili wa kutosha, unaotabirika na endelevu, na aina za msaada kwa AUSSOM na, katika suala hili, **UNAIOMBA ZAIDI** Kamisheniya AU kuandaa mwongozo kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kukusanya rasilimali ili kujaza pengo la ufadhili la 25% kwa mujibu wa Azimio 2719 la Mkutano Mkuu wa 20. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa kuridhia kwao Mwongozo wa Pamoja wa kutekeleza UNSCR 2719, kuanzia Somalia, na kwa kujitolea kwa ujumla kwa hali ya juu kufadhili shughuli za usaidizi wa amani za AU;

9. **UNAZISHUKURU**, Nchi Wanachama ambazo hivi karibuni zilionyesha nia ya kuchangia askari katika AUSSOM, ambazo ni: Burundi, Djibouti, Misri, Ethiopia, Kenya na Uganda; **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU kukamilisha haraka ripoti kuhusu majibu, kwa kushauriana na Serikali ya Shirikisho la Somalia kuhusu muundo wa Ujumbe; **UNAKARIBISHA** makubaliano yaliyotiwa saini hivi karibuni kati ya Ethiopia na Somalia mjini Ankara, Türkiye tarehe 11 Desemba 2024, **UNAIPONGEZA** Serikali ya Uturuki na Kamisheni ya AU kwa juhudi zilizofanywa; UNASISITIZA dhamira isiyoyumba ya AU ya kuheshimu uhuru, mamlaka, na heshima ya eneo la nchi zote mbili kwa mujibu wa Sheria Anzilishi ya AU na Sheria ya Kimataifa; na **UNAWAOMBA** wachukue hatua zote

muhimu za kuaminiana na kujenga imani katika kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo unafanikiwa.

10. **UNALAANI VIKALI** mzozo mbaya usio na sababu unaoendelea nchini Sudan, ambao umesababisha watu kupoteza maisha na uharibifu wa mali, ikiwa ni pamoja na miundombinu muhimu, pamoja na kuhama kwa watu wengi; **UNASISITIZA** kwa pande husika nchini Sudan kwamba hakuna suluhu ya kijeshi inayowezekana kwa mzozo huo na **UNAZITAKA** kusitisha mara moja na bila masharti mzozo huo, kufanya usitishaji vita wa kudumu na kurejea kwenye mazungumzo yakifuatiwa na mazungumzo ya kitaifa na mpito wa kisiasa uliojumuisha watu wote, ili kupunguza mateso ya muda mrefu ya watu wa Sudan, na kuhifadhi uadilifu wa umoja, usalama wa kitaifa na uhuru wa Sudani kama nchi yake. taasisi; **UNALAANI VIKALI** kutendeka kwa uhalifu wa kikatili unaokiuka sheria za kimataifa za kibinadamu na sheria za kimataifa za haki za binadamu; **AIDHA UNALAANI** kwa nguvu zote uingiliaji wa nje katika mzozo huo unaofanywa na wahusika mbalimbali na **KUWATAKA** wanaochochea mzozo huo ikiwa ni pamoja na kuwapa silaha wapiganaji hao, kinyume na Azimio namba 1556 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2004), kuacha kufanya hivyo mara moja; **UNASISITIZA WASIWASI WAKE** kuhusu kuenea kwa mipango ya upatanishi na amani na vyombo vya uratibu, na **PIA UNASISITIZA** dhima kuu ya AU katika uratibu wa karibu na IGAD na nchi jirani na kutoa wito kwa wadau wote kufanya kazi kupitia Mfumo wa Upanuzi wa AU na Kundi la Msingi la Utatuzi wa Migogoro wa Sudan; UNAIHIMIZA Kamati Maalumu ya Marais ya PSC kuhusu Sudan inayoongozwa na Mhe. Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda, kusaidia kutafuta suluhu ya muda mrefu ya mzozo huo, kwa kuzingatia nguzo sita (6) za Mwongozo wa AU huku ukiweka kipaumbele katika mpango wa kusitishwa kwa uhasama, mazungumzo ya kisiasa, kushughulikia mahitaji ya nchi jirani huku kukiepusha na fujo; na kuhakikisha ufikiaji wa huduma za kibinadamu; **UNALIPONGEZA** Jopo la Ngazi ya Juu la AU kwa ajili ya Sudan, Mjumbe Maalum wa IGAD kwa Sudan na Mwakilishi Maalum wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU kwa Sudan, kwa juhudi zao za ushirikiano na uratibu zenye lengo la kusuluhisha mzozo wa Sudan, na **UNAIOMBA** AU na IGAD kuharakisha kuitisha mazungumzo ya pande zote za kisiasa za nchini Sudan; **AIDHA UNAIPONGEZA** serikali na watu wa nchi jirani za Sudan kwa kuwahifadhi wakimbizi hao wa Sudan; **UNATOA WITO** kwa washirika wa kimataifa wafadhili kutimiza ahadi zao na kutoa fedha hizo ili kusaidia serikali za nchi jirani za Sudan na mashirika ya Umoja wa Mataifa katika juhudi zao za kibinadamu nchini Sudan.

11. **UNAMPONGEZA** Mhe. Salva Kiir Mayardit, Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini na Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Dkt. Riek Machar, na pande zote za Sudan Kusini kwa kuendeleza usitishaji vita wa kudumu wa mapigano kwa miaka sita iliyopita; **UNAWAHIMIZA** wadau wote nchini Sudan Kusini kuendeleza kasi ya sasa ya kutekeleza kwa haraka vifungu vyote vilivyobaki vya Mkataba Uliohuishwa wa Utatuzi wa Mzozo wa Sudan Kusini (R-ARCSS), ikiwa ni pamoja na, mageuzi ya sekta ya usalama, hasa, kuunganisha nguvu, kukamilisha katiba ya kudumu, daftari la wapiga kura, suala la watu waaorejea na wakimbizi wa ndani na kufanya sense ya watu, itafungua njia kwa ajili ya kuandaa uchaguzi huru, wa haki, na wa kuaminika ili kuashiria mwisho wa mpito; **UNAZINGATIA** uamuzi wa Serikali ya Jamhuri ya Sudan Kusini wa

kuongeza muda wa mpito kwa miaka miwili (2), hivyo kuahirisha ipasavyo uchaguzi utasogezwa kutoka Desemba 2024 hadi Desemba 2026; **UNAIHIMIZA** Serikali ya Mpito Iliyoundwa upya ya Umoja wa Kitaifa (R-TGoNU) kutafuta suluhu ya kudumu ya ghasia kati ya jamii, na katika muktadha huu, **UNAZITAKA** mamlaka zinazohusika katika maeneo yote ya nchi yaliyoathiriwa na ghasia za kijamii kushughulikia kwa ukamilifu sababu za msingi, ikiwa ni pamoja na kupitia programu za DDR na udhibiti wa silaha ndogo ndogo na nyepesi, kwa nia ya kuimarisha amani na usalama katika maeneo haya; **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama wa AU, yenye nafasi ya kufanya hivyo, na jumuiya kubwa zaidi ya kimataifa, kuendelea kutoa msaada unaohitajika kuelekea utekelezaji kamili wa R-ARCSS; **UNAIPONGEZA** Serikali na Watu wa Sudan Kusini kwa kuwahifadhi wakimbizi wa Sudan na raia wa Sudan Kusini waliorejea nchini humo wanaokimbia mzozo nchini Sudan na **KUTOA WITO** kwa washirika na wafadhili wa kimataifa kutoa ufadhili na msaada unaohitajika kwa mashirika ya misaada ili kuyawezesha kutoa misaada ya kibinadamu kwa ufanisi kwa wakazi wanaohitaji; **UNAKARIBISHA** juhudi za Kamati ya Ngazi ya Juu ya Awamu ya Tano (C5) kuhusu Sudan Kusini, na **UNAIHIMIZA** C5 kuendelea na mazungumzo yake kuhusu Sudan Kusini; **UNATOA WITO** kwa Umoja wa Mataifa kuondoa kwa haraka vikwazo vya silaha na vikwazo vingine vilivyowekewa dhidi ya Sudan Kusini pamoja na washirika wa kimataifa ili kuondoa hatua zote za adhabu zilizowekwa kwa nchi hiyo, ili kuwezesha utekelezaji wenye mafanikio wa vipengele vilivyobaki vya R-ARCSS.

12. **UNAKARIBISHA** kutiwa saini kwa Mkataba wa Amani na Maridhiano ya Kitaifa wa Libya tarehe 14 Februari 2025 mjini Addis Ababa, Ethiopia, kama maendeleo makubwa yenye lengo la kukuza amani, utulivu na maridhiano nchini Libya na ANATOA WITO kwa pande nyingine zote kufikiria kujiunga na makubaliano kwa lengo la kutia saini Mkataba haraka iwezekanavyo kwa maslahi zaidi ya amani endelevu na utulivu wa nchi.na **UNAPONGEZA** juhudi za Baraza la Rais kwa kuimarisha utulivu na heshima ya Azimio la kusitisha mapigano kwa zaidi ya miaka minne **NA UNAZIHIMIZA** pande zote kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kisiasa. **PIA UNAPONGEZA** jukumu zuri la Tume ya Pamoja ya Kijeshi {5+5) na **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama wa AU, Kamisheni ya AU, UN na Jumuiya ya Kimataifa kwa ajili ya kuungwa mkono na JMC kwa juhudi zake zinazoendelea za kuunganisha taasisi ya kijeshi.

13. **UNARIDHISHWA** na juhudi endelevu za Kamati ya Ngazi ya Juu ya AU kuhusu Libya kwa juhudi zake na **UNATOA WITO** wa kuzidisha uungaji mkono wake kuelekea Maridhiano ya Kitaifa ya ndani ya Libya ya wadau wote, kwa uungaji mkono wa karibu wa nchi jirani za moja kwa moja za Libya na nchi zingine muhimu za eneo la kaskazini ambazo zina jukumu muhimu katika kudumisha amani ya nchi na utulivu wake; **UNAMPONGEZA,** hasa, Rais Denis Sassou Nguesso, Mwenyekiti wa Kamati ya Ngazi ya Juu ya AU kuhusu Libya kwa uongozi wake na kujitolea kwake kuelekea amani na maridhiano ya kitaifa ya Libya; **AIDHA UNAPONGEZA** juhudi za upatanishi za Jean-Claude Gakosso, Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Congo, na Profesa Mohamed Al Hacen Ould Lebatt, Mkuu wa Wafanyakazi wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU, kwa juhudi zao za kuunga mkono mchakato wa maridhiano ya Libya chini ya usimamizi wa Kamati ya Ngazi ya Juu kuhusu Libya. Mkutano mkuu **UNASISITIZA** kwamba Makubaliano ya Skhirat ya tarehe 17 Disemba 2015, yaliyotokana na

mchakato wa maridhiano kati ya vyama vya Libya, chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa, yanabaki kuwa msingi na mpango wa kuaminika wa suluhisho la kudumu la kisiasa kwa mgogoro wa Libya; na **UNAKARIBISHA**, maendeleo makubwa yaliyopatikana katika maandalizi ya mwenendo wa mchakato wa uchaguzi nchini Libya wakati wa mkutano wa Kamisheniya Pamoja kati ya Baraza la Wawakilishi na Baraza Kuu la Nchi, uliofanyika Bouznika, Morocco, Desemba 2024, ambao ulisuluhisha kutokubaliana na kutunga sheria zinazosimamia uchaguzi ujao wa rais na bunge.

14. **UNAIPONGEZA** Serikali ya Msumbiji, kwa juhudi zilizofanywa katika kushughulikia changamoto za usalama huko Cabo Delgado kwa usaidizi wa Kikosi cha Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika nchini Msumbiji (SAMIM) na washirika wengine wa nchi mbili; **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU kuendelea kutoa msaada unaohitajika kwa Serikali ya Msumbiji kushughulikia hali ya kibinadamu na usalama huko Cabo Delgado ; **UNAIHIMIZA** Serikali ya Msumbiji kuendelea kuimarisha mafanikio yaliyopatikana hadi sasa, pamoja na kuchukua hatua zote zinazohitajika ili kurejesha mamlaka ya Serikali katika maeneo yote yaliyotekwa tena kutoka kwa magaidi, ikiwa ni pamoja na kupitishwa kwa "jamii nzima na serikali nzima" katika kushughulikia sababu za msingi na vichochezi vya ugaidi, kurejesha huduma za msingi za umma, kurejesha amani na shughuli za upatanishi kwa ufanisi zaidi. kuzuia kurudi tena na kuundwa kwa Ukosefu wa usalama; **UNASISITIZA HAJA** ya kufanya juhudi maradufu kukuza masimulizi ya kupingana, mipango ya kuondoa misimamo mikali na kuwajumuisha tena raia ambao walihusika na ugaidi na kuweka mazingira kama vile msamaha kwa wale wanaojitenga na ugaidi na kujisalimisha kwa hiari, na pia kuzuia unyanyapaa kutoka kwa jamii zao; **UNATOA WITO** kwa jumuiya ya kimataifa kuongeza juhudi zake katika kuunga mkono juhudi za amani za Msumbiji na SADC ; **PIA UNAIPONGEZA** Serikali ya Msumbiji kwa kufanya uchaguzi Oktoba 2024; **UNAIHIMIZA** Serikali kushirikiana na SADC na AU, katika kuendeleza mazungumzo kwa ajili ya utatuzi wa amani wa mgogoro wa baada ya uchaguzi, na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuepusha hali hiyo kuwa mbaya zaidi;

15. **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU kuongeza uungaji mkono wake kwa nchi zilizo katika kipindi cha mpito wa kisiasa katika kanda hiyo ili kuhakikisha zinarejea haraka katika utaratibu wa kidemokrasia wa kikatiba na kusisitiza tena umuhimu kwa Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano wa kikanda na nchi za Sahel, katika kubadilishana taarifa za kijasusi, mifumo ya pamoja ya usalama wa mpaka, na juhudi za kukabiliana na ugaidi, haswa ndani ya azma ya Mchakato wa Nouakchott na Kuungana na Kikosi maalumu cha cha Kimataifa dhidi ya Kundi la kigaidi la Boko Haram (MNJTF); **UNATOA WITO** kwa mamlaka za mpito kuweka masilahi ya juu zaidi ya nchi zao na watu wao juu ya yote, na kuhakikisha utekelezwaji madhubuti wa miongozo yao ya mpito, ndani ya muda uliokubaliwa, na kufanya kazi kwa kamati za pamoja za ufuatiliaji wa mpito katika nchi husika na vile vile kuhakikisha michakato ya mpito jumuishi na ya uwazi; na **UNAZIHIMIZA** nchi za Sahel kushughulikia vyanzo vya migogoro ambavyo vinaweza kujumuisha malalamiko yanayohusiana na utawala, kutengwa, na ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi, kwani hii inaweza kusaidia katika kufikia hatua kuu katika kukuza utawala wa kidemokrasia, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria.

16. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Chad (LCBC) kwa msaada wao usioyumba kwa MNJTF; **UNATOA WITO** kwa AU, kupitia Mfuko wa Amani, pamoja na Nchi Wanachama wa AU na Umoja wa Mataifa kuunga mkono juhudi zinazoendelea zinazolenga kutoa msaada kwa makazi mapya ya wakimbizi wa ndani na wanaorejea, pamoja na kuwajumuisha tena wapiganaji waliojisalimisha wa Boko Haram **; UNAIOMBA** Kamisheni ya AU na washirika wa kimataifa kuongeza utoaji wa ufadhili wa kutosha, unaotabirika na endelevu ili kusaidia MNJTF, na utoaji wa viongeza nguvu vya kutosha na viwezeshaji, ikijumuisha kutoka ghala kuu la lojistiki la Bara la ASF, ili kuwezesha Jeshi hilo kuendelea vyema na operesheni zake dhidi ya Boko Haram; **AIDHA UNAIOMBA** Kamisheni ya AU na Washirika kufufua utekelezaji wa Mkakati wa Kuimarisha Kikanda kwa jamii zilizoathiriwa na vitendo vya kigaidi vya Boko Haram .

17. **UNAWAHIMIZA** washirika wa nchi mbili na kimataifa, pamoja na Kamisheni ya AU kuendelea kutoa misaada ya kibinadamu kwa taasisi za Serikali zinazofanya kazi katika Sahel kwa wakati ufaao na bila upendeleo, na kuwafikia watu walio katika mazingira magumu zaidi .

18. **UNAZIPONGEZA** Nchi zote Wanachama zilizofanikisha uchaguzi wa kidemokrasia katika mwaka 2024, zikiangazia uhamishaji mzuri wa mamlaka nchini Botswana, Ghana, Mauritius na Senegal, na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa nchini Afrika Kusini; **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama zote kwa kufanya juhudi za dhati katika kuunganisha utawala wa kidemokrasia na mgawanyo wa amani, kwa nia ya kutimiza Ajenda 2063 na kuheshimu Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala ; **UNAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama kuendelea kuimarisha mifumo ya kitaasisi ambayo itaimarisha ushiriki wa wanawake na vijana katika michakato ya kitaifa ya kisiasa na uchaguzi. na pia kwa kuendelea kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa mashirika ya kitaifa ya usimamizi wa uchaguzi na mahakama, ikijumuisha kutoa fedha na rasilimali watu ya kutosha ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi; PIA **UNAZIHIMIZA N**chi Wanachama kushughulikia suala la kutojali kwa wapigakura kwa kuhimiza mashirika ya usimamizi wa uchaguzi kuanzisha programu za uhamasishaji na elimu ya uraia wakati wa michakato ya uchaguzi ili kuhakikisha idadi kubwa ya wapigakura na katika muktadha huo huo, **UNAZIHIMIZA** asasi za kiraia na vyombo vya habari kuwa na jukumu chanya kwa kuchangia kufanikisha upangaji uchaguzi katika Nchi Wanachama, ikijumuisha kupitia ripoti zinazohusiana na elimu ya uraia na malengo; **AIDHA UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuendelea kukuza na kuimarisha demokrasia, kutanguliza mazungumzo kati na miongoni mwa wahusika wa kisiasa, kupitisha kanuni za maadili za uchaguzi na kutumia njia zilizopo za kisheria kushughulikia mizozo yoyote inayohusiana na uchaguzi; na **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kualika Umoja wa Afrika mara kwa mara kutazama chaguzi zao za kitaifa na kuweka kipaumbele kwa wakati ufaao wa kutumwa kwa Ujumbe huo.

19. **UNAIPONGEZA** Serikali ya Ufalme wa Morocco kwa kuendelea kuunga mkono mafunzo ya waangalizi wa uchaguzi, kwa mara ya tatu mfululizo; **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU kuandaa toleo la 4 la mafunzo hayo maalum, kwa nia ya kuhakikisha uendelevu wake na kuimarisha zaidi mienendo ya kitaaluma ya Misheni za Waangalizi wa Uchaguzi wa AU (AUEOMs) ; **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuiunga mkono Kamisheni katika kutoa mafunzo na kupeleka waangalizi ikiwa ni pamoja na kupitia michango ya hiari katika bajeti ya uchaguzi na katika suala hili, unatambua mchango wa hiari wa dola za Marekani milioni 1 wa Serikali ya Jamhuri ya Niger, mwaka wa 2023, ambayo ilitumika kama bajeti ya usambazaji wa AUEOM mwaka 2024 na **UNAZIHIMIZA** Nchi nyingine zote Wanachama kuiga mfano wa Niger.

20. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo zimeweka mifumo husika ya kisheria kwa ajili ya utekelezaji wa michakato yao ya haki ya mpito na **UNAZIHIMIZA** kushughulikia vyanzo vya msingi vya migogoro, ikiwa ni pamoja na kukuza utamaduni wa amani, uvumilivu wa tofauti za maoni, mapambano dhidi ya matamshi ya chuki, ushirikishwaji, umoja wa kitaifa, mazungumzo na maridhiano, ili kuhakikisha amani na utulivu inadumu.

21. **UNAUPONGEZA** Ufalme wa Morocco, kama nchi ya Kiafrika, kwa kuchukua Urais wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, huko Geneva**.**

22. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuridhia Mkataba wa Afrika wa Maadili na Kanuni za Utumishi wa Umma na Utawala, na Mkataba wa Afrika wa Maadili na Kanuni za Serikali za Mitaa na Maendeleo ya Mitaa, ili kukuza utoaji wa huduma kwa ufanisi na kuimarisha juhudi za kupambana na rushwa.

23. **UNATOA WITO** wa kuandaliwa kwa mkakati wa bara la Afrika ili kushughulikia suala la makundi ya kigaidi na yenye silaha yasiyo ya serikali barani Afrika na **UNAIOMBA** Kamisheni ya AU, UN na washirika wengine kuendelea kutoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama katika programu zao za kitaifa za DDR .

24. **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa juhudi zao za kutegua mabomu na **UNAIHIMIZA** Kamisheni ya AU kuchunguza mbinu za kuanzisha Kituo cha Ubora ili kutoa msaada wa kitaalamu na kuhamasisha ufadhili ili kusaidia Nchi Wanachama zilizoathiriwa katika juhudi zao za kushughulikia mabomu ya ardhi, kwa kuzingatia kusitishwa kwa kuundwa kwa Vyombo vipya vya AU.

25. **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA, kufanya kazi na RECs/RMs, na kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa na washirika wa kimataifa, kuongeza msaada kwa Nchi Wanachama ili kupambana na usambazaji haramu, usafirishaji haramu, usambazaji wa silaha ndogo na nyepesi (ALW) ili kuwanyima magaidi, makundi yenye silaha na wahalifu zana za vita.

26. **UNATOA WITO** wa kuongeza jitihada za kuimarisha zaidi mipango ya bara katika usalama wa baharini.

27. **UNAIPONGEZA** Kamati ndogo ya PRC ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Utawala kwa kazi yake na **KUIHAMASISHA** Kamati ndogo kuendelea kuongeza jitihada katika kuhimiza demokrasia, uwajibikaji, utawala bora, utawala wa sheria na haki za binadamu.

28. **UNAWAPONGEZA** Wajumbe wa Jopo la Washauri la UA kwa mchango wao mkubwa katika mipango ya kuleta utulivu wa kisiasa katika Nchi Wanachama zinazopitia mabadiliko ya kisiasa kwa sasa; **UNALIHAMASISHA** Jopo kudumisha njia za mawasiliano, kukuza uaminifu na imani kati ya nchi hizi, Umoja wa Afrika, na RECs/RMs ili kuhakikisha msaada wa mshikamano na uratibu wakati wa mabadiliko changamani; **UNALIOMBA** Jopo kuimarisha na kupanua zaidi ushirikiano wake na vyombo vya Kikanda vilivyo na mamlaka sawa, ikiwa ni pamoja na Kamati ya Wazee ya ECCAS, Jopo la Wazee la SADC, Baraza la Washauri la ECOWAS, na Kamati ya Wazee ya COMESA, kupitia Mtandao wa PanWise, na vyombo vingine vinavyofanana, ikiwa ni pamoja na Jukwaa la Waliokuwa Wakuu wa Nchi na Serikali Afrika (Jukwaa la Afrika), na Jukwaa la Wazee wa Afrika Magharibi (WAEF), kwa pamoja kuandaa mikakati na mipango ya mshikamano inayolenga kushughulikia kikamilifu changamoto za pamoja na kuendeleza amani, usalama, na utawala endelevu katika Bara; **UNASISITIZA** kuendelea kwake kuunga mkono Jopo katika kutekeleza majukumu yake hususan kuhusiana na uzuiaji, usimamizi na utatuzi wa migogoro; **UNAIELEKEZA** Kamisheni ya UA kuandaa na kutekeleza taratibu za uendeshaji zilizoratibiwa za utumiaji mzuri wa Jopo la Washauri na Wawakilishi wengine wa ngazi ya Juu na Wajumbe Maalumu kwenye maeneo yanayokabiliwa na migogoro.

29. **UNAKARIBISHA** maendeleo yaliyopatikana katika mchakato wa ugatuaji wa madaraka wa Mtandao wa FemWise-Africa; **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama na RECs/RMs kuharakisha juhudi zao za kuanzisha makundi ya kitaifa na kikanda ili kuimarisha nafasi muhimu ya wanawake katika diplomasia ya kuzuia, kupatanisha, na mazungumzo ya amani katika ngazi zote; na **PIA UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama, RECs/RMs, na Kamisheni kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwatumia wapatanishi wanawake na wajenzi wa amani ili kuziba pengo kati ya tahadhari ya mapema na ushughulikiaji wa mapema, kwa kushiriki katika juhudi za kuleta amani katika ngazi za jamii, kitaifa, kikanda na bara.

30. **UNAKARIBISHA** uteuzi wa Kundi la kwanza la wanachama 20 la Mtandao wa WiseYouth; **UNAIPONGEZA** Kamisheni kwa kujumuisha vijana katika diplomasia ya kuzuia na upatanishi katika bara na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama na RECs/RMs kuhimiza matumizi ya Mtandao wa WiseYouth katika kuzuia na kutatua migogoro katika ngazi ya kitaifa, kikanda, na bara, kwa lengo la kuimarisha michakato ya amani inayozingatia na kujumuisha mahitaji ya vijana.

31. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kupitisha mbinu ya pamoja ya kuweka kipaumbele katika ushirikiano wa kikanda, uvumbuzi wa kiteknolojia na masuala ya

kibinadamu ili kulinda amani, usalama na maendeleo katika bara; **UNATHIBITISHA** Azimio la Mkutano wa Viongozi wa Ngazi ya Juu la Kupambana na Ugaidi Afrika, uliofanyika tarehe 22 hadi 23 Aprili 2024, mjini Abuja, Nigeria chini ya kaulimbiu; "Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Ujenzi wa Taasisi Ili Kushughulikia Kuibuka kwa Tishio Linaloendelea la Ugaidi Barani Afrika" na **UNAKARIBISHA** uamuzi wa kuboresha Kituo cha Taifa cha Kupambana na Ugaidi cha Nigeria huko Abuja, kuwa Kituo cha Kupambana na Ugaidi cha Kanda.

32. **UNAIPONGEZA** Kamisheni kwa jitihada zake zinazoendelea za kujumuisha Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama (WPS) katika bara zima; **UNAZIHAMASISHA** Nchi zote Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kupitisha Mipango ya Utekelezaji ya Taifa (NAPs) kwa ajili ya utekelezaji kamili wa Azimio namba 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, pamoja na kutenga fedha za bajeti za kutosha na kwa muktadha mahususi ili kuhakikisha utekelezaji mzuri na endelevu wa Ajenda ya WPS katika ngazi ya taifa.

33. **UNAPONGEZA** maendeleo yaliyofikiwa na kuhimiza kuharakisha ujumuishaji wa ulinzi wa mtoto katika mifumo yote ya tahadhari na ushughulikiaji ya AU ili kuhakikisha ulinzi wa kina katika Nchi Wanachama zote; **UNALAANI VIKALI**, mauaji yanayoendelea, kuajiriwa na kutumiwa kwa watoto katika Bara na makundi ya wapiganaji kwenye mgogoro, hasa, makundi yenye silaha yasiyo ya serikali na mashirika ya kigaidi, kwa ushiriki wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja katika uhasama au madhumuni mengine yoyote; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA iandae waraka wa utendaji bora wa kurejea ili kuzuia na kukomesha ajira na matumizi ya askari watoto yanayofanywa na makundi yenye silaha; **UNAZIHIMIZA** umuhimu wa Nchi Wanachama kutekeleza sera za taifa zinazowiana na maagizo ya UA kuhusu ulinzi wa watoto katika mazingira ya migogoro; **UNASISITIZA HAJA** ya kujumuisha ulinzi wa mtoto katika mchakato wa kuwapokonya silaha, kuwaondoa katika makundi, na kuwarejesha katika jamii ili kuweka mazingira ambayo yanatoa kipaumbele kwa mahitaji ya watoto na kuhakikisha upatikanaji sawa wa programu hiyo; **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama kutoa msaada wa kisaikolojia na baada ya kiwewe kwa watoto na waelimishaji walioathiriwa na migogoro, ikiwa ni pamoja na kujumuisha huduma za afya katika programu za elimu na kutekeleza hatua zinazolengwa ili kuhakikisha usalama wa watoto kama vile njia salama za kwenda shule na mazingira salama ya kujifunzia. **UNASISITIZA HAJA YA HARAKA** kwa Mwenyekiti wa Kamisheni kuteua Mjumbe Maalumu wa Watoto walio katika Mazingira ya Migogoro kulingana na uamuzi wake wa awali;

34. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuendelea kuimarisha ulinzi wa wakimbizi na kambi za wakimbizi wa ndani, na kuendelea kuchukua hatua za ziada ili kuzilinda dhidi ya unyonyaji wowote unaofanywa na makundi yenye silaha na ya kigaidi; **UNAIOMBA**Kamisheni ya UA kuandaa mifumo ya ukusanyaji, uchambuzi na usimamizi wa data na takwimu zinazohusiana na wakimbizi, wanaorejea makwao na wakimbizi wa ndani kwa ajili ya usajili wao, ili kuboresha ufanyaji uamuzi na kuhakikisha hatua madhubuti za misaada ya kibinadamu katika Bara; kipekee, **UNAOMBA** Idara ya Masuala ya Siasa, Amani na Usalama, kuandaa orodha kamili ya viongozi wa makundi

yenye silaha na magaidi barani Afrika wenye hatia ya uhalifu dhidi ya wakimbizi na wakimbizi wa ndani na kwa ajli ya kufunguliwa mashtaka kwa wale wanaotekeleza, kuhimiza, kufadhili au kuwezesha uhalifu huo.

35. **UNAPONGEZA** Kundi la 3 la Mabalozi wa Vijana wa Amani Afrika (AYAPs) kwa kuanzisha jukumu lisiloweza kurejeshwa la miaka 2 kama watetezi wa ajenda ya Vijana, Amani na Usalama katika maeneo yao husika pamoja na kuundwa kwa Orodha ya Wataalamu Vijana kwa Amani ili kutoa msaada wa kitaalamu kwa ajenda ya YPS; **UNAMPONGEZA** Kinara wa UA kwenye YPS, Mhe. Evariste Ndayishimiye, Rais wa Jamhuri ya Burundi, kwa kuitisha Majadiliano ya 3 ya Mwaka ya Bara kuhusu Vijana, Amani na Usalama; **PIA UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama kwa uungaji mkono wao thabiti na wa makusudi kuelekea ajenda ya YPS barani hasa katika uandaaji wa Mipango ya Utekelezaji ya Taifa (NAPS) na **UNAZIHIMIZA** kuzingatia kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa NAPs kuhusu amani na usalama wa vijana kwa kuzingatia sera zao za kitaifa, ili kuongeza ushirikishwaji na uendelevu wa ajenda ya YPS katika ngazi ya Taifa, kanda na bara; **UNATAMBUA** uandaaji wa Rasimu ya Mwongozo wa Bara wa Uendelezaji na Utekelezaji wa NAPS kwenye YPS; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuharakisha mchakato wa kuidhinishwa na kupitishwa na Baraza la Amani na Usalama kufuatia utaratibu uliowekwa, na ndani ya miezi mitatu ijayo, kwa nia ya kuwasilisha kwenye Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi wa UA na **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama kuendelea kukuza ushiriki mzuri wa vijana kupitia vyombo vya kuchukua hatua madhubuti za bara kwa kusaidia mashirika maalumu ya Umoja wa Vijana kama vile Umoja wa Vijana wa Afrika.

36. **UNAIOMBA** Kamisheni kukamilisha mashauriano na Nchi Wanachama, RECs/RMs, Taasisi za Afrika, na washirika kuhusu Msimamo wa Pamoja wa Afrika katika Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama; **UNAIPONGEZA** Kamisheni kwa uongozi wake wa kimkakati katika mchakato wa kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Amani na Usalama, duniani kote, na **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuhakikisha Afrika inapata Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabianchi kupitia mikopo ya masharti nafuu, ikiwa ni pamoja na, ruzuku, dhamana na mikopo ya dhamana za rasilimali na umuhimu wa taratibu za tahadhari ya mapema ili kuunga mkono ahadi za kimataifa za kusaidia jitihada za nchi za Afrika kupunguza na kurekebisha mabadiliko ya tabianchi kama nyenzo muhimu za kujenga amani na mshikamano wa jamii.

37. **UNAMPONGEZA** Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Kinara wa AU wa Ujenzi upya na Maendeleo baada ya Migogoro, kwa uongozi wake endelevu; **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kusaidia kazi ya Kituo cha PCRD huko Cairo; **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyofikiwa na Kamisheni ya UA katika utekelezaji wa shughuli za PCRD katika Bara zima la Afrika na kuihimiza Kamisheni kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Sera wa AU PCRD Uliorekebishwa ili kutoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama zote, hasa zile zilizo katika kipindi cha mpito wa kisiasa na zile zinazotoka katika migogoro mikali; **UNAITAKA** Kamisheni ya UA na RECs/RMs kuandaa uungwaji mkono na Nchi Wanachama katika kushughulikia kikamilifu sababu za msingi za kimuundo, vichochezi na viwezeshi vya migogoro ya

kikatili katika Afrika huku ukisisitiza umuhimu wa ujenzi wa Nchi na uundaji wa taasisi thabiti za Nchi kama msingi muhimu wa amani na maendeleo endelevu barani Afrika. Mkutano Mkuu **PIA, UNAITAKA** Kamisheni ya UA kuharakisha uanzishaji wa Shirika la Misaada ya Kibinadamu la UA ili kuongeza uwezo wa Afrika wa kushughulikia matatizo ya kibinadamu na kukuza ustahimilivu kwa kuhakikisha ushughulikiaji ulioratibiwa na wa kina kwa changamoto za kibinadamu ambao unaunga mkono amani ya muda mrefu, utulivu na maendeleo endelevu katika Bara; **UNATOA WITO** kwa Kamisheni ya UA, Umoja wa Mataifa na washirika wengine kuendelea kuunga mkono shughuli za Kituo cha AU PCRD katika juhudi zake za kuendeleza juhudi za ujenzi mpya baada ya vita na kuleta amani katika Bara la Afrika na **UNATAMBUA** mchango muhimu wa wadau wote wanaohusika, ikiwa ni pamoja na mashirika ya kiraia, sekta binafsi, na jamii za wenyeji, katika kuendeleza kazi ya ujenzi upya baada ya migogoro na maendeleo, hususan katika nchi zinazopitia kipindi cha mpito kisiasa na zile zilizo katika mazingira ya baada ya migogoro, kwa lengo la kujenga na kuimarisha ipasavyo amani barani Afrika.

38. **UNAIPONGEZA** Kamisheni ya UA, Nchi Wanachama, na RECs/RMs kwa kujitolea kuendelea kuimarisha Kikosi cha Dharura cha Afrika (ASF), **UNARIDHIA** kupitishwa kwa Sera ya Mafunzo ya UA ya Operesheni za Kusaidia Amani, Dhana ya Mkakati ya Msaada wa Kijeshi ya UA, na Miongozo ya Usimamizi wa Kesi katika Operesheni za Msaada wa Amani; **UNAIOMBA** Kamisheni ya UA kuharakisha na kupanua mchakato wa mashauriano kuhusu mapitio ya kimkakati ya ASF ili kujumuisha PSC, Nchi Wanachama, REC/RMs zote na Vyuo vya Taaluma Afrika vilivyoidhinishwa na UA, na kuharakisha mchakato wa uandaaji wa mpango wa kina na jumuishi kwa ajili ya mapitio ya kina ya ASF7, na kuwasilisha ripoti ya mapitio ya kina ya Mkutano wa 17 wa STCDSS; **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kujitolea kutoa msaada wa kimkakati wa usafiri wa anga, barabara na baharini kama sehemu ya utekelezaji wa ASF, pamoja na misheni za misaada ya kibinadamu wakati wa matukio ya majanga.

39. **UNALIPONGEZA** Baraza Kuu, Mwenyekiti wa Kamisheni, PSC, PRC, F-15, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya PRC (GSCBFAM), Bodi ya Wadhamini na EMC kwa hatua zilizochukuliwa za kuanzisha Mfuko wa Amani na kuitaka Sekretarieti ya Mfuko wa Amani kuharakisha jitihada za kutafuta rasilimali zaidi, hususan kutoka sekta binafsi na washirika wa Mfuko wa Amani. **PIA, UNAPONGEZA** michango ya moja kwa moja ya UA kupitia malipo kwa EAC, ATMIS na Ethiopia kama wanufaika waanzilishi wa Mfuko, na kama uthibitisho wa ahadi ya Umoja wa Afrika katika kuchangia katika utekelezaji wa amani, utulivu, urejeshaji wa hali ya kawaida na shughuli za DDR; **AIDHA UNAPONGEZA** mgao wa mwaka 2024 kutoka kwa CRF kwa ajili ya Msaada wa mchakato wa kipindi cha mpito wa Sudan Kusini, msaada kwa Mazungumzo ya Amani ya Sudan/Mazungumzo ya Kisiasa, Msaada kwa Ujumbe wa SADC Mashariki mwa DRC (SAMIDRC), Kwa ajili ya kuimarisha Utulivu wa Bonde la Ziwa Chad kupitia MNJTF (Benin, Cameroon, Chadi, Libya, Niger), Msaada kwa Libya - Shughuli za Usuluhishi, Mazungumzo na Utulivu, Msaada wa kuleta utulivu kama sehemu ya kipindi cha mpito kwa Niger, Burkina Faso kwa Msaada wa Uwezo wa Kukabili Ugaidi, Msaada wa jitihada za kuleta utulivu kama sehemu ya mipango ya Mali ya Kupambana na Ugaidi na Msaada kwa Msumbiji kwa Kuimarisha Mipango ya Kupambana na Ugaidi kuelekea Utulivu huko Cabo Delgado.

40. **UNAZINGATIA** maendeleo thabiti katika utekelezaji wa Mpango wa Mipaka wa UA; na kutoa wito kwa Nchi Wanachama, ambazo bado hazijafanya hivyo, kuharakisha uwekaji alama na mipaka kwenye mipaka yao, kupitisha sera za taifa za usimamizi wa mipaka kulingana na Mkakati wa UA wa Usimamizi Mzuri wa Mipaka, na kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa miundo ya kitaifa inayohusika na usimamizi wa mipaka; **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo zimetia saini na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Ushirikiano wa Mipaka, ambao utahimiza kwa kiasi kikubwa mabadiliko ya mipaka kuwa vichocheo vya utangamano na maendeleo endelevu; UNAZIHIMIZA Nchi Wanachama ambazo bado hazijafanya hivyo, kusaini na kuridhia; wakati wa kutekeleza Mpango wa Mipaka wa UA, **UNAIOMBA** Kamisheni na RECs/RMs kuimarisha uratibu ili kuwezesha uingiliaji kati wa pamoja, ili kuleta matokeo zaidi katika maeneo ya mipakani; na **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Cote d'Ivoire kwa kufanikiwa kuandaa kwa kushirikiana na Kamisheni Mkutano wa Pili wa Mipaka wa Abidjan na kuidhinisha kuanzishwa kwa Jukwaa hilo kama jukwaa la bara la wadau wa mipaka, litakaloitishwa kila baada ya miaka miwili, na kusimamiwa kwa pamoja na Serikali ya Cote d'Ivoire na Kamisheni ya UA.

41. **UNATHIBITISHA** Hitimisho la Semina ya Viongozi wa Ngazi ya Juu ya Mawaziri kuhusu AU PSC kuhusu kaulimbiu: Kuadhimisha miaka 20 ya PSC kwa kuzingatia Ushiriki wa Wanawake na Uongozi katika Mazungumzo ya Amani Barani Afrika, "Mazungumzo ya Swakopmund" yaliofanyika tarehe 23 Machi 2024 huko Swakopmund, Namibia; Azimio la Dar es Salaam la Maadhimisho ya Miaka 20 ya Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika lililopitishwa tarehe 25 Mei 2024 jijini Dar es Salaam, Tanzania; Mahitimisho ya Mkutano wa Mwaka wa Mapitio wa 16 wa PSC wa Mapitio ya Mbinu zake za Utendaji Kazi yaliyofanyika tarehe 5 -7 Novemba 2024 nchini Djibouti; na Mahitimisho ya Semina ya 11 ya Viongozi wa Ngazi za Juu kuhusu Amani na Usalama Afrika, Mazungumzo ya Oran yaliyofanyika Algiers, Algeria tarehe 1 - 2 Desemba 2024; na **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuhakikisha utekelezwaji wa Mahitimisho haya katika barua na nafsi zao.

42. **UNAPONGEZA** jitihada zinazofanywa na Wajumbe wa Afrika wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa pamoja na (A3 plus) katika kueleza vyema, kukuza, na kutetea misimamo na maslahi ya pamoja ya Waafrika ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa; **UNAIPONGEZA** Msumbiji, kwa uwakilishi wake wa kupigiwa mfano kwa Afrika ndani ya Baraza la Usalama wakati wa uongozi wake; **UNAIPONGEZA** Somalia kwa kuchaguliwa kwake katika Baraza la Usalama kwa kipindi cha miaka miwili na **UNATARAJIA** ushirikiano na mchango wa Algeria, Sierra Leone na Somalia, pamoja na Guyana kama sehemu ya ziada, katika kueleza kikamilifu, kukuza na kutetea misimamo ya pamoja na maslahi ya Afrika katika UNSC;

43. **UNAIPONGEZA** Kamisheni ya UA kwa jitihada zake za kuimarisha usimamizi wa maarifa na ujifunzaji wa kitaasisi na **UNAHAMASISHA** kuendelea kuwekeza katika kujenga uwezo ili kuimarisha ufanisi na uratibu wa taasisi katika bara zima.

44. **UNAPONGEZA** juhudi za Kinara wa AU katika Kupambana na Ugaidi na misimamo mikali, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, Mhe. Bw. Abdelmadjid Tebboune, katika kuendeleza ajenda ya AU ya kupambana na ugaidi na itikadi kali za kikatili, na **UNATOA WITO** wa utekelezaji wa haraka wa mapendekezo yake madhubuti katika mwelekeo huu;

45. **UNAONYESHA** kuridhishwa na juhudi za A3+ kwa ajili ya kutetea maslahi ya Afrika katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na **UNAKARIBISHA** katika muktadha huu kupitishwa kwa miongozo ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la Algeria kuhusu mapambano dhidi ya ufadhili wa ugaidi;

46. **UNATAMBUA** juhudi za Kituo cha AU cha Kukabiliana na Ugaidi (zamani CAERT) katika kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Nchi Wanachama katika mapambano yao dhidi ya ugaidi na misimamo mikali ya kikatili na **UNAIELEKEZA** Kamisheni kukipatia Kituo hiki cha AU rasilimali watu na nyenzo muhimu ili kukiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

# UAMUZI
# KUHUSU RIPOTI YA NUSU MWAKA YA BARAZA LA AMANI NA USALAMA (PSC) KUHUSU UTEKELEZAJI WA MWONGOZO MKUU WA AU WA HATUA ZA KIVITENDO ZA KUSITISHA MAPIGANO BARANI AFRIKA, 2023-2024 – DOC. Assembly/AU/4(XXXVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPITISHA** Ripoti ya Saba ya Baraza la Amani na Usalama (PSC) la Umoja wa Afrika (AU) kuhusu Utekelezaji wa Mwongozo Mkuu wa Umoja wa Afrika wa Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano Barani Afrika ifikapo Mwaka 2030;

2. **UNAREJELEA** Azimio la Dhati la Maadhimisho ya Miaka 50 ya Shirika la Umoja wa Afrika/ Umoja wa Afrika (OAU/AU) lililopitishwa tarehe 25 Mei 2013, mjini Addis Ababa, ambapo Mkutano Mkuu wa Umoja huo uliahidi kutorithisha mzigo wa vita kwa kizazi kijacho cha Waafrika na kuahidi kumaliza vita vyote barani Afrika ifikapo mwaka 2020; na Uamuzi [Assembly/AU/Dec.630 (XXVIII)] uliopitishwa katika Mkutano wake wa Kawaida wa 28 wa Wakiuu wa Nchi na Serikali wa umoja wa Afrika uliofanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 30 – 31 Januari 2017, ambao uliidhinisha, kufuatia kuwasilishwa na PSC, Mwongozo Mkuu wa AU wa Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano barani Afrika ifikapo 2020; **PIA UNAREJELEA** Azimio la Johannesburg [Ext/Assembly/AU/Decl.1(XIV)] na Uamuzi [Ext/Assembly/AU/Dec.1(XIV)] uliopitishwa na Mkutano Maalumu wa 14 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Kusitisha Mapigano, uliofanyika tarehe 6 Desemba 2020, Johannesburg, Afrika Kusini, ambao uliongeza muda wa utekelezaji wa Mwongozo Mkuu wa AU kuhusu Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano barani Afrika hadi mwaka 2030;

3. **UNALIPONGEZA** Nchi zote Wanachama na RECs/RMs, Kamisheni ya AU; Wabia wa Kimataifa, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi na Vyombo vya Habari kwa michango yenye thamani kubwa katika utekelezaji wa mwongozo MKuu wa Umoja wa Afrika (AU) wa Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano (AUMR) Barani Afrika ifikapo 2030;

4. **UNAPONGEZA** juhudi za Mwakilishi Mkuu wa AU wa Kusitisha Mapigano, Mhe. Dkt. Mohamed Ibn Chambas, na **UNAMWOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuhakikisha kuwa Ofisi ya Mwakilishi Mkuu ina uwezo wa kutosha wa kutekeleza ipasavyo mamlaka yake**;**

5. **UNALAANI** ushiriki wa wahusika wa nje wa serikali na wasio wa serikali katika migogoro ya Afrika, pamoja na utumiaji haramu wa maliasili (madini) unaofanywa

na makundi yenye silaha na ya kigaidi barani Afrika huku ukihimiza Nchi Wanachama kuimarisha ushirikiano na upashanaji habari;

6. **UNASISITIZA UMUHIMU** wa kuheshimu kanuni zilizomo katika hati za kisheria za AU, hususan, Sheria ya Kuanzishwa kwa AU, Protokali inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama la AU, ikiwa ni pamoja na, uhuru wa Nchi Wanachama; uadilifu wa taifa; umoja wa kitaifa; kutoingiliwa katika mambo ya ndani ya Nchi Wanachama; kutokuwa na uchokozi; utatuzi wa migogoro kwa amani;

7. **PIA UNASISITIZA WITO** kwa pande zote zinazopigana, katika Nchi Wanachama zinazokabiliana na migogoro mikali, kukomesha mara moja na bila masharti uhasama wote, kuanzisha usimamishaji vita wa kudumu na kukumbatia mazungumzo ya kweli, jumuishi na maridhiano kama njia pekee inayoweza kutumika kuelekea suluhu za maafikiano na za kudumu;

8. Kwa mara nyingine tena, **UNASISITIZA HAJA** ya kuimarishwa kwa ushirikiano kati na miongoni mwa watendaji wote wanaohusika katika utekelezaji wa AUMR, ikiwa ni pamoja na kupitia kupeana intelijensia na habari na shughuli za pamoja, katika ngazi ya nchi mbili, kikanda na kibara ili kupambana ipasavyo zaidi na usambazaji wa silaha haramu ndogo na nyepesi kuelekea kusitisha kikamilifu mapigano katika Bara;

9. **UNAHIMIZA** Nchi Wanachama kushughulikia kwa kina sababu za kimuundo na vichochezi vya migogoro mikali na ukosefu wa utulivu unaoongozwa na uhusiano wa amani, usalama na maendeleo, ikiwa ni pamoja na mipango ya kimakusudi ya kijamii na kiuchumi ya kuwawezesha wananchi, hasa wanawake na vijana, ili kuwaelekeza upya wananchi kutoka siasa za utambulisho hadi kwenye siasa za maslahi, **PIA UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kupitisha mbinu jumuishi za Serikali nzima-Jamii nzima '*Whole of government-whole of society'*, kwa kuzingatia uhusiano kati ya amani, usalama na maendeleo, kama inavyooneshwa katika Azimio la Tangier, na kutoa ripoti mara kwa mara kwa Kamisheni ya AU juu ya mipango yao ya kazi na shughuli katika kusitisha mapigano, kwa kuzingatia nyanja tano za AUMR kwa madhumuni ya kukuza uzoefu na kubadilishana mafunzo, pamoja na kujadili mapendekezo ya Toleo la 4 la Jukwaa la Aswan kwa ajili ya Amani na Mendeleo Endelevu;

10. **UNASISITIZA HAJA** ya utekelezaji wa haraka na kamili wa Azimio 2719(2023) la Baraza la Usalama la UN, ili kuhakikisha ufadhili wa Shughuli za kuleta amani zinazoongozwa na AU, pamoja na haja ya kuchunguza njia za ubunifu za kukusanya rasilimali za fedha za ndani, ikiwa ni pamoja na kupitia ushirikiano na sekta binafsi na taasisi za fedha za Afrika (Bara);

11. **AIDHA UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kukuza ushirikiano na kutafuta fursa za kiuchumi, hususan, uwezeshaji wa biashara na miundombinu inayovuka mipaka, ili kuimarisha utangamano wa kikanda, jambo ambalo ni muhimu kwa uimarishaji wa amani na usalama katika Bara;

12. **UNAHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha mamlaka ya nchi na kuanzisha uwepo mzuri wa serikali katika maeneo yao ya kitaifa na kuimarisha taasisi za serikali, kwa nia ya kuepuka ombwe ambalo linaweza kutumiwa na makundi ya uhalifu, yenye silaha na ya kigaidi kusababisha ukosefu wa utulivu kiuchumi, kijamii na kiusalama;

13. **AIDHA UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuimarisha uwezo wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na lakini sio tu kujenga vikosi vya kijeshi vya kitaifa vyenye nguvu na utaalamu ambavyo vina itikadi sahihi ya kutokuwa na udini na utaifa, ili pamoja na mambo mengine, kulinda na kutetea uadilifu wa Serikali na kuushinda ugaidi;

14. **UNASISITIZA HAJA** ya Nchi Wanachama kuandaa taratibu, zikiwemo katika ngazi ya kikanda, kwa ajili ya kushughulikia vyanzo vya ufadhili wa ugaidi ili kupunguza shughuli za makundi ya kigaidi na yenye silaha, ukibainisha kuwa bila chanzo endelevu cha ufadhili, makundi ya kigaidi na yenye silaha yasingeweza kufanya shughuli zao;

15. **UNASISITIZA UMUHIMU** kwa Nchi Wanachama, RECs/RMs na taasisi za AU, kuongeza juhudi katika kuingiza ushiriki wa wanawake na vijana, pamoja na asasi za kiraia, kama mawakala wa mabadiliko, kwenye ngazi zote katika utekelezaji wa AUMR;

16. **UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama, RECs/RMs na wadau wengine kuhakikisha utekelezaji mzuri wa maamuzi yote ya Mkutano Mkuu na PSC kuhusu masuala ya amani na usalama, huku hasa, kuharakisha utekelezaji wa Azimio la Malabo kuhusu Ugaidi na Mabadiliko yasiyo ya Kikatiba ya Serikali lililopitishwa na Mkutano maalumu wa 16 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU uliofanyika tarehe 28 Mei 2022, mjini Malabo, Equatorial Guinea;

17. **UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kutekeleza Azimio la Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Kupambana na Ugaidi Afrika, uliofanyika kuanzia tarehe 22 hadi 23 Aprili 2024, mjini Abuja, Nigeria chini ya kaulimbiu; "Kuimarisha Ushirikiano wa Kikanda na Ujenzi wa Taasisi ili Kukabiliana na Tishio Linaloendelea la Ugaidi Barani Afrika";

18. **UNAZINGATIA** Hitimisho la Toleo la 3 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Kutokuwa ana vurugu, Biennial of Luanda, lililofanyika tarehe 22 na 23 Novemba 2023 chini ya kaulimbiu: "Elimu; Utamaduni wa Amani; Uraia kama Nyenzo za Maendeleo ya Bara", na unaweza kutaka kuhimiza ushiriki wa Nchi

Wanachama na RECs/RMs katika Toleo la 4 litakalofanyika mwaka 2025 chini ya kaulimbiu: "Kuheshimu Yaliyopita; Kuthamini Mafanikio Yetu; na Kujenga Afrika Tunayoitaka", kama nyenzo muhimu ndani ya mfumo wa utekelezaji wa Mwongozo Mkuu wa AU wa Hatua za Kivitendo za Kusitisha Mapigano Barani Afrika ifikapo 2030**;**

**19.** **UNASISITIZA HAJA** ya kuimarisha diplomasia ya kuzuia mgogoro kama nyenzo madhubuti ya kuzuia, kusimamia na kutatua migogoro na, katika suala hili, unasisitiza haja ya kutumia nyenzo zote zilizopo, zikiwemo Ofisi Bora za Mwenyekiti wa Kamisheni, Jopo la Wenye Busara, FEMWISE, Youth-Wise, Wajumbe Maalum, Jukwaa la I-RECKE na N NETT4Peace;

**20.** **UNAIAGIZA** Kamisheni kuitisha jukwaa la tafakuri la ngazi ya juu mwaka 2025 (ikiwa ni miaka mitano tangu kuongezwa kwa utekelezaji wa Mwongozo Mkuu wa AU) ili kutathmini kwa kina maendeleo yaliyofikiwa na changamoto katika utekelezaji wa Mwongozo Mkuu wa AU wa Kusitisha Mapigano Barani Afrika; huku ukisisitiza kuwa jukwaa hilo pia litatoa fursa kwa Nchi Wanachama na wadau wengine muhimu kubadilishana uzoefu, mafunzo na mbinu bora katika utatuzi wa migogoro na ukuzaji wa amani, usalama na maendeleo katika Bara; na

**21.** **UNAIOMBA** Kamisheni kuunda mfumo sanifu wa utoaji ripoti kwa Nchi Wanachama na wadau wengine ifikapo 2026, kulingana na Jedwali la Ufuatiliaji na Tathmini la AUMR.

# UAMUZI
# KUHUSU RASIMU YA MKATABA WA MAELEWANO KATI YA UMOJA WA AFRIKA NA JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KIKANDA NA TAASISI ZA KANDA KUHUSU MATUMIZI YA KIKOSI CHA DHARURA CHA AFRIKA
# - Doc. Assembly/AU/6(XXXVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNATHIBITISHA TENA** jukumu la Kikosi cha Dharura cha Afrika kama chombo muhimu cha kukuza amani, usalama na utulivu barani Afrika, kwa kuzingatia Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika na Protokali ya uanzishwaji wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika;

**2. UNAZINGATIA** Uamuzi EX.CL/Dec.1220(XLIII) wa tarehe 20 Julai 2023 kuhusu ripoti za mikutano ya kawaida ya 15 na 16 ya Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Ulinzi na Usalama (STCDSS) ya Mei 2023 na Juni 2024 mtawalia, ambayo ilipendekeza kupitishwa na Mkutano Mkuu kwa Mkataba wa Maelewano kati ya AU na RECs/RMs kuhusu matumizi ya Kikosi cha Dharura cha Afrika.

**3. UNAREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Des.869(XXXVII) wa Februari 2024, ulioahirisha kujadiliwa kwa rasimu ya mkataba wa maelewano kati ya AU na RECs/RMs kuhusu matumizi ya Kikosi cha Dharura cha Afrika wakati wa Mkutano wa 38 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Februari 2025;

**4**. **UNAIOMBA** Kamisheni kuharakisha na kupanua mchakato wa mashauriano kuhusu kujadiliwa kimkakati na ASF kujumuisha PSC, Nchi Wanachama, RECs na RM zote pamoja na Vituo vya Ubora vya Afrika vilivyoidhinishwa na AU; na kuharakisha mchakato wa uandaji wa mwongozo wa jumla na jumuishi kwa ajili ya kujadiliwa kwa kina kwa ASF na kuwasilisha ripoti yake kwenye mkutano wa 17 wa STCDSS na kwenye Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali, Februari 2026; na

5. **UNAREJELEA** mchakato unaoendelea wa kukamilisha Mkataba wa Maelewano na **KUSISITIZA** haja ya kuukamilisha katika Mkutano wa 39 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Februari 2026.

# UAMUZI KUHUSU
# RIPOTI YA USHIRIKI WA AU KWENYE G20 ILIYOWASILISHWA NA MWENYEKITI WA UMOJA WA AFRIKA, AKISAIDIWA NA MWENYEKITI KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA– DOC. BUNGE/AU/7 (XXXVIII)

UAMUZI KUHUSU TARATIBU ZILIZOREKEBISHWA ZA USHIRIKI WA UMOJA WA AFRIKA KATIKA MIKUTANO YA MAWAZIRI YA G20 NA MIKUTANO YA KITENGO CHA FEDHA CHA G20

**Mkutano Mkuu**,

**UKIREJELEA** Uamuzi Assembly/AU.Dec.845(XXXVI) unaoeleza kuwa Mwenyekiti wa sasa wa AU akisaidiwa na Mwenyekiti wa Kamisheni ataiwakilisha AU katika Mikutano Mikuu ya Viongozi wa G20;

**UKIREJEA PIA** Uamuzi Assembly/AU.Dec.873 (XXXVII) kuhusu Taratibu za Ushiriki wa Umoja wa Afrika katika G20 na Vipaumbele vya Awali vya kufuatwa ambao unaeleza ushiriki wa AU katika mikutano wa mawaziri kwamba: Mwenyekiti wa Baraza Kuu, atasaidiwa na Mwenyekiti wa Kamisheni kuiwakilisha AU kwenye Mikutano ya G20 ya Mawaziri wa Mambo ya Nje; Wenyeviti wa Kamati Maalumu za Kitaalamu za AU, watasaidiwa na Makamishna husika, kuongoza ujumbe wa AU kwenye Mikutano ya Mawaziri ya Kisekta; na kwamba Mwenyekiti wa STC ya Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano atasaidiwa na Kamishna wa Maendeleo ya Kiuchumi, Biashara, Utalii, Viwanda na Madini kuwakilisha AU kwenye mikutano ya Mawaziri wa Fedha wa G20 na Magavana wa Benki Kuu;

**UKIREJELEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU.Dec.873 (XXXVII) kuhusu Taratibu za Ushiriki wa AU katika G20 na Vipaumbele vya Awali vya kufuatwa ambao unaeleza kuwa taratibu zitapitiwa baada ya mwaka mmoja wa kushiriki katika G20;

1. **UNAKARIBISHA NA KUZINGATIA** Ripoti ya Mwenyekiti kuhusu Ushiriki wa AU katika G20 kwa mwaka 2024 iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania na Mwenyekiti wa AU mwaka 2024;

2. **UNAZINGATIA** changamoto katika kupata ushiriki wa Wenyeviti wa STC katika mikutano ya G20 na athari kubwa jambo hilo iliyo nayo katika uelezaji wa misimamo ya Umoja wa Afrika katika mikutano hiyo;

3. **UNAZINGATIA ZAIDI** ukosefu wa sauti ya AU katika majadiliano ya G20 kuhusu masuala ya fedha kutokana na ukweli kuwa Benki Kuu ya Afrika bado haijaanzishwa;

4. **UNAAMUA ZAIDI** kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Fedha ya Afrika, pale itakapokuwa inafanya kazi, na ikisubiriwa kuanzishwa kwa Benki Kuu ya Afrika, atakuwa sehemu ya ujumbe wa AU kwenye mikutano ya Kitengo cha Fedha cha G20.

5. **UNAAMUA** kwamba Ripoti ya Mwenyekiti kuhusu Ushiriki wa AU katika G20 kinapaswa kuwa kipengele cha kudumu chini ya kipengele cha ajenda kuhusu ripoti za kimkakati;

6. **UNAZITAKA** Nchi zote Wanachama wa AU kuunda na kuhifadhi kumbukumbu ya kitaasisi kwenye G20;

7. **UNAZITAKA ZAIDI** Nchi zote Wanachama wa AU kufuatilia na kutekeleza ahadi za Azimio la Viongozi wa G20 la Rio de Janeiro;

8. **UNAZIPONGEZA** Benki ya Maendeleo ya Afrika na benki ya *African Export and Import Bank* kwa kutimiza ahadi zao za kutoa rasilimali fedha ili kusaidia ushiriki wa AU katika G20*, na* **UNAZIALIKA** Taasisi zingine za Fedha za Kimataifa za Afrika kutoa michango kama hiyo; na,

9. **UNAAHIDI** kuunga mkono kikamilifu Urais wa G20 wa Afrika Kusini kwa mwaka 2025.

## UAMUZI
## KUHUSU RIPOTI KUHUSU MAGEUZI YA KITAASISI YA UMOJA WA AFRIKA ILIYOTOLEWA NA MHE. WILLIAM RUTO, RAIS WA JAMHURI YA KENYA

Mkutano Mkuu,

**UKIZINGATIA** Ibara ya 9 (1) (a) ya Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika kuhusu mamlaka na kazi za Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika kuainisha sera za Umoja wa Afrika na ulazima wa kuzingatia Maamuzi ya Mkutano huo;

**UKIREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Des.635(XXVIII) wa Januari 2017 na kuanzishwa kwa mchakato wa mageuzi ya kitaasisi ya Umoja wa Afrika (AU);

**UKIREJELEA PIA** uamuzi Assembly/AU/Des.635(XXVIII) aya ya 5 (c) (i) kuhusu usimamizi wa kisiasa wa Umoja wa Afrika: Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika utashughulikia ajenda ya mambo yasiyozidi matatu ya kimkakati katika kila Mkutano kwa mujibu wa mapendekezo ya Mkutano wa Mawaziri wa Mekelle. Shughuli nyingine mahususi zitakabidhiwa kwa Baraza Kuu;

**UKIREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Des. 866(XXXVII) wa Februari 2024, uliomteua Mhe. Rais William Samoei Ruto (PhD), Rais wa Jamhuri ya Kenya kuwa Kinara mpya wa AU kuhusu Mageuzi ya Kitaasisi, na **UKIZINGATIA** kwa kuridhishwa na ripoti ya maendeleo ya 2025 kuhusu mageuzi ya kitaasisi ya AU.

**UKISISITIZA** haja ya kutekeleza Uamuzi EX.CL/Dec.893(XXVII) wa Juni 2015 kuhusu kiwango cha tathmini na utekelezaji wa vyanzo mbadala vya kufadhili Umoja wa Afrika na uamuzi Assembly/AU/Dec.605(XXVII) wa Juni 2016 kuhusu ufadhili wa Umoja wa Afrika;

**UNAMPONGEZA** Kinara kwa kujitolea kwake katika uendeshaji wa mchakato wa mageuzi na **UNAAMUA** kama ifuatavyo:

1. **KUPITISHA** ripoti ya maendeleo ya 2025 kuhusu Mageuzi ya Kitaasisi ya AU iliyowasilishwa na Mhe. William Samoei Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, Kinara wa mageuzi ya Kitaasisi ya AU yanayohusiana na urekebishaji wa vyombo, taasisi, mashirika na ofisi za AU zilizosalia na mgawanyo wa kazi kati ya AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda, Taasisi za Kikanda na Nchi Wanachama pamoja na masuala mengine yanayohusu mageuzi;

### A. Kuhusu urekebishaji wa Mashirika, Taasisi na Ofisi za AU zilizobaki

2. **UNAIELEKEZA** PRC, kwa msaada wa AUC, kuhitimisha mapitio yake ya mchakato wa urekebishaji wa Mashirika, taasisi na ofisi za AU zilizosalia na **KUWASILISHA** ripoti kwa Baraza Kuu wakati wa Mkutano wake wa Julai 2025.

### B. Kuhusu mgawanyo wa Kazi kati ya AU, RECs, RMs na Nchi Wanachama

**3. UNAIAGIZA** AUC, wadau husika wa AU, RECs, RMs na Nchi Wanachama kuharakisha kujadiliwa kwa Utafiti kuhusu Mgawanyo wa Kazi kati ya AU, Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs), na Nchi Wanachama na kuwasilisha mapendekezo katika Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka (MYCM) mwezi Julai 2025.

**C. Kuhusu uangalizi wa Mageuzi ya AU:**

4. **KUANZISHA** Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya kusimamia Mageuzi ya AU, chini ya uongozi wa Kinara wa Mageuzi wa AU Mhe. Rais Ruto wa Jamhuri ya Kenya. Kamati itadumisha kasi ya kisiasa, kutoa uangalizi na mwongozo na kuongoza utekelezaji wa mchakato wa mageuzi ya AU Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya Uangalizi wa Mageuzi ya AU itaundwa na wajumbe kumi (10) kama ifuatavyo:

a) Wakuu Watano wa Nchi na Serikali, akiwemo Kinara wa Mageuzi ya AU, kutoka kanda mitano;
b) Wajumbe watano (5) wa Ofisi ya Wakuu wa Nchi na Serikali.

**5. KUFANYA** Mkutano Maalumu wa Mageuzi ya AU mwezi Julai 2025. Kabla ya kufanyika kwa mkutano huu, Kamisheni itafanya mashauriano ya mwisho na wadau wa AU na kutoa mapendekezo madhubuti kwenye Mkutano huo kwa ajili ya awamu ya mwisho ya Mageuzi.

**D. Kuhusu Ajenda ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU:**

**6. KUIELEKEZA** Kamisheni kuwasilisha mapendekezo madhubuti kwa kuzingatia utekelezaji wa Uamuzi Assembly/AU/Des.635 (XXVIII) 5(c) (i) unaotamka kwamba "Umoja wa Afrika utashughulikia ajenda zisizozidi mambo matatu (3) ya kimkakati katika kila Mkutano" na kuwasilisha mkakati wa utekelezaji kwa Wakuu wa Nchi na Serikali na Kamati ya Usimamizi kwa ajili ya Mageuzi ya AU kabla ya mwezi Juni 2025.

**E. Kuhusu uainishaji wa Maamuzi**

7. **KUIELEKEZA** Kamisheni kuanzisha, bila kucheleweshwa, kuainisha maamuzi ya Mkutano Mkuu na Baraza Kuu kwa mujibu wa Uamuzi Assembly/AU/Des. 687(XXX) wa Januari 2018.

**F. Kuhusu Amani na Usalama:**

**UKIZINGATIA KWA MASIKITIKO** kuhusu kuongezeka kwa vitishio na changamoto na mabadiliko ya haraka ya mazingira ya kiusalama ya kimataifa na bara ambayo yamezuia mfumo wa sasa wa amani na usalama wa AU.

**UKISISITIZA** kwamba amani na usalama ni sharti muhimu kwa ushirikiano na maendeleo ya bara.

**8. UNAMRUHUSU** Mwenyekiti wa Kamisheni ya AU kwa kushauriana na Kinara kuteua Jopo la Ngazi ya Juu linalojumuisha Wataalamu watano Mashuhuri wa Afrika, ili kupitia upya Mfumo wa Amani na Usalama wa AU ndani ya miezi minne ijayo.

**9. UNAMUOMBA** Kinara wa AU kuhusu Mageuzi ya Kitaasisi kuripoti kwenye Mkutano Maalumu wa AU baada ya kufuata utaratibu unaostahili.

**G. Kuhusu Kufadhili Umoja wa Afrika:**

**UKIREJELEA** uamuzi Assembly/AU/Des. 578(XXV) wa 2015 na Uamuzi Assembly/AU/Des. 605 (XXVII) wa 2016;

**UKIKARIBISHA** maendeleo yaliyofikiwa kuhusu mageuzi ya ufadhili ya AU hasa kuhusiana na utawala wa kifedha na ufufuaji wa Mfuko wa Amani wa AU;

**UKIZINGATIA KWA MASIKITIKO** kwamba uhuru wa kimkakati wa kifedha na uhuru bado haujapatikana. Malengo yaliyowekwa katika Uamuzi Assembly/AU/Des. 578(XXV) na Assembly/AU/Des. 605(XXVII) haijatekelezwa kikamilifu. Nchi Wanachama wa AU hufadhili 24% tu ya bajeti ya programu. Bajeti ya Operesheni za Msaada wa Amani bado ni tegemezi kwa washirika wa nje;

**UKITAMBUA** Nchi Wanachama wa AU ambazo zimetekeleza kikamilifu Uamuzi wa Kigali wa Ufadhili wa 0.2%;

**UNAKARIBISHA** ufufuaji wa Mfuko wa Amani wa AU ambao umefikia kiwango kamili cha dola 400m;

10. **UNAMWOMBA** Mwakilishi Mkuu wa AU wa Kufadhili Umoja wa Afrika kufanya mashauriano kuhusu maendeleo yaliyofikiwa katika Ufadhili wa jumla wa Umoja wa Afrika kama ifuatavyo:

a) kutambua vikwazo vya utekelezaji kamili wa maamuzi ya Johannesburg na Kigali na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na changamoto hizi;

b) kutathmini changamoto za kuchangiwa kwa Mfuko wa Amani wa AU na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuongeza ufanisi wa matumizi na ufanisi wa Mfuko;

c) kutathmini viwango vya mapato ya Mfuko kulingana na malengo ya Mfuko na vipaumbele vya sasa vya amani na usalama na kutoa mapendekezo.

11. **UNAMWOMBA PIA** Mwakilishi Mkuu kuwasilisha ripoti kwenye Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa mwezi Julai 2025.

12. **AIDHA UNALIOMBA** Baraza Kuu liitishe Mkutano Maalumu wa Baraza Kuu, utakaowakutanisha Mawaziri wa Mambo ya Nje na Mawaziri wa Fedha wa Nchi

Wanachama ili kuimarisha ufadhili wa Umoja wa Afrika na Mfuko wa Amani, kwa kuzingatia Uamuzi Assembly/AU/Des.687 (XXX) wa Januari 2018.

**H. Kuhusu uendeshaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika:**

**UKIREJELEA** Mkutano wa Pili wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Maputo, Msumbiji, tarehe 11 Julai 2003, ambaco ulipitisha Protokali ya Mahakama ya Umoja wa Afrika iliyoanza kutumika tarehe 11 Februari 2009;

**UKIZINGATIA** kwamba Protokali ya Mkataba wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu, iliyopitishwa tarehe 1 Julai 2008 huko Sharm El-Sheikh, Misri, ambayo inataka kuunganisha Mahakama hizo mbili na kuanzisha Mahakama moja, bado haijaanza kutumika;

**UKIZINGATIA ZAIDI** kwamba Marekebisho ya Protokali ya Sheria ya Mahakama ya Haki za Binadamu iliyoanzisha mahakama ya uhalifu iliyopitishwa Juni 2014 huko Malabo, Equatorial Guinea, bado hayajaanza kutumika.

**UNAREJELEA PIA** Uamuzi Assembly/AU/Des.757(XXXIII) wa Februari 2020 kuhusu Usimamizi wa Matokeo na Wajibu wa Uangalizi wa Mwenyekiti wa Kamisheni ndani ya Umoja wa Afrika kuhusu Utendaji wa Kamisheni na Vyombo vingine vya AU, ambao uliitaka Kamisheni kuwasilisha ripoti ya utendaji kazi wa Mahakama iliyopewa mamlaka ya kushughulikia rufaa kutoka kwenye Mahakam ya Utawala ya AU.

**UKITAMBUA** umuhimu mkubwa wa uendeshaji wa Mahakama ya Umoja wa Afrika ili kufikia malengo ya Umoja huo na kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi.

**13. UNAAMUA** kwamba kabla ya Mahakama kuanza kufanya kazi, Kamisheni, PRC na wadau husika lazima waonyeshe athari za kisheria, kimuundo na kifedha za uendeshaji wa Mahakama na kuwasilisha ripoti yake kwa Baraza Kuu wakati wa Mkutano wake ujao wa Kawaida mnamo Julai 2025. Athari za kisheria za uendeshaji wa Mahakama zinahitaji uchambuzi wa kina wa Mahakama kutokana na suala lijalo la Mahakama na AfCHPR

**I. Kuhusu maboresho ya Bunge la Afrika**

14. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kuridhia Protokali ya Malabo ya Julai 2014, ambayo inahitaji uridhiaji wa nchi 28 ili kuanza kutumika, ambapo uridhiaji wa nchi kumi na tatu (13) bado unahitajika.

15. **UNAMWOMBA** Kinara kutoa taarifa ya utekelezaji wa Uamuzi huu na Uamuzi Assembly/AU/Des.866(XXXVII) wa Februari 2024 katika Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Februari 2026 na **UNAMWAGIZA** Mwenyekiti wa Kamisheni na Kitengo cha Utekelezaji wa Maboresho ili kumsaidia Kinara katika majukumu yake;

16. **UNAAMUA** kushughulikia suala hilo.

# UAMUZI KUHUSU RIPOTI ZA JUKWAA LA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WANAOSHIRIKI KATIKA MPANGO WA KUJITATHMINI KIUTAWALA BORA (JUKWAA LA APRM) YA MHE. ABDELMADJID TEBBOUNE RAIS WA JAMHURI YA KIDEMOKRASIA WA WATU WA ALGERIA NA MWENYEKITI WA MPANGO WA KUJITATHMINI KIUTAWALA BORA AFRIKA (APRM) – Doc. Assembly/AU/10 (XXXVIII)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Ripoti ya Mkutano wa 3 wa Dharura na Mkutano wa Kawaida wa 34 wa Mpango wa Afrika wa Kujitathmini wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Nchi Wanachama wa Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Afrika (Kamati ya APR) uliofanyika tarehe 14 Februari 2025;

2. **UNAMPONGEZA** MHE. Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti wa Kamati ya APRM kwa uongozi wake mzuri wa APRM na kujitolea kwake bila kutetereka katika kuendeleza demokrasia na utawala bora katika bara;

3. **UNAKARIBISHA KWA SHUKRANI KUBWA** mchango wa hiari wa APRM wa kiasi cha Dola milioni 1 zilizotolewa na MHE. TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kwa niaba ya Serikali na watu wa Algeria; UNAMSIFU Rais TEBBOUNE kwa kujitolea huku kwa uthabiti kunakolenga kuhakikisha umiliki kamili wa APRM kwa Nchi Wanachama;

4. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.874(XXXVII), uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa Kawaida wa 37 uliofanyika mwezi Februari 2024 mjini Addis Ababa, Ethiopia, ambapo Mkutano Mkuu uliunga mkono uamuzi wa Kamati ya APRM inayoipa mamlaka Sekretarieti ya APRM kuandaa, pamoja na Kamati ya Wataalamu ya APRM na Kamisheni katika Mkutano Mkuu wa 3 wa Dharura wa APRM kutokana na maombi ya Jamhuri ya Zambia;

5. **UNAREJEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU/Dec.758(XXXIII) uliopitishwa na Mkutano wa Kawaida wa 3 wa Mkutano Mkuu wa UA uliofanyika Februari 2020 ambapo Mkutano Mkuu ulipitisha Sheria za APRM na Kanuni za Uendeshaji za Wakuu wa Nchi na Serikali wanachama wa APRM;

6. **UNAREJEA ZAIDI** Ibara ya 11 (1) ya Katiba ya APRM ambayo inaeleza kwamba Kamati ya APRM itakuwa chombo cha juu cha uamuzi cha APRM, ambacho kinatoa uongozi wa kisiasa na mwongozo wa kimkakati kwa APRM na kuwa kama Kamati Ndogo ya Mkutano Mkuu na Ibara ya 11 (8) ya Katiba ya APRM ambayo inaeleza kwamba Kamati ya APRM itakutana mara moja kwa mwaka katika mkutano wa kawaida ili kujadili ripoti za tathmini za Nchi wanachama wa

APRM, kufanya tathmini ya nchi na kufanya uamuzi mwingine kuhusu usimamizi na utekelezaji wa mamlaka ya APRM;

7. **UNARIDHISHWA KWA KIASI KUBWA** kuitishwa kwa Mkutano Mkuu Maalumu wa 3 wa APRM kulingana na Uamuzi Assembly/AU/Dec.874(XXXVII), na Ibara ya 11 (1) (8) ya Sheria za APRM pamoja na vifungu husika vya Kanuni za Uendeshaji wa Kamati ya APRM;

8. **UNASISITIZA** kwamba APRM ribakie kuwa chombo cha kwanza cha utawala bora kinachoongozwa na Afrika, na kumilikiwa na Afrika kilichoanzishwa mwaka 2003 na kimekubaliwa ka hiari na Nchi Wanachama wa UA arobaini na tano zinazowakilisha Zaidi ya theluthi mbili ya wanachama wa UA;

9. **UNAPONGEZA KWA KURIDHIKA** na kukamilika kwa kipindi cha mpito katika APRM na **UNATOA** shukrani zake kwa aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, Profesa Eddy Maloka, kwa kushughulikia kitaalamu na kusimamia kipindi cha mpito cha APRM;

10. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.887(XXXVII) uliopitishwa na Mkutano Mkuu wa 37 uliofanyika Februari, 2024 ambapo Mkutano Mkuu ulimchagua Balozi Marie Antoinette Rose-Quatre kuwa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM kuanzia tarehe 3 Juni 2024 na kwa kipindi cha miaka minne (4) kinachoweza kurudiwa mara moja; na kuielekeza Sekretarieti ya APRM, kwa kusgirikiana na Kamisheni ya UA, kuandaa kiapo cha Mtendaji Mkuu mpya aliyechaguliwa;

11. **UNAIPONGEZA** Sekretarieti ya Bara ya APRM na Kamisheni ya UA kwa utekelezaji wenye mafanikio wa Uamuzi Assembly/AU/Dec.887(XXXVII;

12. **UNAMSHUKURU SANA** MHE. Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Algeria na Mwenyekiti wa Kamati ya APR, kwa maandalizi yenye mafanikio ya sherehe za kuapishwa kwa Balozi Marie Antoinette Rose-Quatre kuwa Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, tarehe 20 Novemba, 2024 huko Algiers, Algeria;

13. **UNAKARIBISHA KWA SHUKRANI** Ripoti ya tathmini ya utawala bora ya Jamhuri ya Zambia, **UNAMPONGEZA** MHE. Hakainde Hichilema, Rais waJamhuri ya Zambia kwa uongozi wake madhubuti na unaokubalika katika kuendeleza utawala bora katika nchi yake kwa kufanya Tathmini ya Nchi ya Kipindi cha Pili;

14. **UNATAMBUA KWA KUTHAMINI** Ripoti za tathmini Zilizolengwa za Jamhuri ya Senegali kuhusu rasilimali za madini katika kipindi cha mageuzi ya uchumi ya Wasenegali;

15. **UNAMPONGEZA** MHE. Bassirou Diomaye FAYE, Rais wa Jamhuri ya Senegali kwa kujitolea kwa nia njema ya utawala bora pamoja na matukio yake yote matano, ikiwa ni pamoja maendeleo mapana na endelevu ya kiuchumi na kijamii na kujitolea bila kuchoka kwa ajili ya mabadiliko ya kiuchumi ya nchi yake na bara;

16. **UNAMTIA MOYO** MHE Hakainde HICHILEMA, Rais wa Jamhuri ya Zambia na MHE. DIOMAYE FAYE, Rais wa Jamhuri ya Senegali fkwa kufanikiwa kukamilisha tathmini; NA kuwahamasisha kuchukua hatua ya pamoja katika kuandaa Programu za Utekelezaji za Taifa ili kutekeleza matokeo na mapendekezo ya ripoti zao; **UNAWAOMBA** kulinganisha program hizo na Ajenda ya UA ya 2063, hususan Mpango wake wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka 10;

17. **UNAUNGA MKONO** Jopo la APR la Watu Mashuhuri kwa uongozi wake wa mfano katika kufanya Tathmini ya Hatua ya pili ya Zambia na tathmini iliyolengwa ya Senegali; na kwa kuweka viwango vya juu Zaidi vya uadilifu, uaminifu, weledi wa kitaalamu, utaalamu na kujitegemea wakati wote wa mchakato wa tathmini;

18. **UNAZIHAMASISHA** Nchi wanachama wa APRM ambazo bado hazijajifanyia tathmini kuchukua hatua muhimu za kufanya tathmini ya nchi na kuhakikisha ripoti zao zinawasilishwa katika Kamati ya APRM**; UNAZIOMBA** kulingana na Uamuzi uliopita wa Mkutano Mkuu, Nchi Wanachama wote wa UA ambazo bado hazijajiunga na APRM kukubaliana na Utaratibu ili kuharakisha ufanikishaji wa haraka wa Ajenda ya 2063, Afrika Tunayoitaka;

19. **UNAZIOMBA ZAIDI** Nchi Zinazodhiriki APRM ambazo zimeshatathminiwa kutekeleza Mipango yao ya Utekelezaji ya Taifa na mapendekezo ili kueleza marekebisho ya taasisi katika ngazi ya taifa na kuzuia changamoto zilizoelezwa kwenye ripoti zao za tathmini ya nchi;

20. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** Ripoti za Maendeleo za Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Cote d'Ivoire kuhusu utekelezaji wa Ripoti za tathmini ya Nchi;

21. **UNAMPONGEZA NA KURIDHISHWA na** MHE. William Samoei RUTO, Rais wa Jamhuri ya Kenya na MHE. Alassane OUATTARA, Rais wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire, kwa uongozi wao uliotukuka na jitihada za bila kuchoka katika kuimarisha utawala katika nchi zao;

22. **UNASISITIZA** upatikanaji kikamilifu wa Utaratibu wa kuendelea kutoa msaada wake kwa Kenya na Côte d'Ivoire kwa nia ya kuimarishamafanikio ya kidemokrasia na utawala bora;

23. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.874. (XXXVII) unaoielekeza Sekretarieti ya Bara ya APRM, kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni ya

Umoja wa Afrika, kuandaa na kuwasilisha kwa Mkutano Mkuu katika mkutano wa kawaida ujao kwa ajili ya kuidhinishwa, vigezo vya wazi vya uchaguzi na uteuzi wajumbe wa Jopo wa APR na kuweka vigezo vya muda maalumu katika uchaguzi na uteuzi wa Wajumbe wapya wa Jopo hadi vigezo vya wavi vitakapokuwa vimeandaliwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa UA; **UNAPITISHA** vigezo vya uchaguzi na uteuzi wa Wajumbe wa Jopo la APR na kuielekeza APRM kuhakikisha utekelezaji wake wa haraka;

24. **UNATOA SHUKRANI ZA DHATI** kwa wajumbe wa Jopo la APRM waliomaliza muda wao, Balozi Inonge Mbikusita-Lewanika, Dkt Ousmane Diallo, na Dkt. Honore Mobonda fkwa utendaji wao wa mfano wakati wa kipindi cha uongozi wao; **UNAIELEKEZA** APRM kuanzisha mara moja mchakato wa kuteua wajumbe wapya katika Jopo la APR la Watu Mashuhuri, kwa kufuata kikamilifu vigezo vilivyoidhinishwa, ili kuhakikisha Jopo lililoundwa kikamilifu linawekwa na kufanya kazi ifikapo Februari 2026.

25. **UNAKARIBISHA KWA SHUKRANI** uteuzi wa Kamati ya APR, BaloziEl-Henfy Houssam El Din, anawakilisha Afrika ya Kati kama Mwenyekiti Anayeingia madarakani wa Jopo la APR la Watu Mashuhuri na Balozi Ali Ahmed Araita, Anawakilisha Afrika Mashariki kama Makamu Mwenyekiti anayeingia madarakani wa Jopo la kwa mwaka 2025;

26. **UNAZINGATIA** umuhimu wa utawala wa kutumia teknolojia ya habari kwa ajili ya kuongeza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Nchi Wanachama na umuhimu wake katika kuharakisha ufanikishaji wa Ajenda 2063; **UNAPITISHA** mapendekezo ya Kamti kwa Utawalam kkupitia teknolojia ya habari (E-governance) kuwa eneo la sita maalumu la mchakato wa tathmini ya APRM;

27. **UNATAMBUA KWA KURIDHIKA** hatua zilizochukuliwa katika kuhakikisha mafanikio yanayofaa ya APRM katika kutekeleza mamlaka yake kwa matokeo yanayoonekana;

28. **UNAZIOMBA** Nchi Zinazoshiriki APRM pia kufikiria kutoa michango ya hiari kwa APRM na zile ambazo bado zina madeni kuyalipa ili kuhakikisha umiliki wa kweli wa APRM wa Nchi Wanachama na utekelezaji wa mamlaka yake kwa matokeo yanayoonekana;

29. **UNAMPONGEZA KWA SHUKRANI** Mwenyekiti wa Kamisheni MHE. Moussa Faki na Mtendaji Mkuu wa Sekretarieti ya Bara ya APRM, Balozi Marie-Antoinette Rose Quatre, kwa uongozi wake wa ushirikiano na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika miezi minane (8) iliyopita, ambayo inaonyesha kujituma kwao katika kuiwezesha APRM kutekeleza mamlaka yake ipasavyo na bila ya kizuizi; **UNAPITISHA** kwa kuridhika Ripoti ya Mwaka 2024 ya APRM na kutoa wito kwa Sekretarieti ya Bara ya APRM kuhakikisha inasambazwa kwa kiasi kikubwa;

30. **UNASISITIZA** Uamuzi wake Ext/Assembly/AU/Dec.1-4(XI) wa Novemba, 2018 ambapo Mkutano Mkuu ulisisitiza tena haja ya kuimarisha uwezo wa APRM wa kuhudumia katika mamlaka yake yaliyoongezwa na kuendeleza kazi yake ya kujitawala;

31. **UNASISITIZA** haja ya APRM kupatiwa rasilimali watu wa kutosha na wenye ufanisi na mgao wa bajeti ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo na bila ya kizuizi;

32. **UNAZINGATIA KWA KURIDHIKA** utekelezaji kamili wa Mpango wa Pili wa Kimkakati wa APRM wa APRM 2020-2024, na **UNAIPONGEZA** APRM kwa kutimiza maeneo yake yote muhimu ya kipaumbele; **UNAIDHINISHA** Mpango wa Utekelezaji wa Tatu wa APRM wa 2025-2028;

33. **UNAIPONGEZA** APRM kwa kuhakikisha kwamba Mpango Mkakati wa Tatu unawianishwa na Ajenda ya UA ya 2063 na Mpango wa Utekelezaji wa Pili wa Miaka Kumi, Mpango Mkakati Mpana wa UA na Matokeo ya Utafiti ya APRM na kutumia mkabala wa UA wa kadi ya matokeo kunaongeza katokeo ya ufuatiliaji na athari;

34. **UNAAHIDI** kuisaidia APRM ili kuhakikisha utekelezaji kikamilifu wa Mpano wa tatu wa Utekelezaji; **UNAIHIMIZA** APRM kuchukua hatua muhimu ili kufanikisha maeneo muhimu ya kipaumbele ya Mpabgo Mkakati wa tatu wa APRM 2025-2028 wa APRM;

35. **UNAREJEA** Uamuzi wake Assembly/AU/Dec.874(XXXVII) wa Februari, 2024, ambapo Mkutano Mkuu ulisisitiza umuhimu wa Ushirikiano wa Kubadilishana maarifa na kujifunza katika kuendeleza utawala bora na mabadiliko ya kiuchumi katika bara; na ahadi ya Jamhuri ya Sierra Leone ya kuwa mwenyeji wa Mkutano wa tatu wa Viongozi wa Ngazi ya Juu Afrika kuhusu Ushirikiano wa Kubadilishana Maarifa na kujifunza kwa ajili ya maendeleo endelevu;

36. **UNATAMBUA NA KURIDHISHWA** na jitihada za Serikali ya Sierra Leone kuwa mwenyeji wa Mkutano wa tatu wa Viongozi wa Ngazi ya Juu kuhusu Ushirikiano wa Kubadilishana maarifa na kujifunza kwa ajili ya maendeleo endelevu mwaka 2025; **UNAPITISHA** kaulimbiu "Kuendeleza Utawala Bora na Uhimilivu wa Kiuchumi ili kuendeleza Utangamano wa Afrika na Ajenda ya 2063" kama hatua muhimu katika kuimarisha malengo ya maendeleo;

37. **UNASISITIZA** Uamuzi wake Assembly/AU/Dec.631(XXVIII), wa Januari, 2017 ambapo Mkutano ulikaribisha ahadi ya kuipa nguvu mpya Tathmini ya Utawala Bora, kwa lengo la kushirikishana modeli yake, uzoefu na maarifa na kanda nyingine za dunia, kwa ajili ya kuweka vigezo na utambuzi mkubwa wa tathmini;

38. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** jitihada za APRM za kusaidia uwezo wa taifa wa Nchi Wanachama katika ufuatiliaji na tathmini ya Ajenda ya 2063/Ajenda ya

2030 kupitia Utoaji ripoti wa Hiari wa Taifa (VNRs), Uandaaji wa Taifa wa Mipango ya Jamii ya kujifunza shughuli za nchi wakati wa mkutano wa Kisiasa wa Viongozi wa Ngazi ya Juu katika Umoja wa Mataifa;

39. **UNAREJEA** Uamuzi wake, Assembly/AU/Dec.686(XXX), wa Januari, 2018, ambapo Mkutano Mkuu ulikubali hatua zilizochukuliwa kuiweka APRM kama chombo cha tahadhari ya mapema cha kuzuia migogoro katika Bara, kwenye mazingira ya maelewano na ushirikiano kati ya APRM, Muundo wa Amani na Usalama Afrika, na Muundo wa Utawala Afrika;

40. **PIA UNAREJELEA** Uamuzi wake **Assembly/AU/Dec.874(XXXVII)** wa Februari 2024, ambapo ilihimiza Sekretarieti ya Bara ya APRM kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na Nchi Wanachama kuendelea kuandaa Kikao cha Pamoja kati ya Jopo la APR la Watu Mashuhuri na Jopo la Hekima la AU, pamoja na Kikao cha Pamoja kati ya APRM na Baraza la Amani na Usalama la AU.

41. **UNAIOMBA** Sekretarieti ya Bara ya APRM, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika na Nchi Wanachama, kuchukua hatua zinazohitajika kuandaa na kufanya Kikao cha Pamoja kati ya Jopo Watu Mashuhuri na Jopo la Wazee la APR na AU, pamoja na Kikao cha Pamoja kati ya APRM na Baraza la Amani na Usalama la AU mwaka 2025.

42. **UNAREJELEA** Uamuzi wake **Assembly/AU/Dec.720(XXXII)** wa Februari 2019, uliokabidhi jukumu kwa APRM kuandaa, kwa kushirikiana na Muundo wa Serikali Afrika (AGA), Ripoti ya Muundo wa Serikali Afrika na kuiwasilisha kila baada ya miaka miwili (2) kwa ajili ya kujadiliwa na Mkutano wa Wakuu wa nchi katika mikutano yake ya Kawaida.

43. **UNAZINGATIA KWA SHUKURANI** Ripoti ya Muundo wa Serikali Afrika 2025 (**AGR-2025**) inayozungumzia Usimamizi wa Rasilimali barani Afrika, ambayo inapendekezwa kupitishwa na Mkutano wa APR.

44. **UNAIPONGEZA** miundo ya AU na APRM, wanachama wa AGA, Nchi Wanachama, taasisi za utafiti za Afrika, na wataalamu huru walioshiriki katika uandaaji wa **AGR-25** kwa kazi yao nzuri; **UNATO SHUKURANI** kwa washirika kwa msaada wao wa thamani na kujitolea kwao katika kuandaa **AGR-2025**.

45. **UNAIDHINISHA** maitimisho na mapendekezo ya **AGR-2025** na **UNAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU kutekeleza mapendekezo yaliyomo katika Ripoti hiyo, kwa lengo la kuimarisha utawala bora, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu, na kushirikishana mbinu bora katika ngazi ya kitaifa na ya bara.

46. **PIA, UNAHIMIZA** Sekretarieti ya Bara ya APRM kuhakikisha usambazaji mpana wa **AGR-2025** baada ya kujumuisha maoni kutoka kwa Nchi Wanachama.

47. **UNASISITIZA** umuhimu wa kutafuta rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya usambazaji wa **AGR-2025** na utekelezaji wa mapendekezo yake; **UNAIOMBA** APRM kuzindua rasmi **AGR-2025** kwa kushirikiana na AGA;

48. **UNAHIMIZA** wanachama wote wa AGA kujumuisha Ripoti hiyo katika Mipango yao ya Kazi ya Mwaka na **PIA UNAHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa AU kuandaa ripoti za utawala wa kitaifa kama zana ya kujitathmini, ili kukuza utawala bora na usimamizi bora na wenye ufanisi wa maliasili, kulingana na mapendekezo ya **AGR-2025**

49. **UNAIOMBA** APRM kuandaa, kwa kushirikiana na AGA, mada na lengo la Ripoti ya Tano ya Utawala wa Afrika na kuwasilisha Ripoti hiyo katika Mkutano wa Kawaida wa 40 Wakuu wa Nchi unaotarajiwa kufanyika mwezi Februari 2027.

50. **UNAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1189-1216(XLII) wa Februari 2023 uliopitisha Misingi na Miongozo ya Utawala wa Afrika na kuelekeza APRM kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika kusaidia Nchi Wanachama katika utekelezaji wa Misingi ya Afrika.

51. **UNIAOMBA** Sekretarieti ya Bara la APRM na Kamisheni ya Umoja wa Afrika ikiungwa mkono na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuhakikisha maandalizi ya kutosha na kuzindua Kanuni na Miongozo ya Afrika kuhusu Utawala wa Taasisis katika nusu ya kwanza ya 2025;

52. **UNAREJELEA** Uamuzi wake Assembly/AU/Dec.631 (XXVIII) uliopitishwa katika Mkutano wa 28 Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali, uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia Januari 2017, ukiielekeza APRM kutoa msaada kwa Nchi Wanachama katika nyanja ya ukadiriaji wa mikopo;

**53.** **UNAREJELEA** Uamuzi EX.CL/ Dec.1268(XLV), wa Julai, 2024 ambapo Baraza Kuu liliiomba AUC na APRM kwa kushirikiana na AfreximBank na Taasisi nyingine za Kifedha za Afrika, kuharakisha shughuli za Shirika la Afrika la Ukadiriaji wa Mikopo linaloendeshwa na sekta binafsi kwa kuzingatia ufadhili wa kujitegemea;

**54.** **UNAKARIBISHA KWA SHUKRANI** hatua na maendeleo yaliyofikiwa na Kamisheni ya AU na APRM katika uanzishaji na uendeshaji wa Shirika la Afrika la Ukadiriaji wa Mikopo; **UNAIPONGEZA** Kamisheni, na APRM kwa msaada wa Kamisheni ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AfriximBank kwa kuandaa kwa mafanikio hafla ya Rais kuhusu uanzishwaji wa Shirika la Afrika la Tathmini ya Mikopo;

55. **UNATOA SHUKRANI KUBWA** kwa Mhe. Abdelmadjid TEBBOUNE, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti wa Jukwaa la APR; Mhe. Taye Atske Selassie, Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia, Mhe. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mhe. Hakainde

Hichilema, Rais wa Zambia kwa msaada wao usioyumba kwa uendeshaji wa haraka wa Shirika la Afrika la Ukadiriaji wa Mikopo linaloendeshwa na sekta binafsi kwa ufadhili binafsi;

56. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama, Taasisi za Kifedha za Afrika, Sekta ya binafsi kusaidia utendaji kazi kamili na wenye ufanisi wa Shirika la Afrika la Ukadiriaji wa Mikopo;

57. **UNATOA SHUKRANI** kwa Jukwaa la APR na vyombo vyote vya APRM na AU kwa kufanya kazi bila kuchoka katika kuhakikisha kwamba APRM iko katika nafasi nzuri ya kutekeleza majukumu yake kwa matokeo yanayoonekana;

58. **UNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa Jukwaa la APR, Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria kwa uongozi bora kwa APRM na mafanikio ya kipekee yaliyopatikana kwa Mpango huo chini ya uongozi wake.

**UAMUZI KUHUSU
RIPOTI YA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI YA AUDA-NEPAD YA MHE. ILIYOWASILISHWA NA RAIS ABDEL FATTAH EL-SISI RAIS WA JAMHURI YA KIARABU YA MISRI– Doc. Assembly/AU/11 (XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA KWA KUTHAMINI** ripoti ya Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa Kamati ya Maelekezo ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC) ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika - Ushirikiano Mpya wa Maendeleo ya Afrika (AUDA- NEPAD).

2. **UNAIDHINISHA** hitimisho na mapendekezo ya Mkutano wa 42 wa AUDA-NEPAD HSGOC, uliofanyika tarehe 10 Februari 2025, kwa kuzingatia sheria na taratibu za AU.

3. **UNAREJELEA** hitimisho na mapendekezo ya Mkutano wa 41 wa HSGOC, uliofanyika tarehe 13 Februari 2024; na unaipongeza AUDA-NEPAD kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana.

4. **UNASISITIZA** jukumu kuu, pamoja na kukua kwa umuhimu na athari za AUDA-NEPAD, kama Shirika kuu la maendeleo la bara la Afrika; na **KUSISITIZA** kwamba mamlaka yake ni kuratibu na kutekeleza miradi ya kipaumbele ya kikanda na bara ili kuongeza kasi ya kufikiwa kwa Ajenda ya mwaka 2063.

5. **UNATAMBUA** kwamba, kwa mujibu wa Mkataba wa AUDA-NEPAD, Shirika kuu la Maendeleo wa Bara la Afrika, HSGOC, Kamati ya Uongozi na Sekretarieti, ni miundo pekee ya utawala ya AUDA-NEPAD.

6. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.813-838(XXXV) wa Februari 2022 ukiitaka AUDA-NEPAD kuharakisha michakato ya kuanzisha Mfuko wa Maendeleo; **UNAPONGEZA** maendeleo ya AUDA-NEPAD tangu wakati huo, ikiwa ni pamoja na kuitishwa mikutano faragha ya Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15) mwezi Juni 2024 ili kutathmini Upembuzi Yakinifu, kuanzishwa kwa bodi ya ushauri ili kupitia utafiti huo, majadiliano na Benki za Maendeleo za Kimataifa na Taasisi za Kifedha za Maendeleo, pamoja na Kamati ya Utendaji ya AUDA-NEPAD, pamoja na kuitisha mkutano mwingine mkutano tarehe 3-4 Februari 2025 ili kupitia utafiti uliofanyiwa marekebisho; na kwa hivyo **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kushirikiana kwa karibu na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha ili kukamilisha upembuzi yakinifu, na kupata ridhaa kutoka kwa Kamati ya Utendaji na Mashirika yanayohusika ya Sera ya AU kufuata utaratibu unaofaa, ili kuidhinishwa kwenye mkutano wa Uratibu wa nusu mwaka wa Julai 2025.

7. **UNAREJELEA** kanuni ya michango ya hiari ya Nchi Wanachama kwa AUDA-NEPAD, kama ilivyoanzishwa na maamuzi Assembly/AU/Des 6-32 (II),/AU/Des

268-288 (XIV), na Ext/Assembly/AU/Des.1-4(XI); **UNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo tayari zinachangia, **UNAZINGATIA** vikwazo muhimu vya kifedha vya AUDA-NEPAD; na katika suala hili **UNASISITIZA** mahitaji ya dharura ya Nchi Wanachama kuzingatia michango ya hiari ili kuhakikisha ufadhili unaotabirika na endelevu kwa ajili ya uendeshaji bora wa AUDA-NEPAD.

8. **UNATAMBUA** umuhimu wa ushirikiano ulioratibiwa wa Afrika katika Kongamano la 4 la Kimataifa la Ufadhili wa Maendeleo (Hispania; Juni 2025); **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC, RECs, Nchi Wanachama, na taasisi za fedha husika, kufanya mapitio ya kina ya maendeleo ya Ajenda ya Hatua ya Addis Ababa 2015; na **UNAIAGIZA** AUDA- NEPAD kuanzisha mchakatio wa majadiliano ili kukuza msimamo wa pamoja wa Afrika.

9. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi /AU/Des. 283 (VIV) kuhusu hitaji la AUDA- NEPAD kuwa na unyumbufu unaohitajika na wepesi wa kutekeleza majukumu yake; na **UNAZINGATIA** vikwazo vya uendeshaji vilivyowekwa kwenye AUDA-NEPAD.

10. **UNAIHIMIZA** AUDA-NEPAD kushirikiana na Kamati ndogo husika za PRC kuchunguza fursa bunifu za ufadhili ili kujaza nafasi muhimu ambazo tayari zimeidhinishwa katika muundo, kwa kutumia ufadhili wa Nchi Wanachama na Washirika wa Maendeleo (DP).

11. **UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Des.852 (XXXVI) wa Februari 2023 na Assembly/AU/9 (XXXVII) wa Februari 2024 kuhusu upanuzi wa AUDA-NEPAD kuwa kitaifa na kikanda; **UNAZINGATIA** nia ya baadhi ya Nchi Wanachama kufungua Ofisi za AUDA-NEPAD kwa gharama zao na **UNAPONGEZA** juhudi za Shirika hilo katika kushughulikia maombi ya Nchi Wanachama ya kuongeza wigo wa AUDA- NEPAD bila gharama ya ziada kwa bajeti ya Nchi Wanachama. **INAIOMBA** AUDA-NEPAD kufuata utaratibu wa kawaida wa udhibiti wa utekelezaji wa mchakato huu unaolenga kufungua ofisi za kitaifa.

12. **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kuanzisha Jukwaa la Dijitali la Ajenda ya mwaka 2063 kama nyenzo ya bara ya kuratibu, kufuatilia, kutathmini na kutumika kama jukwaa la hazina kukuza maarifa, kubadilishana maarifa, mawasiliano, utetezi na kufanya uamuzi na **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kutumia zana hii muhimu.

13. **UNAZINGATIA KWA KUTHAMINI** Ripoti ya Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Mwenyekiti wa AUDA-NEPAD HSGOC, iliyowasilisha na kupitishwa katika Mkutano wa 6 wa Uratibu wa Nusu Mwaka (Accra, Ghana; tarehe 21 Julai 2024) kuhusu “Jukumu la AUDA-NEPAD la kutumika kama nyenzo kufanikisha Mpango wa Uwekezaji wa Awamu ya Pili ya miaka 10 kwa kushirikiana na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda”.

14. **UNAREJEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec875(XXXVII) wa Februari 2024 ambao

liliipongeza AUDA-NEPAD kwa kubuni na kuendeleza Mpango wa Kukusanya Rasilimali za Timu ya Afrika kama mfumo wa juhudi za uhamasishaji wa rasilimali katika bara zima.

**15.** **UNAPONGEZA** Mpango wa Timu ya Afrika kama mpangomkakati wa kutekeleza Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi; **UNATHIBITISHA** juhudi za pamoja za uhamasishaji wa rasilimali zinazoongozwa na AUDA-NEPAD na RECs kwa ushirikiano na taasisi nyingine za AU, zinazolenga kupata ufadhili endelevu na wa kiubunifu kwa ajili ya utekelezaji wa programu za kipaumbele chini ya STYIP; **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD na RECs kutoa taarifa ya utekelezaji ya mara kwa mara ya Mpango wa Timu ya Afrika, ikijumuisha maendeleo ya uhamasishaji wa rasilimali, utekelezaji wa programu, na tathmini ya athari, kwenye mkutano wa uratibu wa nusu mwaka; na **UNATOA WITO** KWA washirika wa maendeleo, Benki za Maendeleo ya Kimataifa, na sekta binafsi kuunga mkono kikamilifu Mpango wa Timu ya Afrika na kushirikiana na AUDA-NEPAD, RECs, na Nchi Wanachama katika kutafuta rasilimali na utaalamu wa kiufundi kwa ajili ya maendeleo ya mabadiliko ya Afrika.

**16.** **UNAUNGA MKONO** Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kuitishwa kwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Mpango wa Rais wa Kinara wa Miundombinu (PICI) tarehe 9 Februari 2025; **UNAKARIBISHA** uimarishaji upya wa PICI kwa kuzingatia upya kupanua utafutaji wa rasilimali kupitia Majadiliano ya kila mwaka ya Rais na Wawekezaji na kuanzisha Mkutano wa Kila Mwaka wa Kikosikazi cha Kitaalamu cha ya PICI kwa ajili ya uratibu na ufuatiliaji; InaIhimiza Nchi Wanachama kuthibitisha kujizatiti kwao katika Sekretarieti ya PICI kupitia michango ya kifedha na kitaalamu na kuimarisha maeneo makuu ya kitaifa kwa ajili ya uratibu unaofaa; **UNATOA WITO** kwa Jamhuri ya Afrika Kusini kushirikisha washirika wa G20 na wafadhili wa maendeleo wa kimataifa ili kutumia Urais wake wa G20 (2024-2025) katika kutetea ongezeko la uwekezaji wa miundombinu barani Afrika; na UNAKIOMBA Kikosikazi cha Kitaalamu cha PICI kupanga upya mchakato wa PICI na kuanzisha mfumo unaoboresha usaidizi kwa wanachama wa PICI ili kuharakisha ukamilishaji wa mradi na kuhakikisha uwasilishaji wa mipango ya miundombinu kwa wakati.

**17.** **UNAZINGATIA** umuhimu mkubwa wa miundombinu, uunganishaji wa usafiri, na uwezeshaji wa biashara katika kufikia malengo ya ushirikiano na maendeleo ya Afrika; **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa Kuandaa Wiki ya 8 ya PIDA (26–29 Novemba 2024, Addis Ababa.

**18.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kupata uidhinishaji wa Mpango Kabambe wa Mifumo ya Umeme ya Bara (CMP) kama mradi wa AU 2063 wa Ajenda ya mwaka 2063.

**19.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kuandaa mwongozo wa akili unde wa Bara na Mpango, unaoeweka mwongozo wa AI barani Afrika na kuendeleza Mpango wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Usimamizi wa Data ili kukuza uhimilivu wa

mtandao wa kikanda; na **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele katika uwekezaji katika usalama wa mtandao, akili unde na utawala wa kidijitali, kulinda uchumi wa kidijitali wa Afrika.

**20.** **UNATAMBUA** uwezo wa kuleta mabadiliko ya teknolojia ya kidijitali, akili unde (AI), na usalama wa mtandao kwa maendeleo ya Afrika; **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa ushirikiano wake wa kiubunifu na Meta; **UNAWAPONGEZA** AUDA-NEPAD na Meta kwa kubuni na kuendeleza akili unde, mfumo unaotumika kusaidia wajasiriamali wa Kiafrika na kukuza bara kwa siku zijazo; na UNAIOMBA AUDA-NEPAD na washirika wake wa kitaalamu na kifedha kutayarisha na kuwasilisha program kamili ya AKILI AI wakati wa Mkutano ujao wa Uratibu wa AU wa Julai 2025 ili kujadiliwa na HSGOC.

**21.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kuzindua Mwelekeo wa 4 wa Ubunifu wa Kiafrika (AIO-2024); UNAZITAKA Nchi Wanachama kuimarisha uwezo wao wa kupima Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STI); na **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kushughulikia kushuka kwa data ya STI kwa kuharakisha uteuzi wa vituo vya kufanya kazi kwa karibu na AUDA-NEPAD katika kuboresha ukusanyaji na upimaji wa data kote Afrika.

**22.** **UNAIPONGEZA** AUC na AUDA-NEPAD kwa kuandaa na kuidhinisha STISA-2034; UNATHIBITISHA jukumu la AUDA-NEPAD katika utekelezaji na uratibu wa STISA 2034 kwa ushirikiano na AUC na wadau wengine; na **UNAITAKA** AUDA-NEPAD kukamilisha mpango wa utekelezaji na kuhakikisha unatekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi.

**23.** **UNALIPONGEZA** Jopo la Viongozi wa Ngazi ya Juu la AU kuhusu Teknolojia Zinazochipuka (APET) na AUDA-NEPAD kwa kuendeleza athari za kimaendeleo za teknolojia zinazoibukia kote barani Afrika; na **UNAELEKEZA** AUDA-NEPAD na APET kuunda mfumo wa udhibiti unaosimamia upitishwaji wa teknolojia zinazoibuka na kuzipa Nchi Wanachama usaidizi wa kiufundi na kisera ili kuongoza upitishwaji.

**24.** **UNAMPONGEZA** Mhe. Rais Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda, Kinara wa AU kuhusu Ufadhili wa Afya ya Ndani, kwa uongozi wake wa kupigiwa mfano ambao umekuwa chanzo cha mwongozo wa kimkakati na msukumo wa kuendeleza ajenda ya ufadhili wa afya ya ndani ya Afrika; na **UNAZINGATIA** maendeleo yaliyofikiwa ya AUDA-NEPAD katika kufanya kazi kwa Vituo vya Ufadhili wa Afya vya Kikanda (RHFHs) katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, na Shirika la Afya la Afrika Magharibi.

**25.** **UNATOA WITO** kwa RECs zilizosalia kuharakisha utendaji kazi wa RHFHs ili kuhakikisha hakuna Nchi Mwanachama iliyoachwa nyuma katika kufikia mifumo endelevu na yenye usawa ya afya.

26. **UNAREJEA** Azimio Assembly/AU/Dec.4(XXXII) ambalo linasisitiza kukuza ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi ili kuimarisha mifumo endelevu ya ufadhili wa afya; na **UNAMPONGEZA** Mhe. Rais William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, kwa uzinduzi wa Mpango wa AUDA-NEPAD wa Uwekezaji na Ufadhili katika Sekta ya Afya ya Afrika (PIFAH).

27. **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama zinazotekeleza ahadi za Mkutano wa Uongozi wa Afrika (ALM) kutumia utaratibu huu wa kuendeleza na kutekeleza miradi ya kipaumbele ya uwekezaji wa afya ili Kubadilisha Uchumi wa Afya wa Afrika.

28. **UNAIPONGEZ**A AUDA-NEPAD kwa kuanzisha dhana na kuendeleza Mpango wa Mgao wa Demografia wa Afrika na Mpango wa Afya ya Jinsia na Uzazi (A2DSRH) ambao utachangia katika kuimarisha mifumo ya afya ya kitaifa na kikanda, na kukuza upatikanaji wa huduma za afya zilizo salama, bora, na uhakika; na KUREJELEA uamuzi Assembly/AU/Des. 629 (XXVII) kuhusu Mkakati wa Afya wa Afrika (2016-2030) pamoja na Assembly/AU/Des.591(XXVI) kuhusu Kuweka Gawio la Idadi ya Watu kupitia Uwekezaji kwa Vijana.

29. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuharakisha utekelezaji wa maamuzi haya na vilevile kujitahidi kuoanisha michakato ya sera zinazohusu afya ya ngono na uzazi na mgao wa idadi ya watu huku zikiheshimu sheria za kitaifa na utamaduni na sifa maalum za kijamii; na **UNAIELEKEZA** AUDA- NEPAD, kushirikiana na AUC, kuratibu na wadau husika, kuandaa ripoti ya maendeleo ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Maputo (2016-2030) na Mwongozo wa AU wa 2017 wa Kuweka Gawio la Idadi ya Watu kupitia uwekezaji kwa vijana, na kuandaa mapendekezo ya kuharakisha utekelezaji ndani ya kipindi kilichobaki.

30. **UNAMPONGEZA** Mhe. Rais Abdel Fatah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, kwa kuanzisha Kituo cha Ubora cha AUDA-NEPAD cha Mabadiliko ya Tabianchi, Uhimilivu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi huko Kairo, Misri; na **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD kuongeza kasi ya uendeshaji wa kituo.

31. **UNAMPONGEZA** Rais William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kilele wa Mabadiliko ya Tabianchi barani Afrika na **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD kwa kushughulikia kuanzishwa kwa Viwango vya Dhahabu vya kukabiliana hewa ukaa barani Afrika.

32. **UNAZIHAMASISHA** Nchi Wanachama kubadilishana maoni na mbinu bora kuhusu masoko ya kaboni, kwa kutilia maanani kanuni ya "Majukumu ya Pamoja Lakini Yanayotofautiana" ambayo huongoza mataifa ya Afrika katika ushughulikiaji wa mabadiliko ya tabianchi.

33. **UNAKARIBISHA** kupitishwa kwa Azimio la CAADP la Kampala na Mkakati na Mpango Kazi wa CAADP: 2026–2035; na kutambua jukumu muhimu la mifumo himilivu ya kilimo katika kufikia usalama wa chakula, lishe na maendeleo endelevu

barani Afrika; **UNAAHIDI** kuendeleza na kutekeleza mikakati ya kitaifa ya mabadiliko ya mifumo ya chakula, inayowiana na mfumo wa CAADP na Azimio la Kampala.

**34.** **UNAIPONGEZA** AUDA-NEPAD na AUC kwa msaada wao kwa Nchi Wanachama katika kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika mchakato wa baada ya Mkataba wa Malabo; na **UNAIELEKEZA** AUDA-NEPAD kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Azimio la Kampala, Mkakati, na Mpangokazi wa Nchi Wanachama, RECs na wadau wengine.

**35.** **UNAKARIBISHA** na **KUIDHINISHA** Miongozo ya Kujumuisha Mifumo ya Kilimo cha Chakula katika Mipango na Programu za Kitaifa", iliyotayarishwa na AUDA-NEPAD, kama nyenzo muhimu kwa Nchi Wanachama; **UNAIELEKEZA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC, kutoa msaada wa kitaalamu na kujenga uwezo kwa Nchi Wanachama kwa ajili ya matumizi ya Miongozo katika kuingiza mifumo ya chakula katika mipango ya kitaifa, na kukusanya rasilimali, ikiwa ni pamoja na kutoka kwa washirika wa maendeleo ili kuunga mkono juhudi za Nchi Wanachama katika kutekeleza Azimio la Kampala na Mkakati na Mpango Kazi wa CAADP.

**36.** **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na Kituo cha Mfumo wa Chakula wa Umoja wa Mataifa, kusaidia Nchi Wanachama kuandaa ripoti yao ya pili ya mfumo wa chakula wa kitaifa; **UNAIOMBA ZAIDI** AUDA-NEPAD, kwa kushirikiana na AUC na Nchi Wanachama, kuratibu uundwaji wa msimamo mmoja wa Afrika kwa ajili ya Mkutano wa Pili wa Umoja wa Mataifa wa Mifumo ya Chakula (UNFSS+4), unaofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 28–30 Julai 2025.

**37.** **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kutwaa Urais wa "Afrika" wa kwanza kabisa wa G20 mnamo 2025; na **KUTHAMINI** michango ya muda mrefu na yenye kujenga ya AUDA-NEPAD kwa michakato ya G20, pamoja na kuwa nchini Afrika Kusini; **UNAIOMBA** AUDA-NEPAD ijumuishwe katika ujumbe rasmi wa AU kwenye mikutano yote ya G20 iliyofanyika Afrika Kusini mwaka wa 2025, ikijumuisha Mkutano wa viongozi.

**38.** **UNAMPONGEZA** Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, kwa uongozi wake wa kipekee wa AUDA-NEPAD HSGOC tangu Februari 2023, na **UNAAMUA** kuongeza muda wa uenyekiti wa HSGOC kwa mwaka mmoja hadi Februari 2026.

**39.** **UNAUNGA MKONO** kuendelea kwa ubora endelevu wa AUDA-NEPAD katika kutoa matokeo makubwa ya maendeleo na kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji, Bi. Nardos Bekele-Thomas, kwa uongozi wake wenye maono.

**40.** **UNAREJELEA** kuwa uanachama wa AUDA-NEPAD HSGOC kwa kipindi cha Februari 2023 hadi Februari 2025 ni kama ifuatavyo:

| **Kanda ya Kati** | **Kanda ya Mashariki** | **Kanda ya Kaskazini** | **Kanda ya Kusini** | **Kanda ya Magharibi** |
|---|---|---|---|---|
| 1. Cameroon | 6. Ethiopia | 11.**Algeria*** | 16. Lesotho | 21. Cote d'Ivoire |
| 2. DRC | 7. Kenya | 12.**Misri*** | 17. Malawi | 22. Ghana |
| 3. Afrika ya Kati | 8. Rwanda | 13. | 18.**Afrika Kusini*** | 23. Guinea Bissau |
| 4. Equatorial Guinea | 9.Uganda | 14. | 19. Zambia | 24. **Nigeria*** |
| 5. Gabon | 10.Tanzania | 15. | 20. Zimbabwe | 25. **Senegal*** |

*** Wajumbe waanzilisi wasio wa mzunguko**

| **WAKUU NANE (8) WA NCHI NA SERIKALI WENYEVITI WA JUMUIYA ZA UCHUMI – 2025** | | |
|---|---|---|
| 1. | **ECOWAS** | Naijeria |
| 2. | **ECCAS** | Equatorial Guinea |
| 3. | **IGAD** | Djibouti |
| 4. | **UMA** | Libya |
| 5. | **COMESA** | Burundi |
| 6. | **SADC** | Zimbabwe |
| 7 | **EAC** | Kenya |
| 8. | **CENSAD** | Chad |

**41.** **UNAAMUA kuongeza** muda wa uanachama wa HSGOC kwa mwaka mmoja hadi Februari 2026.

**42.** **UNAREJELEA** kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za AUDA-NEPAD na kwa kuzingatia mashauriano ya kikanda, Makamu Wenyeviti wanne (4) wa AUDA-NEPAD HSGOC kwa kipindi cha Februari 2023-Februari 2026 ni kama ifuatavyo:

- Makamu wa Kwanza – Kanda ya Kati: Nafasi iko wazi.
- Makamu wa Pili –Kanda ya Kusini: Jamhuri ya Afrika Kusini.
- Makamu wa Tatu – Kanda ya Magharibi: Nafasi iko Wazi
- Makamu wa Nne/Katibu – Kanda ya Mashariki: Jamhuri ya Rwanda (Mwenyekiti wa AUDA-NEPAD HSGOC anayemaliza muda wake).

**43.** Kulingana na Sheria na Taratibu, **UNAZIHIMIZA** kanda ya Kati na Magharibi kuhitimisha majadiliano yao na kuchagua wawakilishi wao wa Uongozi wa HSGOC.

**UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUMI (10) KUHUSU MAGEUZI YA BARAZA LA USALAMA LA UMOJA WA MATAIFA, YA MHE. JULIUS MAADA BIO, RAIS WA JAMHURI YA SIERRA-LEONE–** Doc. Assembly/AU/12(XXXVIII)

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAREJELEA** Ripoti ya 25 ya Kamati ya Umoja wa Afrika ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na **UNAIDHINISHA** Matokeo ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Kamati ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, uliofanyika Algiers, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria, kuanzia Juni 20–21, 2014.

2. **UNAREJELEA** maamuzi, yakiwemo Assembly/AU/Des.853(XXXVI), Assembly/AU/Des.564(XXIV), Assembly/AU/Des.574(XXV), na Assembly/AU/Des.724(XXXII).

3. **UNASISITIZA** kwamba kuufanya mageuzi Umoja wa Mataifa ni muhimu ili kuhakikisha kwamba unaendana na hali halisi ya jiografia na siasa za kisasa na changamoto zinazojitokeza duniani. Katika suala hili, ni muhimu kushughulikia dhulma ya kihistoria inayoikabili Afrika, hasa kutokuwepo kwake katika kundi la wanachama wa kudumu na uwakilishi wake mdogo katika kundi lisilo la kudumu la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

4. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** ushiriki wa Kamati ya Wakuu Kumi, ambayo inaendelea kupiga hatua kubwa katika kukuza, kutetea, na kuhamasisha Msimamo wa Pamoja wa Afrika, kama ilivyoainishwa katika Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte la 2005 kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

5. **UNAPONGEZA** kuitishwa kwa mkutano huo wakati wa Wiki ya Ngazi ya Juu ya Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kati ya Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Wajumbe wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Kamati ya Nchi Wanachama Kumi; pamoja na mjadala wa kwanza wa Ngazi ya Juu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu "Udumishaji wa Amani na Usalama wa Kimataifa: Kushughulikia Udhalimu wa Kihistoria na Kuimarisha Uwakilishi Bora wa Afrika" wakati wa Urais wa Sierra Leone wa Baraza hilo mwezi Agosti.

6. **UNAKARIBISHA** uungwaji mkono unaoongezeka na msukumo wa Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, hasa kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 39, aya ya (a) ya Mkataba wa Baadaye, ambayo inaidhinisha umuhimu wa ‘Kurekebisha dhuluma ya kihistoria dhidi ya Afrika kama kipaumbele na, huku ikiichukulia Afrika kama suala maalumu, kuboresha uwakilishi wa makundi yasiyokuwa na uwakilishi na uwakilishi mdogo’.

7. **UNATHIBITISHA** dhamira yake kwa Msimamo wa Pamoja wa Afrika, kama ilivyoainishwa katika Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte, kama chaguo PEKEE linalowezekana kwa uwakilishi kamili wa Afrika katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Katika muktadha huu, IGN iliyoanzishwa na Uamuzi 62/557 inabaki kuwa jukwaa mwafaka na halali zaidi la mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

8. **UNASISITIZA** kwamba uwakilishi kamili wa Afrika katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililofanyiwa mageuzi unahusisha:

(i) Viti visivyopungua viwili (02) vya kudumu vyenye haki na stahiki zote za uanachama wa kudumu, ikiwa ni pamoja na haki ya kura ya turufu, iwapo itabakizwa.
(ii) Viti vitano (05) visivyo vya kudumu.
(iii) Haki ya Umoja wa Afrika kuchagua wawakilishi wake kwa ajili ya kuchaguliwa kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kutenda kwa jina lake na kwa niaba yake.

9. UNAIOMBA

(i) Kamati ya Viongozi Kumi wa Nchi na Serikali kushiriki katika ngazi za juu za kisiasa, ikijumuisha na Wajumbe watano wa Kudumu wa Baraza la Usalama, ili kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa;

(ii) Kamati ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali kuendelea kuzidisha ushirikiano wake na Makundi mengine yenye maslahi na Kikanda na wadau, kwa kuzingatia maendeleo yaliyopatikana katika kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Katika suala hili, **UNAIHIMIZA** Kamati ya Wakuu Kumi wa Nchi na Serikali kufanya Mikutano ya Ngazi ya Juu pembezoni mwa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika;

(iii) Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika kuwa na kauli sahihi ya pamoja ili kuendeleza Msimamo wa Pamoja wa Afrika katika Hotuba zao za Kitaifa wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa 80 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Septemba 2025, zikirejelea mwito wa mageuzi ya kina ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, na kutekeleza dhamira ya kurekebisha dhuluma ya kihistoria dhidi ya Afrika kama suala la kipaumbele na kuichukulia Afrika kama suala la kipaumbele na

(iv) Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kulipa kipaumbele suala la mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa katika ushirikiano wao wa sera za nje na washirika wasio Waafrika, hasa kusisitiza haja ya kurekebisha dhuluma ya kihistoria ambayo Afrika inaendelea kukabiliana nayo, na kuichukulia Afrika kama suala maalum na kipaumbele katika mchakato wa mageuzi.

10. **UNASISITIZA** dhamira yake thabiti ya kuendeleza umoja na mshikamano wa Afrika katika vipengele vyote vya mchakato wa mageuzi wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ikiwa ni pamoja na ushiriki ndani na nje ya mazungumzo baina ya serikali, na

kuendelea kuzungumza kwa sauti moja kuhusu vipengele vyote vya mchakato wa mageuzi.

11. **UNATOA WITO KWA** Afrika kujihusisha katika mazungumzo ya maandishi ili mradi kuna maafikiano ya awali kati ya Nchi Wanachama kuhusu makundi matano na mfumo uliokubaliwa, ambao unashughulikia kwa mapana suala la ukosefu wa haki wa kihistoria, ambao una makubaliano mapana, na mfano wa mageuzi ambayo yanashughulikia kwa uwazi upanuzi katika makundi yote mawili ya UNSC.

12. **UNASISITIZA** kwamba Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika huko New York zilizo na wanachama mara mbili zinapaswa kuondoa uanachama huo kutoka kwenye Makundi mengine yote ya Maslahi, hasa yale yenye misimamo isiyolingana katika Msimamo wa Pamoja wa Afrika, kama inavyoonyeshwa katika Makubaliano ya Ezulwini na Azimio la Sirte na kuepuka kukinzana na Msimamo wa Pamoja wa Afrika na maoni na/au misimamo ya Makundi mengine ya Maslahi na Kikanda.

13. **UNAKARIBISHA** uamuzi wa kufanya Mkutano wa Mawaziri wa C-10 katika Jamhuri ya Zambia mwezi Juni 2025 na mkutano wa Ndani wa wa Mabalozi wa C-10 kabla ya Mkutano wa Mawaziri katika Jamhuri ya Sierra Leone.

14. **UNAAMUA:**

(i) Kwamba Msimamo wa Pamoja wa Afrika kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa utabaki kuwa kipengele cha kimkakati kwenye ajenda na mpango kazi wa Mkutano Mkuu. Kwa maana hiyo, **UNATHIBITISHA** Umuhimu wa Kamisheni kuendelea kutoa fedha na msaada unaohitajika ili kuwezesha kazi za Kamati ya Wakuu Kumi, kuhakikisha ufanisi wake katika kutekeleza majukumu yake.

(ii) Kuongeza mgao katika bajeti za Kamisheni na Ujumbe wa Kudumu wa Waangalizi wa Umoja wa Afrika ili kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Kamati ya Wakuu Kumi ya Mageuzi ya Umoja wa Mataifa, kuwezesha Kamati kushiriki kikamilifu na Nchi Wanachama, Makundi ya Maslahi, na wadau katika mchakato wa IGN. UNASISITIZA kuwa fedha ni muhimu katika kuwezesha Kamati ya Wakuu Kumi kutekeleza majukumu na malengo yake ya kiutendaji. UNAZIHIMIZA Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kutoa fedha za hiari ili kusaidia kazi ya Kamati ya Wakuu Kumi.

(iii) Kwamba Kamati ya Wakuu Kumi itaendelea kushikilia mamlaka yake hadi Afrika ifikie malengo yake kuhusu mageuzi ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

# UAMUZI KUHUSU KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI YA AFRICA CDC INAYOWASILISHWA NA MHE. MOHAMED OULD CHEICK EL GHAZOUANI, RAIS WA JAMHURI YA KIISLAMU YA MAURITANIA – Doc. Assembly/AU/13 (XXXVIII)

Mkutano Mkuu,

1. **UNAPOKEA** Ripoti za Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali (CHSG) ya Africa CDC, chini ya Uenyekiti wa Mhe. Mohamed Ould Cheick El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania.

2. **UNAUPONGEZA** uongozi wa Mhe. Cyril Ramaphosa, Rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini na Kinara wa AU wa utekelezaji wa Uzuiaji, Utayari na Mwitikio dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko (PPPR) na Mhe. Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania na Mwenyekiti wa AU na Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya Africa CDC kwa uongozi wao katika kuongoza Africa CDC katika uzuiaji na udhibiti wa magonjwa barani.

3. **UNAIPONGEZA** Africa CDC kwa hatua iliyofikiwa mwaka 2024, hususan mwitikio wake kwa tangazo na usimamizi wa mlipuko wa Mpox kama Dharura ya Afya ya Umma na Usalama wa Bara (PHECS) na juhudi za ushirikiano katika kushughulikia Marburg, kipindupindu, ugonjwa wa mlipuko ambao sababu zake hazijulikani, homa ya Lassa, na magonjwa mingine ya milipuko.

4. **UNASIKITISHWA SANA na** kuongezeka kwa idadi ya milipuko mipya kama vile AMR (usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (*Anti-Microbial Resistance*)) inayoathiri Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika, Mpox inayoathiri takriban 40% ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, Marburg, kipindupindu, ugonjwa X, kidingapopo (*dengue*), homa ya Lassa, na mingine, ambayo inaweza kusababisha magonjwa makubwa barani Afrika ikiwa hayatasimamiwa ipasavyo kutokana na uhaba wa rasilimali watu na fedha, udhaifu katika mifumo ya afya, na ukosefu wa bidhaa za afya.

5. **UNAKARIBISHA** utekelezaji wa uamuzi Assembly/AU/Dec.835(XXXV) kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Magonjwa ya Mlipuko wa Afrika (AfEF) kupitia kuidhinishwa kwa Mfumo wa AfEF, unaolenga kutekeleza mfumo endelevu, ulioratibiwa, na wa uwazi wa kukabiliana na dharura za afya ya umma **NA UNAIAGIZA** Africa CDC kukusanya rasilimali na kuhakikisha mwitikio endelevu, ulilioratibiwa, na wa uwazi kwa dharura za afya barani Afrika.

6. **UNATAMBUA NA KUTHIBITISHA KIKAMILIFU** jukumu muhimu la Africa CDC, la kulinda afya ya umma kwa kutoa mwongozo wa kimkakati na msaada kwa nchi wanachama kutokana na jukumu lake kama wakala wa afya ya umma barani Afrika kwa mujibu wa katiba yake na kufanya kazi kwa ushirikiano na Kamisheni, AUDA-

NEPAD, AMA, AfCFTA na Vyombo na vingine vya AU katika nyanja zote za afya ya umma ikiwa ni pamoja na yale yanayohusiana na ufadhili wa afya ya ndani na kimataifa, utengenezaji wa bidhaa za afya ndani ya nchi, Utaratibu wa Ununuzi wa Pamoja wa Afrika, ushirikishwaji wa jamii, uwekaji wa mifumo ya taarifa za afya kidijitali, na ubunifu mwingine mbalimbali katika afya.

7. **UNAELEZEA WASIWASI** kutokana na ukosefu wa uratibu na utayari kati ya Nchi Wanachama zinaposhiriki katika mikutano ya kimataifa ya usimamizi wa afya, hasa ile ya mipango mbalimbali ya afya ya kimataifa na majukwaa mengine ya kimataifa ya afya. Mwenendo wenye mgawanyiko unadhoofisha ajenda ya afya ya kimataifa ya Afrika.

8. **UNAZINGATIA** hatua iliyofikiwa katika kutekeleza uamuzi Assembly/AU/Des.880(XXXVII) kuhusu kuanzisha mfumo wa uwajibikaji kwa ajili ya utekelezaji bora wa Ajenda ya Lusaka kuhusu kuimarisha mipango ya afya ya kimataifa (GHIs) kuelekea kufikia Huduma ya Afya kwa Wote (UHC) barani Afrika.

9. **UNAIPONGEZA** Africa CDC, AfreximBank, na UNECA kwa hatua nzuri zilizopigwa kuelekea utengenezaji wa bidhaa za afya ndani ya Afrika kupitia PHAHM (Jukwaa la Liliooanishwa la Utengenezaji wa bidhaa za Afya barani Afrika) na utendaji kazi mzuri wa APPM (Utaratibu wa Ununuzi wa Pamoja barani Afrika).

10. **UNAZIPONGEZA** nchi za Afrika zinazopiga hatua katika utengenezaji wa bidhaa za ndani ikiwa ni pamoja na Algeria, Benin, Botswana, Burkina Faso, Cameroon, Cape Verde, Cote d’Ivoire, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Guinea, Kenya, Lesotho, Liberia, Morocco, Malawi, Mali, Mauritius, Morocco, Msumbiji, Namibia, Tanzania, Nigeria, Sudan, Rwanda, Rwanda Tunisia, Uganda, Zambia, Zimbabwe katika eneo la utengenezaji wa ndani wa chanjo, dawa, uchunguzi na zana za matibabu.

11. **UNAAMUA** kutangaza mpango wa ufadhili wa utengenezaji wa bidhaa za ndani kuwa ni "Mpango wa Rais Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani wa Ufadhili wa Utengenezaji wa Bidhaa za Afya barani Afrika," kwa kutambua uongozi na msaada usioyumba kutoka kwa Mhe. Rais Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, katika kukusanya dola bilioni 3.2 ili kuunga mkono ajenda ya Africa CDC ya utengenezaji wa ndani wa chanjo, dawa, uchunguzi na bidhaa zingine za afya.

12. **UNAZINGATIA** kazi inayoendelea na Africa CDC ili kuhakikisha mahitaji ya uhakika na kutabirika kupitia ahadi za nchi wanachama kununua bidhaa za muda wa karibu za Watengenezaji wa Afrika kwa ajili ya uendelevu wa wazalishaji waliopo barani Afrika.

13. **UNATAMBUA** jitihada endelevu za Africa CDC kukusanya fedha kutoka wabia mbalimbali kusaidia Nchi Wanacjhama katika kukabiliana na milipuko mbalimbali na **UNAVITAKA** Vyombo vya Sera vya AU kutenga mgao mkubwa wa ufadhili kwa

Africa CDC kwa muundo ulioidhinishwa wa kiwango cha chini cha wafanyakazi 312 kulipwa na Nchi Wanachama, jambao ambalo litahakikisha ufanyaji kazi kamili wa shirika hilo na uwezowa kutekeleza mamlaka yake

14. **UNAIAGIZA** Africa CDC kuunganisha sauti ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika inayowakilisha bara katika GHIs, **UNAIHIMIZA** Africa CDC kuwasilisha maombi ya kuwa mjumbe wa bodi wa GHIs hizi ili kuunga mkono vyema ajenda ya Afrika, **NA UNAIAGIZA** Africa CDC kushirikiana na AUC kwa ajili ya uwakilishi wa Afrika katika mihimili ya afya ya G20, G7, FOCAC, na majukwaa mengine na kutoa ripoti kwa vyombo vya sera vya AU.

15. **UNAHIMIZA** Africa CDC kuendelea kuunga mkono Nchi Wanachama katika mazungumzo ya Mkataba kuhusu Magonjwa ya Mlipuko (*Pandemic Agreement*), yatakayokamilishwa wakati wa Mkutano wa Afya wa Dunia mwaka 2025, na kutoa ripoti kwa Mkutano Mkuu wa AU.

16. **UNAELEKEZA** Africa CDC kuendelea kuongoza Ajenda ya Lusaka na kutumika kama Sekretarieti, wakati ikisaidia ajenda wa ufadhili unaofaa wa mifumo ya afya barani Afrika, ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mgawanyo wa rasilimali za ndani.

17. **UNAIAGIZA ZAIDI** Sekretarieti ya Afrika CDC kuhakikisha utekelezaji wa ahadi zilizotajwa tajwa hapo juu na kutumika kama daraja la kuelezea maslahi ya Afrika na kutoa ripoti ya maendeleo katika Mkutano wa Kawaida wa arobaini na saba wa Baraza kuu mnamo Julai 2025 na Mkutano wa 47 wa Kawaida wa Baraza Kuu na 39 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

**RASIMU YA UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI YA MWAKA YA MWENYEKITI IKIJUMUISHA RIPOTI ZA VINARA ZILIZOAMBATISHWA– Doc. Assembly/AU/15 (XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAZINGATIA KWA SHUKRANI** ripoti ya mwaka ya Mwenyekiti na unapitisha yaliyomo.

2. **UNAPOKEA KWA SHUKRANI** ripoti ya mwaka ya Mwenyekiti ikijumuisha Ripoti za Vinara na **UNAPITISHA** mapendekezo ambayo utekelezaji wake unategemea mchakato wa kutathmini athari zao za kifedha, kisheria na kimuundo.

## UAMUZI KUHUSU RIPOTI YA MRATIBU WA KAMATI YA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI ZA AFRIKA KUHUSU MABADILIKO YA TABIANCHI (CAHOSCC), MHE. WILLIAM RUTO, RAIS WA JAMHURI YA KENYA
**Doc. Assembly/AU/16 (XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu**

1. **UNAZINGATIA** Ripoti ya Mratibu wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC), Mhe. William Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya, na pia **UNAZINGATIA** Mapendekezo yaliyomo;

2. **UNATOA SHUKRANI** kwa Jamhuri ya Kenya kwa kuratibu kazi ya CAHOSCC, kutoa mwelekeo wa kisiasa na kudumisha umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama (COP29) kwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), Mkutano wa 19 wa Nchi Wanachama zinazofanya kazi kama Mkutano wa Mkataba wa Kyopto na Mkutano wa Wanachama wanaofanya kama Mkutano wa Wanachama wa Makubaliano ya Paris;

3. **UNATAMBUA KWA SHUKRANI** nafasi ya Mhe. Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti wa Kamisheni katika kuratibu na kuweka matukio ya mabadiliko ya tabianchi katika COP29, ambayo yalikuza vitendo vya tabianchi kwa Afrika na hivyo kuinua hadhi ya Bara letu;

4. **UNATOA SHUKRANI** kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Shirikisho la Ethiopia kama Rais wa Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu Mazingira (AMCEN) kwa uongozi na uungwaji mkono wa kisiasa wa AMCEN. **UNAPONGEZA** jukumu lililotekelezwa na Mkutano wa Mawaziri wa Afrika kuhusu Mazingira (AMCEN) na Kundi la Afrika la Majadiliano (AGN) kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi katika maandalizi na ushirikiano katika COP29;

**5. UNATAMBUA** kwa shukrani kazi ya Tume za Tabianchi za Afrika (Visiwa vya Afrika, Bonde la Congo na Sahel), na **UNAOMBA** uratibu madhubuti wa Tume ili kuongeza utekelezaji wa mipango hii na kuongeza athari chanya zilizoratibiwa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi barani Afrika;

**6. UNATHIBITISHA** hitaji la dharura la kutekeleza matokeo ya Mkutano wa Kwanza wa Tabianchi Afrika - Azimio la Viongozi wa Afrika la Nairobi kuhusu Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua.

**7. UNAPONGEZA** utendaji kazi wa Sekretarieti ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Tabianchi Afrika katika Makao Makuu ya Wizara ya Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, jijini Nairobi, Kenya kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

8. **UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Des.883 (XXXVII) ambapo Jamhuri ya Kenya ilijitolea kuandaa na kufadhili Ofisi ya Sekretarieti ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na

Serikali kuhusu Tabianchi barani Afrika jijini Nairobi, ikijumuisha utekelezaji wa mwongozo wake na muundo wa utawala.

**9. UNAPONGEZA** utendaji kazi wa Sekretarieti ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Tabianchi barani Afrika katika Makao Makuu ya Wizara ya Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu, Nairobi, Kenya kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika.

**10. UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Des.883 (XXXVII) ambapo Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika walijitolea kufanya Mkutano Mkuu wa Tabianchi wa Afrika kila baada ya miaka miwili kupitia Azimio la Viongozi wa Afrika la Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua na **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama kujitolea kuandaa Mkutano ujao wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Tabianchi barani Afrika.

**11. UNAAMUA** kwamba Sekretarieti ya ACS itaisaidia Kamisheni kwa kushirikiana na Nchi Mwanachama mwenyeji kuitisha Mikutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Tabianchi barani Afrika inayofanyika kila baada ya miaka miwili.

**12. UNAKARIBISHA** maombi ya kuandaa Mkutano wa Pili wa Tabianchi barani Afrika (ACS II) yaliyowasilishwa na Shirikisho la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ethiopia katika Makao Makuu ya AU mapema Septemba 2025.

**13. UNAPENDEKEZA** kuwa Kaulimbiu ya ACS ijayo iwe ya Kukusanya Fedha kwa ajili ya Kukabiliana na Uhimilivu wa Afrika.

**14. UNAMPONGEZA** Mhe. Moussa Faki Mahamat kwa uongozi wake wa kupigiwa mfano kwa namna Kamisheni ilivyoitisha Mkutano wa Kwanza wa Wadau Mbalimbali wa Afrika kuhusu Masoko ya Kaboni uliofanyika kuanzia tarehe 24 hadi 16 Julai 2024 katika Makao Makuu ya AU, **UNAPITISHA** Mpangokazi wa Afrika kuhusu Masoko ya Kaboni na **KUIOMBA** Kamisheni kuharakisha utekelezaji wa Mpangokazi huu;

**15. UNAMPONGEZA** Mhe. Ilham Aliyev, Rais wa Jamhuri ya Azerbaijan, Mhe. Mukhtar Babayev, Rais wa COP29, kwa kuandaa Mkutano wenye mafanikio wa Wanachama wa Mkataba wa Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, na kutoa wito muhimu na mpya wa malengo ya kitaifa ya tabianchi ya kuendeleza ajenda ya kina ya hatua za tabianchi na hasa, uendeshaji wa Mfuko wa Hasara na Uharibifu na Ibara ya 6 ya Mkataba wa Paris;

**16. UNAKARIBISHA** ufadhili mwingine wa kihistoria kwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA) na tangazo la Benki kuu za Maendeleo ya Kimataifa (MDBs) la kuongeza ufadhili wa tabianchi kwa nchi za kipato cha chini na cha kati kufikia dola bilioni 120 kwa mwaka ifikapo 2030.

**17. UNAELEZEA KWA MASIKITIKO MAKUBWA** kutokubaliana kwa nchi zilizoendelea kukusanya dola trilioni 1.3 ifikapo 2030 ambacho ndicho kiwango cha chini kinachohitajika ili kushughulikia hatua za haraka za mabadiliko ya tabianchi barani Afrika na nchi nyingine zinazoendelea zenye uwezo mdogo wa kukabiliana na athari hizo na **UNAKARIBISHA** uamuzi wa kujadili Mwongozo wa 1.3T kwa lengo la kuongeza ufadhili wa tabianchi ili kusaidia uzalishaji mdogo wa gesi chafuzi na njia zinazohimili tabianchi, kupitia hati ambazo hazitengenezi deni na hatua za kuunda mfumo wa kifedha katika wa mfumo wa kifedha wa kimataifa..

**18. UNATAMBUA** kuzinduliwa kwa Mwongozo wa Marekebisho ya Baku ambao unalenga kuendeleza maendeleo kwa mujibu wa Ibara ya 7, aya ya 1, ya Mkataba wa Paris na kusaidia utekelezaji wa vipengele vilivyoainishwa katika aya ya 38 ya uamuzi 2/CMA.5 na **UNAVIOMBA** vyombo tanzu kuweka taratibu za kufanya kazi kwa mujibu wa mwongozo huo;

**19. UNABAINISHA** umuhimu wa COP30 inayokuja huko Belem, Brazili, katika kujenga imani zaidi na kushughulikia mahitaji ya kupata matarajio na utekelezaji wa juhudi zote za kukabiliana na tabianchi ifikapo 2030 kwa kuzingatia matarajio na ahadi za Baku;

**20. UNATAMBUA PIA** kwa shukrani matamko na ahadi kabambe zilizotolewa wakati wa COP29.

**21. UNAELEZEA WASIWASI WAKE** kuhusiana na tabianchi na mazingira kwa kuzingatia hatua, sera na kodi kwa upande mmoja na athari zake kwa mauzo na biashara ya Afrika; na **UNATOA WITO** kwa mazungumzo kuhusu hatua kama vile Utaratibu wa Marekebisho ya Mipaka ya Kaboni ya Umoja wa Ulaya, Kanuni za Ukataji Misitu za Umoja wa Ulaya, Sheria ya Kupunguza Mfumuko wa Bei, miongoni mwa nyinginezo ili kuelewa athari zake kwa uchumi wa Afrika, ikiwa ni pamoja na ustawi wa pamoja katika kipindi cha mpito cha kupunguza joto na kuhimili tabianchi katika harakati zao za kuleta maendeleo endelevu.

**22. UNATOA WITO KWA** Wanachama wote wa UNFCCC kuendeleza matokeo kuelekea ustawi wa pamoja chini ya Mpangokazi wa Mpito wa Haki, ikijumuisha kupitia Mfumo wa Mpito wa Haki ambao unakuza ushirikiano wa kimataifa unaowezesha kushughulikia mapungufu ya kimuundo na kimfumo kwa mchango mzuri wa nchi za Afrika katika mabadiliko; na **UNASISITIZA** umuhimu wa mpito wa haki, utaratibu, na usawa kutoka kwenye mifumo ya nishati inayotegemea mafuta.

**23. UNAPONGEZA** kazi ya Tume za Tabianchi za Afrika, Mpango wa ClimDev -Africa katika kuratibu utekelezaji wa mwitikio wa Afrika kwa Mabadiliko ya Tabianchi na **UNATOA WITO** uratibu madhubuti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika ili kuongeza utekelezaji wa mipango hii na kuongeza athari chanya zilizoratibiwa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi barani Afrika.

**24. UNAIPONGEZA** Afreximbank kwa msaada unaotolewa kwa Kamisheni katika eneo la mabadiliko ya tabianchi, ikijumuisha michango katika Banda la Afrika wakati wa Mikutano ya Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi.

**25. UNAIOMBA** Afreximbank kujiunga na Mpango wa CLIMDEV – Afrika chini ya uongozi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika kusaidia Nchi Wanachama na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda katika utekelezaji wa hatua za kukabiliana na tabianchi barani Afrika.

**26. UNATAMBUA** kwa shukrani msaada wa ziada unaotolewa na washirika wote kwa Kundi la Wapatanishi wa Afrika, hasa na Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mpango wa ClimDev Afrika, na Washirika wengine;

**27. UNAIPONGEZA** Kamisheni, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika, AUDA-NEPAD, Africa Risks Capacity na AfreximBank kwa ufanisi wa Banda la Afrika katika COP29 na **UNAWAOMBA** wote kuendelea kuunga mkono na kujiunga na ushirikiano wa kitaasisi wa Afrika kwa ajili ya UNFCCC COP29;

**28. UNAZIHIMIZA** Nchi Wanachama kuhakikisha kwamba Kundi la Wapatanishi wa Kiafrika ni uwakilishi na lina wajumbe rasmi kutoka kwa kila Nchi Wanachama, **UNASISITIZA** umuhimu mkubwa wa kufuata uwakilishi sawa wa makundi yote madogo ya Afrika katika mashirika na fedha tofauti zilizobuniwa chini ya UNFCCC na Makubaliano yake ya Paris, na **UNAIOMBA** AGN hii kuhakikisha utekelezaji kamili wa utaratibu huu;

**29. UNALIHIMIZA** Kundi la Wapatanishi wa Kiafrika kuzingatia mazungumzo katika mwelekeo wa kanuni ya ufadhili na kuacha maendeleo ya programu kwa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, AUDA-NEPAD na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda miongoni mwa zingine;

**30. UNAIPA MAMLAKA** Kamati Ndogo ya Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC) ya Masuala ya Mazingira kufuta hati zote zitakazojadiliwa na vikao vijavyo vya CHOSCC kwa kuzingatia Kanuni za Taratibu zinazoongoza Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU.

**31. UNATHAMINI** juhudi za Kamisheni katika kushughulikia vikwazo vinavyohusiana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya tabianchi na **UNAIPONGEZA** Kamisheni na washirika katika utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo ya AU na Mpangokazi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (2022-2032) na Mpangokazi wa Utunzaji Mazingira;

**32. UNAZITAKA** Nchi Wanachama kubuni mikakati ya kitaifa na ya kina kwa ajili ya madini muhimu au yasiyo na athari za kimazingira na masoko ya kaboni yanayowiana na maono mapana ya maendeleo na vipaumbele na kuzingatia mnyororo mzima wa

thamani kutoka kwenye utafiti hadi utumiaji wa mwisho; na kuimarisha mifumo ya kisheria na udhibiti wa madini muhimu au yasiyo na athari za kimazingira na masoko ya kaboni;

33. UNAIOMBA Kamisheni kuharakisha utekelezaji wa Mkakati wa AU wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo ya Kuhimili, Mpangokazi wa AU wa Utunzaji wa mazingira wa AU na Azimio la Viongozi wa Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na **UNAWAHIMIZA** washirika wa maendeleo na Mashirika ya ufadhili ya bara kuunga mkono juhudi hizi.

**34. UNAZINGATIA** kuzinduliwa kwa Mpango wa Uwekezaji wa Unaziongatia Mazingira barani Afrika (AGII) katika COP28 mwaka 2023, unaolenga kuendeleza mageuzi ya Afrika nzima kupitia ukuaji wa viwanda unaozingatia mazingira, unaowiana na Azimio la Viongozi wa Afrika la Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua wa mwaka 2023;

**35. UNAKARIBISHA** kuanzishwa kwa Sekretarieti ya AGII kama chombo cha kitaalamu cha kusimamia shughuli za kila siku, kuratibu maendeleo ya sera ya bara, na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji Unaozingatia Mazingira Afrika, na **UNAIOMBA** Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) kusaidia utekelezaji wa AGII, na UNATOA WITO kwa Washirika wa Maendeleo, Wadau wa Sekta Binafsi, na wadau wengine husika kutoa msaada unaohitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa AGII

**36. UNAMUOMBA** Mhe. Dkt. William Samoei Ruto, Rais wa Jamhuri ya Kenya na Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC), kusimamia utekelezaji wa uamuzi huu na kuripoti maendeleo katika Mkutano wa Ujao wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

**37. UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Des.15(XVI) Add.3, ambao ulifanya bioanuwai kuwa mojawapo ya vipaumbele vya AU. **UNATAMBUA** umuhimu wa uchumi unaotegemea bioanuwai katika maisha na ukuaji wa uchumi wa Afrika. **UNAAMUA** kufanya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Bioanuwai mwaka 2025 ili kuvutia uwekezaji na kuchochea biashara iliyodhibitiwa ya bioanuwai, kuhakikisha uendelevu wa rasilimali za kibiolojia na kusaidia jamii tegemezi katika bara hili na UNAIOMBA Kamisheni kukusanya rasilimali kwa ajili yake na kutoa wito kwa Nchi Wanachama kujitolea kuwa mwenyeji.

**38. UNATOA WITO PIA** kwa washirika kuunga mkono kuitishwa kwa Mkutano wa Kwanza wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Bioanuwai wa Afrika kwa manufaa ya bara na kimataifa.

**39. UNAHIMIZA ZAIDI** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele katika kuongeza uwekezaji wa fedha za tabianchi katika kilimo na sekta zinazohusiana na zinazoelekezwa kwa wazalishaji wa chakula, hasa wakulima wadogo ili kusaidia kuongeza uwezo wao wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**40. UNAONESHA** uharaka wa kushughulikia uhamiaji wa binadamu katika muktadha wa mabadiliko ya tabianchi na mazingira, pamoja na fursa za kutumia kushughulikia uhamiaji katika kukabiliana na hali, na mabadiliko ya haki na kuelekea maendeleo ya muda mrefu, endelevu; **UNAZITAKA** Nchi za Afrika kufanya kazi kwa ushirikiano na Kamisheni ya Umoja wa Afrika katika juhudi zake za kuendeleza Azimio la Mawaziri la Kampala kuhusu Uhamiaji, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

**41. UNAZINGATIA** kuongezeka kwa kasi na ukubwa wa majanga barani Afrika kama vile ukame, mafuriko na vimbunga. **UNATAMBUA** juhudi zinazoendelea za kukabiliana na athari za maafa haya kwa njia ya uandaaji wa taarifa za hatari, uundaji wa sera na taasisi zinazohusika na kupunguza hatari za maafa katika nchi wanachama na RECs, uundaji wa Mfumo wa Tahadhari wa Afrika na Hatua za Mapema (AMHEWAS) na uanzishwaji wa Ofisi husika katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika na upanuzi wake kwa RECs na Nchi Wanachama, na utayarishaji unaoendelea wa ripoti za mapitio ya kila baada ya miaka miwili ambayo hutunza taarifa kuhusu hali ya DRR katika Afrika..

**42. UNATHAMINI** jukumu la Kinara wa AU kuhusu Usimamizi wa Hatari za Maafa, Mhe. Filipe Jacinto Nyusi, aliyekiuwa Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, hasa katika suala la kuboresha uhamasishaji wa usimamizi wa hatari za maafa. **PIA UNAZINGATIA** Mpango wa Tahadhari ya Mapema kwa WOTE wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

**43. UNAZINGATIA** kuongezeka kwa kasi na ukubwa wa majanga barani Afrika kama vile ukame, mafuriko na vimbunga na umuhimu wa kuimarisha hatua za kukabiliana na hali hiyo katika bara zima. **UNATAMBUA** hitaji la dharura la kutoa tahadhari za mapema na mbinu za kukabiliana na majanga barani Afrika.

**44. UNATOA WITO KWA** Nchi Wanachama na Kamisheni kuharakisha uanzishaji wa Mfumo wa Uwezo wa Kiraia wa Bara kuhusu Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa.

**45. UNAAMUA** kuwa Mpango wa AMHEWAS ndio chombo kikuu cha Afrika cha kutekeleza shughuli za tahadhari za mapema ikiwa ni pamoja na utumiaji wa Mpango wa Tahadhari ya Mapema kwa WOTE.

**46. UNARIDHISHWA** na matokeo ya mkutano wa ngazi ya juu wa rais uliofanyika wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Viongozi wa Dunia wa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi, ulioitishwa kwa pamoja na Mhe. Denis SASSOU N'GUESSO, Rais wa Jamhuri ya Congo, Mwenyekiti wa Tume ya Bonde la Mto Congo, Dkt. William RUTO. Jamhuri ya Kenya, Mratibu wa CAHOSCC na Dkt. AKINWUMI A. ADESINA, Rais wa Kundi la Benki ya Maendeleo ya Afrika.

**47. UNAAMUA** kuitisha mkutano wa pande zote wa wafadhili kufadhili miradi, ikijumuisha Mkutano wa 30 wa Wanachama wa COP30 kwa UNFCCC huko Belem, Brazili.

**48. UNABAINISHA** kwamba wakati Afrika inatoa bidhaa za umma za mazingira duniani, Pato lake la Ndani (GDP) halizingatii mtaji wake mkubwa wa asili, kwa kiasi kikubwa kudharau Pato la Taifa na utajiri wa Afrika.

**49. UNATAMBUA** hitaji la thamini inayofaa wa mali asili ya Afrika ili kuvutia mtiririko mkubwa wa kifedha, kuboresha viwango vya mikopo, na kupanua ufikiaji wa nchi kwa fedha zinazohusiana na mazingira kwa ajili ya uwekezaji unaohimili tabianchi.

**50. UNAZINGATIA** matokeo ya UNCCD COP 16 iliyofanyika kuanzia tarehe 02-13 Disemba 2024 mjini Riyadh, Saudi Arabia na **UNAUPONGEZA** Ufalme wa Saudi Arabia kwa kuandaa COP yenye mafanikio.

**51. UNAKARIBISHA** uzinduzi wa Ubia wa Kuhimili Ukame wa Riyadh ambao ulipokea ahadi za zaidi ya dola bilioni 12.

**52. UNAKARIBISHA** matokeo ya Mkutano wa Pembezoni wa Ngazi ya Juu uliofanyika Baku, Azerbaijan, wakati wa Mkutano wa Viongozi wa Dunia katika COP29 kuhusu "Kupima Utajiri wa Kimazingira wa Afrika" na athari zake kwa sera ya tabianchi na mabadiliko ya mazingira.

**53. UNAKARIBISHA** ahadi za kifedha zilizotolewa na COP kusaidia programu ya Great Green Wall Initiative na **UNATOA WITO** wa kuwa na mpango ulioratibiwa zaidi chini ya uangalizi wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kuwa na uangalizi wa Bara wa mipango inayohusu Sahel, Sahara na Kusini mwa Afrika (SADC).

**54. UNAIOMBA** Kamisheni na Taasisi nyinginezo za Afrika kusaidia Kundi la Afrika la Wanaohusika na Majadiliano kuhusu hali ya Jangwa katika kuendeleza Msimamo wa Pamoja katika kuelekea UNCCD COP 17 iliyopangwa kufanyika nchini Mongolia, kwa kusaidia kifedha na kitaalamu kuandaa mikutano ya Maandalizi ya Afrika mwaka 2026 na kutoa kujenga uwezo na kubadilishana maarifa kuhusu Makubaliano mengine ya RIO.

**55. UNATOA WITO** kwa Kamisheni na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuanzisha timu ya kitaalamu ya wataalam ili kushirikiana na nchi nyingine zinazoendelea na kanda za dunia, hasa Amerika ya Kusini na Karibiani, pamoja na Asia, kuunda muungano imara wa kimataifa ili kuhakikisha kuingizwa kwa mtaji asilia katika Pato la Taifa la mataifa.

**56. UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Afrika Kusini kwa kutwaa Urais wa G20 kwa 2025; na **UNAZINGATIA** vipaumbele na mapendekezo yanayoweza kutekelezwa kwa Urais wa Afrika Kusini wa Kikosi Kazi cha G20 cha Mazingira na Uendelevu wa Tabianchi (ECSWG) na kuiomba Kamisheni ya AU iitishe mkutano wa mashauriano na Nchi Wanachama wa AU ili kuyajadili kabla ya Mkutano wa kwanza wa G20 ECSWG Machi 2025.

**57. UNAMPONGEZA** Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanikisha Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika jijini Dar Es Salaam na kuwa kinara wa Mission 300 na Njia Safi za Mapishi (Clean Cooking Solutions) barani Afrika; na **UNATHAMINI** uungwaji mkono wa Kamisheni, Kundi la Benki ya Maendeleo ya Afrika na Kundi la Benki ya Dunia katika kuandaa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nishati wa Mission 300 Africa;

**58. UNAPITISHA** Azimio la Dar es Salaam kuhusu Mkutano wa Nishati wa Mission 300 Africa kuhusu kutoa huduma ya umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030;

**59. UNAIHIMIZA** Kamisheni kushirikiana na Nchi Wanachama, RECs, Benki ya Maendeleo ya Afrika, na washirika wengine katika kutekeleza Azimio la Dar es Salaam; na,

**60. UNAITAKA** Kamisheni kutoa taarifa mara kwa mara kuhusu utekelezaji wa Azimio, ikionyesha mafanikio muhimu, changamoto na mapendekezo ya hatua zaidi.

## UAMUZI WA
## KUPITISHA RASIMU ZA HATI ZA KISHERIA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Mapendekezo ya Baraza la Mawaziri ya kujadili na kuidhinisha Rasimu za nyaraka za Kisheria;

2. **UNAIDHINISHA** Rasimu zifuatazo za nyaraka za Kisheria:

   *(i)* *Rasimu ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana;*

   *(ii)* *Rasimu ya Katiba ya Shirika la Usalama wa Chakula wa Afrika; na*

   *(iii)* *Rasimu ya Viambatisho vya Protokali ya Makubaliano ya Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Afrika la Biashara ya Kidijitali:*
   - *a) Rasimu ya Kiambatisho cha Kanuni za Uasili*
   - *b) Rasimu ya Kiambatisho cha Vitambulisho vya Kidijitali*
   - *c) Rasimu ya Kiambatisho cha Malipo ya Kidijitali ya Mpakani*
   - *d) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Uhamishaji wa Data wa Mpakani*
   - *e) Rasimu ya Kiambatisho kuhusu Vigezo vya Kuamua Sababu Halali na za Kisheria za Kfichua Msimbo*
   - *f) Rasimu ya Kiambatisho cha Usalama na Ulinzi Mtandaoni*
   - *g) Rasimu ya Kiambatisho cha Teknolojia Zinazochipukia na Zilizostawi*
   - *h) Rasimu ya Kiambatisho cha Teknolojia ya Kifedha*

   *(iv)* *Rasimu ya Mkataba wa Mfumo wa Bara wa Uwezo wa Raia kwa ajili ya Majanga, Utayari*

3. **UNATOA WITO** kwa Nchi Wanachama kuridhia nyaraka hizi za kisheria, pale inapohitajika, ili kuhakikisha zinaanza kutekelezwa haraka.

# UAMUZI KUHUSU UTEUZI WA WAJUMBE WATANO (5) WA BARAZA LA AMANI NA USALAMA LA UMOJA WA AFRIKA

**Mkutano Mkuu**,

**1. UNAZINGATIA** uchaguzi wa Wajumbe watano (5) wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika unaofanywa na Baraza Kuu;

**2. UNATEUA** Nchi Wanachama nne (4) zifuatazo kwenye Baraza la Amani na Usalama kwa kipindi cha miaka mitatu (3):

| NA. | NCHI | KANDA |
|---|---|---|
| 1. | Cameroon | Kati |
| 2. | Ethiopia | Mashariki |
| 3. | Eswatini | Kusini |
| 4. | Nigeria | Magharibi |

**3. UNAZITANGIA** kuahirishwa kwa uchaguzi wa Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kutoka Kanda ya Kaskazini hadi Mkutano Maalumu wa Ishirini na Nne Baraza Kuu.

**4. UNAAMUA** kukasimu kwa namna ya pekee mamlaka yake ya uteuzi kwa Mkutano Maalumu wa 24 wa Baraza Kuu ili kumteua mjumbe aliyechaguliwa wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kutoka Kanda ya Kaskazini.

## UAMUZI KUHUSU UTEUZI WA WAJUMBE WA JOPO LA WENYE BUSARA

**Mkutano Mkuu,**

**1. UNAREJELEA** Ibara ya 11 ya Protokali inayohusiana na Kuanzishwa kwa Baraza la Amani na Usalama (PSC) la Umoja wa Afrika, ambalo inaamuru kuanzishwa kwa Jopo la Wenye Busara ili kuunga mkono juhudi za PSC na Mwenyekiti wa Kamisheni, hasa katika eneo la kuzuia migogoro na Mpango wa utendaji kazi wake uliopitishwa tarehe 12 Novemba 2007;

**2. UNAREJELEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU/Des.824(XXXV) uliopitishwa katika Mkutano wa 35 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali uliofanyika Addis Ababa Februari 2022 na Uamuzi wa EX.CL/Dec.1183(XLI) wa Mkutano wa 41 wa Kawaida wa Baraza Kuu, ambao ililiteua Jopo la 5 la Wenye Busara kwa muda wa miaka mitatu ambao ulikamilika Februari 2025;;

**3. UNATOA SHUKRANI ZA DHATI** kwa kujitolea na michango ya watu mashuhuri katika kuendeleza amani, usalama na utulivu katika bara zima kupitia diplomasia ya kuzuia, ziara za kutafuta ukweli na juhudi za upatanishi za wajumbe wanaomaliza muda wao—ambao ni,

- Mhe. Domitien Ndayizeye (Burundi),
- Mhe. Amr Mahmoud Abu Zaid Moussa (Misri),
- Mhe. Jaji (Mstaafu) Effie Owuor (Kenya),
- Profesa Babacar Kanté (Senegal), na
- Mhe. Phumzile Mlambo-Ngcuka (Afrika Kusini)

**4. UNAWAPONGEZA** Wakuu wa Wanadiplomasia wa Afrika kwa ujumla na kikanda kwa kuwezesha mchakato wa uteuzi wa uwazi na wa mashauriano kwa Jopo la 6 la Wenye Busara;

**5. UNATAMBUA** kuongezeka kwa matatizo na vitishio vinavyojitokeza kwa amani na usalama barani Afrika, ambavyo vinahitaji Jopo lililo na rasilimali za kutosha, lililowezeshwa, na tendaji lenye uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazoendelea na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

**6. UNAMUA**, kwa mujibu wa Ibara ya 11(2) ya Protokali ya PSC, kuteua watu wafuatao wanaoheshimika sana kama wajumbe wa Jopo la 6 la Wenye Busara kwa muda wa miaka mitatu, kuanzia Februari 2025:

• **Eneo la Afrika ya Kati**: Mhe. Domitien Ndayizeye, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Burundi (ameteuliwa tena);
• **Kanda ya Afrika Mashariki**: Mhe. Jaji (Mst) Effie Owuor, Jamhuri ya Kenya (ameteuliwa tena);

• **Kanda ya Kusini mwa Afrika**: Mhe. Phumzile Mlambo-Ngcuka, Jamhuri ya Afrika Kusini (ameteuliwa tena).

**7. UNAMWAGIZA** Mwenyekiti anayekuja wa Kamisheni kushauriana na Kanda za Afrika Magharibi na Kaskazini ili kuchagua mgombea mmoja (1) kwa kila kanda kwa kuzingatia maridhiano ya nafasi hizi zilizo wazi na kuwasilisha kwenye Mkutano wa Kawaida wa 47 wa Baraza Kuu;

8. Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) ya Kanuni za Uendeshaji za Mkutano Mkuu kuhusu Kukaimisha Mamlaka, **UNAAMUA KUKUKASIMU** kwa Mkutano wa 47 wa Kawaida wa Baraza Kuu mamlaka ya kuteua wawakilishi kutoka Kanda za Magharibi na Kaskazini mwa Afrika ili kukamilisha muundo wa Jopo la 6 la Wenye Busara;

**9. UNASISITIZA** umuhimu mkubwa wa kulipatia Jopo la Wenye Hekima usaidizi unaohitajika wa kitaasisi, kifedha, na wa vifaa ili kuhakikisha uwezo wake kamili wa kiutendaji na uhuru katika kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na:

• Kuimarisha diplomasia yake ya kuzuia, mipango ya kutafuta ukweli wa mambo, na ushirikiano na wadau wa kitaifa, kikanda na bara;
• Kuimarisha uwezo wake wa kuchukua hatua za haraka katika maeneo yenye mizozo kupitia njia zinazolengwa za tahadhari na kuchukua hatua za mapema;
• Kuongeza upatikanaji wake wa rasilimali za msaada wa upatanishi, utafiti, na utaalamu ili kuandaa mikakati inayoweza kutekelezeka ya kuzuia na kutatua migogoro.

**10. UNAZIHIMIZA** Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika kutoa ushirikiano wao kamili na kuwezesha kazi ya Jopo kwa ari ya uwajibikaji wa pamoja wa amani na usalama katika bara hili;

**11. UNAMWOMBA** Mwenyekiti wa Kamisheni kuweka kipaumbele katika ugawaji wa rasilimali za kutosha kwa Jopo la Wenye Busara katika bajeti ya mwaka na kukusanya msaada wa ziada kutoka kwa washirika ili kuimarisha kazi yake, hasa katika diplomasia ya kuzuia na upatanishi.

**UAMUZI**
**KUHUSU RIPOTI JUU YA UENDESHAJI WA TUZO YA UBORA YA COTE D'IVOIRE-CERFAM YA KUIMARISHA LISHE NA USALAMA WA CHAKULA (*Suala lililopendekezwa na Jamhuri ya Côte D'Ivoire*) – DOC. Assembly/AU/21 (XXXVIII)**

Mkuu Mkuu,

**1. UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.892(XXXVII) kuhusu ripoti za Vinara wa Afrika na Viongozi wa Mpango wa Lishe (ALN) na kuongezwa kwa muda wa (2024-2026) wa Mfalme ETSIE III, Mfalme wa Lesotho na Kinara wa Umoja wa Afrika wa Lishe, ili kumwezesha Mwanachama wa Umoja wa Afrika kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Lishe wa Afrika uliandaliwa chini ya Azimio la Malabo;

**2. UNAUPONGEZA TENA** uongozi wa Mhe. ALASSANE OUATTARA, Rais wa Jamhuri ya Côte d'Ivoire, kwa uhamasishaji wake na wenzake kuhusu kupitishwa kwa kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya 2022 kuhusu lishe na usalama wa chakula na pia kwa ajili ya kufanya mkutano wa ngazi ya juu wa lishe ulioandaliwa kwa pamoja na Côte d'Ivoire na Umoja wa Afrika tarehe 8 Desemba 2022 uliohudhuriwa Mtukufu Mfalme wa Lesotho wa ETSI III.

**3. UNAZINGATIA** Azimio la Abidjan/AU/Decl.3(XXXVII) kuhusu kaulimbiu ya Umoja wa Afrika ya mwaka 2022 kuhusu lishe ambalo **LINATOA WITO WA KUCHUKULIWA HATUA** "kuharakisha uwekezaji, utekelezaji na uratibu ili kuboresha lishe na usalama wa chakula barani Afrika";

**4. UNAAMUA** kuanzisha Tuzo ya Ubora ya "Côte d'Ivoire-CERFAM kwa kuimarisha Lishe na Usalama wa Chakula" ambayo inalenga kuheshimu watu, taasisi, mashirika ya umma au binafsi na mashirika hai yasiyo ya kiserikali ambayo yamefanya shughuli madhubuti kutoa mchango mkubwa katika kupunguza utapiamlo na njaa barani Afrika na duniani kote;

**5. UNAPITISHA** hatua kuu zilizochukuliwa na Côte d'Ivoire kuendesha Tuzo hii kama sehemu ya upanuzi wa shughuli za Kituo cha Kikanda cha Ubora Dhidi ya Njaa na Utapiamlo (CERFAM) kilichowekwa mikononi mwa Afrika na ambacho kinalenga kubainisha mbinu bora za mapambano dhidi ya njaa na utapiamlo barani Afrika na kukidhi haja ya Ushirikiano wa Nchi Wanachama wa Afrika Kusini na Umoja wa Afrika Kusini;

6**. UNAPITISHA** taratibu za uendeshaji wa tuzo hii kuwa:

- itatolewa kila baada ya miaka miwili kuanzia 2027 na kiasi cha FCFA milioni 100, sawa na euro 152,000, kwa nafasi ya kwanza, ya pili na ya tatu moja;

- inayofadhiliwa kupitia riba inayotokana na uwekezaji wa awali wa rasimali uliokusudiwa kuhakikisha uendelevu wake kwa angalau miaka 20. Mtaji huu utafadhiliwa na nchi ya Côte d'Ivoire;

- kuwekwa chini ya uangalizi wa aliyekuwa Mkuu wa Nchi wa Afrika ambaye atakuwa kielelezo cha maadili na malengo yake; na

- kusimamiwa na Kituo cha Kikanda cha Ubora Dhidi ya Njaa na Utapiamlo (CERFAM) chenye makao yake mjini Abidjan, na ambacho ndicho chombo kikuu cha Tuzo;

**7. UNAIHIMIZA** Côte d'Ivoire kujumuisha maelezo mahususi na taratibu za uendeshaji wa Tuzo hii ili kuhakikisha utekelezaji wake halisi mwaka 2027; na

**8. BADO** unaamini kwamba "Tuzo ya Ubora ya Côte d'Ivoire-CERFAM ya Lishe na Usalama wa Chakula" itaimarisha shughuli za lishe katika bara.

# UAMUZI
# KUHUSU KUWA MWENYEJI WA MKUTANO WA TATU WA AFRIKA WA UTEKELEZAJI NA USHIRIKIANO (PANAFCON-3) KUANZIA TAREHE 27-29 MEI, 2025 HUKO LUSAKA, ZAMBIA (Suala lililopendekezwa na Jamhuri ya Zambia)
**Doc. Assembly/AU/22(XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** matokeo ya Mkutano wa Kawaida wa 5 wa Kamati Maalum ya Kitaalamu kuhusu Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Uchumi wa Buluu, Maji na Mazingira (STC ya ARBWE) uliofanyika Novemba 2023, ambao ulisisitiza jukumu muhimu la Nchi Wanachama na kuzihimiza kushiriki kikamilifu katika michakato inayoendelea ya kuunda Dira na Sera ya Maji ya Afrika baada ya mwaka 2025.

2. **PIA UNAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1234(XLIV) aya ya II/39 unaoitaka Kamisheni kuandaa Sera ya Maji ya Afrika inayotoa mpango wa kimkakati kuelekea usalama wa maji jumuishi na unaostahimili mabadiliko ya tabianchi barani baada ya mwaka 2025.

3. **UNATAMBUA** uongozi na kujitolea kwa Jamhuri ya Zambia kuwa mwenyeji, wa Mkutano wa tatu wa Afrika wa Utekelezaji na Ushirikiano kuhusu Maji (PANAFCON-3,) wa tarehe 27 – 29 Mei 2025 kama sehemu ya utekelezaji wa Uamuzi wa AMCOW GA/13/2023/CAI/1 wa kufanya mchakato wa mazungumzo wa ngazi mbalimbali ili:
   a. kuhakikisha ushiriki mpana na hai wa wadau katika kipaumbele cha mapendekezo ya kitaalamu na uundaji wa mfumo wa utekelezaji wa Dira na Sera ya Maji ya Afrika baada ya 2025;
   b. kuhakikisha umiliki wa kisiasa wa Dira na Sera na, hivyo kujizatiti kikamilifu kuitekeleza kwa pamoja na kuweka mkazo katika kuunda hoja ya kibiashara kwa uchumi wa maji na usafi wa mazingira kama sababu muhimu ya mafanikio ya sera ya fedha ya kitaifa; na,,
   c. kuhakikisha kwamba Dira na Sera ya Maji ya Afrika baada ya 2025 inaendana na inapitishwa kama mfumo wa utekelezaji wa Ajenda ya mwaka 2063;.

4. **UNATOA WITO** wa ushiriki mpana na ushirikishwaji wa wadau wote ili kupitia rasimu ya awali ya dira na sera ya maji ya Afrika baada ya 2025 kwa kuhakikisha usalama wa maji jumuishi na unaohimili mabadiliko ya tabianchi barani;

5. **UNAZIAGIZA** Nchi Wanachama, RECs, Kamisheni, AMCOW, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Kamisheniya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika, washirika wa maendeleo, wataalamu, washirika wa uratibu na utekelezaji, sekta binafsi na wadau wote kuhakikisha mafanikio ya mkutano na utekelezaji wa matokeo yake;

6. **INARUDIA KUSISITIZA** haja ya kuhakikisha uongozi wa kisiasa thabiti, kujizatiti na kuunga mkono ufanikishaji wa makubaliano ya Mkutano;

7. **UNATOA WITO** kwa Mheshimiwa Rais Hakainde Hichilema wa Jamhuri ya Zambia, akisaidiwa na uongozi wa Kamati ya Mawaziri ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira ya STC ya ARBWE, kuongoza na kuhamasisha utekelezaji wa matokeo ya PANAFCON-3 na kuwasilisha, kwa ajili ya kujadiliwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi utekelezaji wa dira na sera inayowiana na itakayochochea hatua za kufanikisha Tarajio la 1 la Ajenda 2063 la "Afrika yenye mafanikio inayojikita kwenye ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu";

8. **UNATOA WITO ZAIDI** kwa Jamhuri ya Zambia na uongozi wa Kamati ya Mawaziri ya Sekta ya Maji na Usafi wa Mazingira ya STC ya ARBWE kuhakikisha mafanikio ya Mkutano na mchango wa Dira na Sera ya Maji ya Afrika baada ya 2025 katika kushawishi ajenda ya kimataifa kuhusu maji na usafi wa mazingira.

# UAMUZI
# KUHUSU TAARIFA YA MAANDALIZI YA TOLEO LA 4 LA JUKWAA LA AFRIKA LA UTAMADUNI WA AMANI NA UTULIVU "LUANDA BIENNIAL" (*Suala lilopendekezwa na Jamhuri ya Angola*)

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZIPONGEZA** Serikali ya Jamhuri ya Angola, AU, na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuhusu sasisho la maandalizi ya Toleo la 4 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Utulivu "Biennale of Luanda", ambayo itafanyika katika awamu mbili (2), haswa kutoka tarehe 2 hadi 4 Julai, na tarehe 12 -13 Novemba, 2025, mjini Luanda, Jamhuri ya Angola.

2. **UNATAMBUA** uhusiano uliopo kati ya kaulimbiu ya Toleo la 4 la Jukwaa la Kimajumui la Utamaduni wa Amani na Utulivu "*Biennale of Luanda",* **"Kuthamini Yaliyopita, Kuthamini Mafanikio, Kujenga Afrika Tunayoitaka"** na kaulimbiu ya Umoja wa Afrika kwa mwaka 2025, **"Haki kwa Waafrika na Wazawa wa Kiafrika kupitia Fidia."**

3. **UNAIAGIZA** Kamisheni na UNESCO kuandaa na kukuza shughuli na programu zinazohusiana na kaulimbiu ya Toleo la 4 la Jukwaa la Kimajumui la Utamaduni wa Amani na Utulivu "*Biennale of Luanda*" katika mwaka 2025.

4. **UNAZIOMBA** Nchi Wanachama na RECs kujumuisha shughuli zinazohusiana na kaulimbiu ya Toleo la 4 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Utulivu "Biennale of Luanda*"* kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kaulimbiu ya mwaka 2025.

5. **UNATAMBUA** kazi muhimu inayotekelezwa na Jukwaa la Kimajumui kwa ajili ya Utamaduni wa Amani na Utulivu "B*iennale of Luanda*" katika kukuza amani na utulivu katika bara zima.

6. **UNAZINGATIA** muundo wa Toleo la 4 la Jukwaa la Kimajumui la Utamaduni wa Amani na Utulivu "*Biennale of Luanda*," ambalo litajumuisha awamu mbili (2), yaani, tarehe **2 hadi 4 Julai , 2025 kwa** Mdahalo wa Vizazi katika ngazi ya mawaziri, Midahalo, na Matukio Sambamba, na kwa upande mwingine, tarehe **12 hadi 13 ya Novemba, 2025,** kwa Sherehe za Ufunguzi wa Ngazi ya Juu, Uwasilishaji wa matokeo ya midahalo ya Julai, Uzinduzi wa maonyesho makuu (yakionyesha michango ya mafanikio ya kipekee na urithi wa watu mashuhuri wa Kiafrika na wanaoishi nje ya nchi kwa maendeleo ya binadamu), Ajenda ya Utamaduni - Tamasha la Tamaduni.

7. **UNATOA WITO wa** Ushiriki hai wa Nchi Wanachama na RECs katika Toleo la 4 la Jukwaa la Afrika la Utamaduni wa Amani na Utulivu "*Biennale of Luanda".*

**UAMUZI**
**KUHUSU HAKI ZA KIJAMII BARANI AFRIKA : KUKUZA MAENDELEO YA KIUCHUMI, KIJAMII NA MAZINGIRA YANAYOZINGATIA WATU**
**(*Suala lililopendekezwa na Tunisia*)**
**Doc. Assembly/AU/24(XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

**UKIREJELEA** Sheria ya Kuanzisha UA na Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu, ambazo zinasisitiza Umoja kujizatiti katika usawa, utu wa binadamu, na maendeleo endelevu,

**PIA, UKIREJELEA** misingi ya kuundwa kwa Shirika la Umoja wa Afrika (OAU) na UA, ambayo ilisisitiza usawa, utu, na kutokomeza tofauti za kijamii na kiuchumi, na **UKISISITIZA** maadili haya ya Ajenda ya mwaka 2063, ambayo inazingatia maendeleo ya watu kama kiini cha ajenda ya mageuzi ya Afrika huku ikihamasisha ukuaji wa uchumi jumuishi, usawa wa kijamii, na uendelevu katika masuala ya mazingira.

**UKITAMBUA** jukumu muhimu la Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu hususani Ibara za 13, 15, na 22, katika kuhakikisha utawala ujumuishi, haki ya kazi yenye staha, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi yenye usawa.

**UKIUPONGEZA** uongozi wa Afrika katika Muungano wa Kimataifa wa Haki za Kijamii, uliozinduliwa na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO), kama ishara ya kujizatiti katika utangamano wa kimataifa kwenye kukuza haki za kijamii, kazi zenye staha, na maendeleo endelevu.

**UKIKARIBISHA** kupitishwa kwa mpango mkakati wa miaka 10 wa Uchumi na Mshikamano wa Kijamii (SSE) wa Umoja wa Afrika (2024), ambao unalenga kukuza mfano wa uchumi unaozingatia watu unaendana na Ajenda ya mwaka 2063, na **UKITAMBUA** juhudi za Kamati Maalum ya Kitaalamu kuhusu Maendeleo ya Kijamii, Kazi na Ajira (STC-SDLE-5) katika kuendeleza Ajenda ya Kijamii ya Mwaka 2063.

**UKISISITIZA** umuhimu wa Azimio la AU la Ouagadougou+10 na Mpango wa Utekelezaji wa Ajira, Kutokomeza Umaskini, na Maendeleo Jumuishi Barani Afrika, uliopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali Januari 2015, kama muundo muhimu wa kukabiliana na changamoto za ajira, kijamii na kiuchumi.

**UKITAMBUA** jukumu muhimu la haki za kijamii katika kukuza ukuaji wa uchumi jumuishi, kutokomeza umaskini, kushughulikia usawa, na kuhakikisha uendelevu wa masuala ya mazingira.

**UKIREJELEA** Tarajio la 1 la Ajenda 2063, linaloazimia kuwa na Afrika yenye ustawi inayojikita katika ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu, na Tarajio la 6 linaazimia

"Afrika ambayo maendeleo yake yanaendeshwa na watu, ikitegemea uwezo wa watu wa Afrika, hususan wanawake na vijana, na kutunza Watoto."

**UKISIKITISHWA** na changamoto za kudumu za umaskini, ukosefu wa ajira, kutokuwa na usawa, na upatikanaji mdogo wa ulinzi wa kijamii katika bara lote.

**UKITAMBUA** umuhimu wa Mkutano wa Pili ujao wa Dunia kuhusu Maendeleo ya Kijamii kama jukwaa la kimataifa la kutetea mfumo wa maendeleo unaozingatia watu,

**UKIZINGATIA** kipengele kilichopendekezwa na Jamhuri ya Tunisia **"*Haki za Kijamii Barani Afrika: Kukuza Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii, na Masuala ya Mazingira Yanayozingatia Watu*"** kama kielelezo cha kujizatiti kwa bara la Afrika katika kushughulikia umaskini, ukosefu wa ajira, usawa, na mabadiliko ya tabianchi,

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAPONGEZA** pendekezo lililowasilishwa na Jamhuri ya Tunisia na **Unaidhinisha** "***Haki za Jamii Barani Afrika: Kukuza Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii, na Masuala ya Mazingira Yanayozingatia Watu***" kama kipengele cha kipaumbele kwa kaulimbiu ya kila mwaka ya Umoja wa Afrika ambayo itazingatiwa katika miaka inayokuja.

2. **UNAIOMBA** Kamisheni, kwa kushirikiana na Nchi Wanachama na wadau wanaohusika, kufanya upembuzi yakinifu wa utekelezaji madhubuti wa kaulimbiu hii. Upembuzi huu utachunguza mikakati, mifumo, na ushirikiano unaohitajika ili kujumuisha haki za kijamii katika mipango ya Umoja wa Afrika, kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi, kijamii, na masuala ya mazingira yanazingatia watu.
3. **UNAHIMIZA** Nchi Wanachama kuweka kipaumbele na kujumuisha misingi ya haki za kijamii katika sera za kitaifa, mikakati, na mipango ili kuharakisha maendeleo jumuishi na kukuza usawa katika nyanja za kiuchumi, kijamii, na katika masuala ya mazingira.

4. **UNAIAGIZA** Kamisheni:

   a. Kuandaa mpango jumuishi wa utekelezaji wa Kaulimbiu iliyotajwa hapo juu, ukiwa na malengo ya wazi, mikakati, na muda wa utekelezaji.

   b. Kuanzisha ushirikiano na wadau muhimu, ikiwamo mashirika ya kimataifa, taasisi za kifedha, mashirika ya wafanyakazi, na sekta binafsi, ili kuongeza rasilimali na utaalamu.

   c. Kuwezesha ujengeaji uwezo ili kukuza uwezo wa taasisi na rasilimali watu katika Nchi Wanachama.

5. **UNAZISIHI** Nchi Wanachama kushiriki kikamilifu katika Mkutano wa Pili wa Dunia kuhusu Maendeleo ya Kijamii utakaofanyika kuanzia **tarehe 4 hadi 6**

**Novemba 2025 huko Doha, Qatar** na kuwianisha michango yao na malengo ya Umoja wa Afrika, kuhakikisha Afrika inapaza sauti moja na yenye ushawishi katika kuunda matokeo ya kimataifa.

6. **UNAIOMBA** jumuiya ya kimataifa, ikiwamo mfumo wa Umoja wa Mataifa, Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO), na washirika, kuunga mkono jitihada za Afrika katika kukuza haki za kijamii kupitia msaada wa kitaalamu, kifedha, na kisera.
7. **UNATANGAZA** kaulimbiu ya "Haki za Jamii Barani Afrika: Kukuza Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii, na Masuala ya Mazingira Yanayozingatia Watu," kama mpango mkuu wa Umoja wa Afrika katika mwaka 2025, ikitumika kama msingi wa kutekeleza misingi ya haki za kijamii na kuendeleza mageuzi kote barani, na **UNAPENDEKEZA** kupitishwa kwa kaulimbiu ya mwaka ya AU inayotarajiwa katika miaka inayokuja.

# UAMUZI
# KUHUSU KUUCHUKULIA UTUMWA, UHAMISHAJI NA UKOLONI KUWA UHALIFU DHIDI YA UBINADAMU NA MAUAJI YA KIMBARI DHIDI YA WATU WA AFRIKA

***(Suala lililopendekezwa na Jamhuri ya Togo)***

**Doc. Assembly/AU/25 (XXXVIII)**

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** pendekezo lililotolewa na Jamhuri ya Togo kuhusu "*Kuuchukulia utumwa, uhamishaji na ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari dhidi ya watu wa Afrika*" na UNATAMBUA umuhimu wa kaulimbiu hii kwa bara la Afrika;

2. **UNAREJELEA**

   (i) Azimio la Mkutano wa Banjul kufuatia mkutano wa Timu ya Wataalamu kuhusu Utumwa na kufuatia Mkutano wa Dunia kuhusu Mapambano dhidi ya Ubaguzi wa rangi, uliofanyika kuanzia tarehe 10 hadi 13 Juni 2008 huko Banjul, Jamhuri ya Gambia;

   (ii) Azimio la Durban la mwaka 2001 lililopelekea Mkutano wa Dunia kuhusu Mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi, chuki dhidi ya wageni na hali ya kutovumiliana, ambao ulijadili kwa uwazi utumwa na biashara ya watumwa iliyovuka Atlantiki kama majanga ya kutisha katika historia ya ubinadamu na uhalifu dhidi ya ubinadamu;

   (iii) Azimio namba 61/19 la mwaka 2006 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambalo lilisisitiza kwamba "biashara ya utumwa na utumwa ni kati ya ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika historia ya ubinadamu, hususani kwa kiwango na muda wake";

   (iv) Azimio namba 62/122 la mwaka 2007 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lililoanzisha Siku ya Kimataifa ya Kuwakumbuka Waathirika wa Utumwa na Biashara ya Utumwa iliyovuka Bahari ya Atlantiki, itakayoadhimishwa kila mwaka kuanzia tarehe 25 Machi 2008;

   (v) Azimio la Abuja la Aprili 1993 kuhusu fidia iliyotokana na mkutano ambao UA ulikuwa mmoja wa wafadhili ambao ulitambua kuwa "kuna deni la kipekee na lisilo na kifani la kimaadili kwa watu wa Afrika ambao 'bado hawajalipwa - deni la fidia inayodaiwa na Waafrika kama watu waliodhalilishwa na kunyonywa zaidi katika karne nne zilizopita za historia ya sasa';

   (vi) Uamuzi EX.CL/Dec.408 (XII) wa mwaka 2009 kuhusu kumbukumbu ya kukomesha kwa utumwa;

   (vii) Utafiti uliofanywa na Kamisheniya Umoja wa Afrika ya Sheria za Kimataifa(CUADI) kuhusu msingi wa kisheria wa Fidia kwa biashara ya Utumwa wa kuvuka bahari ya Atlantiki na madhila mengi yaliyofanyika katika Bara la Afrika.

(viii) Uamuzi Assembly/AU/Dec.847(XXXVI) wa Mkutano ulioruhusu kufanyika kwa mkutano wa kimataifa mjini Accra kuhusu kuanzisha umoja wa kudai haki na malipo ya fidia kwa Waafrika uliopitishwa na Mkutano wake wa 36 wa Kawaida uliofanyika tarehe 18 na 19 Februari 2023 mjini Addis Ababa, Ethiopia;

(ix) Azimio la Mkutano wa Kimataifa wa Accra kuhusu Fidia, uliofanyika kuanzia tarehe 14 hadi 17 Novemba 2023;

(x) Uamuzi wa Mkutano mkuu Assembly/AU/Dec.884 (XXXVII) ambapo Mkutano huo ulipitisha kaulimbiu ya mwaka 2025, yaani, *“Haki ya Waafrika na watu wenye asili ya Afrika kulipwa fidia”*

(xi) Azimio la Jukwaa la Kimajumui la vijana, lililofanyika tarehe 1- 4 Novemba 2024 mjijini Oran (Algeria) ambalo lilipongeza kaulimbiu ya mwaka 2025 ya Umoja wa Afrika na kusisitiza umuhimu wa kuwarithisha vizazi vya vijana tunu na misingi iliyochagiza harakati za kishujaa za wahenga wetu na wa Afrika kwa ajili ya uhuru, haki na utu;

3. **UNASISITIZA** uzito wa dhulma za kihistoria zilizofanywa dhidi ya Waafrika na watu wenye asili ya Afrika kupitia utumwa, uhamishaji, ubaguzi wa rangi na ukoloni;

4. **UNABAINISHA** hali ya makusudi na iliyopangwa ya utumwa wa watu wa Afrika na uhalifu na maauaji ya kimbari dhidi ya wananchi wa kiAfrika, utesaji na mauaji dhidi ya waAfrika, kuwaweka mahabusu kinyume na sheria, na madhila mengine dhidi ya binadamu na ukiukwaji mwingine wa haki na aina nyingine za dhuluma dhidi ya bara la Afrika wakati wa ukoloni;

5. **UNASISITIZA** kwamba madhila dhidi ya Waafrika na mauaji ya kimbari na uhalifu mwingine uliofanywa kwa bara la Afrika wakati wa ukoloni hayakutokea kwa bahati mbaya, lakini yalitokea kwa makusudi na kwa kupangwa;

6. **UNACHUKULIA** utumwa, uhamishaji na ukoloni kama vitendo visivyo na uhalali wowote wa kisheria na mashambulizi makubwa dhidi ya utu wa binadamu;

7. **UNAZINGATIA** kwamba tofauti iliyopo kati ya kiwango cha maendeleo ya Afrika na mabara mengine inaweza kuhusishwa kwa kiasi kikubwa na utumwa na ukoloni, ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa jamii za Kiafrika na kuathiri maendeleo yao;

8. **UNASISITIZA TENA** kiu ya haki ya watu wa Afrika, diaspora na watu wenye asili ya Afrika na matarajio yao makubwa ya fidia na kurejesha mali za kitamaduni za kitaifa zilizoporwa za kiafrika;

9. **UNASISITIZA** haja ya kulinda ubinadamu na vizazi vijavyo dhidi ya hatari ya kuzuka upya kwa utumwa na ukoloni na kuweka alama zinazofaa kuhusu ukatili na uhalifu wao ili kuepuka kujirudia;

10. **UNAIOMBA** AUCIL, kwa kushirikiana na wadau husika kufanya utafiti kuhusu matokeo ya kuuchukulia ukoloni kuwa uhalifu dhidi ya binadamu pia madhila mengine yaliyofanywa wakati wa utumwa, uhamishwaji, na ukoloni kama mauaji ya kimbari dhidi ya waafrika, na kuwasilisha ripoti hii kwenye Mkutano mkuu februari 2026;

11. **UNAZINGATIA** kwamba kuuchukulia huko ni hatua muhimu na ya lazima katika harakati za kudai fidia;

12. **UNATOA WITO** KWA Nchi Wanachama, taasisi za kikanda na asasi za kiraia za Afrika na waafrika wanaoishi nje ya nchi kufanya kazi kupitia mipango mbalimbali ili kuboresha uelewa miongoni mwa kizazi kipya kuhusu uhalifu na kuficha kwa makusudi matukio ya historia ya utumwa na ukoloni.

13. **UNAIPONGEZA** Jamhuri ya Togo kwa pendekezo lake kuhusu kuuchukulia utumwa, uhamishaji na ukoloni kama uhalifu dhidi ya ubinadamu na mauaji ya kimbari na **UNAITAKA** ifuatilie utekelezaji na athari za Uamuzi wa pendekezo, kwa kushirikiana na Kamisheni, Jamhuri ya Ghana na Afrika Kusini na Algeria pamoja na Nchi Wanachama wa AU, taasisi za diaspora, watu wenye asili ya Afrika na mashirika ya kimataifa

14. **UNAAMUA** kuendelea kushughulikia suala hili.

# RASIMU YA UAMUZI KUHUSU TAREHE NA MAHALI PA MKUTANO WA KAWAIDA WA THELATHINI NA TISA (39) WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA UMOJA WA AFRIKA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAAMUA** kwamba tarehe za Mkutano wa Kawaida wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali, ambao utafanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia, utakuwa kama ifuatvyo:

   **i)** Mkutano wa Kawida wa Hamsini na Moja (51) wa Kamati ya Wawakilishi wa Kudumu (PRC), kuanzia tarehe 12 hadi 30 Janurai 2026;

   **ii)** Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Nane (48) wa Baraza Kuu, tarehe 18 na 19 Februari 2026;

   **iii)** Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Tisa (39) wa Wakuu wa Nchi na Serikali, terehe 21 na 22 Februari 2026.

2. **UNAIOMBA** Kamisheni kuchukua hatua zote muhimu kwa ajili ya kuandaa kwa mafanikio Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Tisa (39) wa Wakuu wa Nchi na Serikali na mikutano ya maandalizi ya Baraza Kuu na PRC kulingana na tarehe zilizotajwa hapo juu.

## UAMUZI KUHUSU TAREHE NA MAHALI PA MKUTANO WA SABA 7) WA URATIBU WA NUSU MWAKA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAREJELEA** Maamuzi Assembly/AU/Dec.635 (XXVIII) na Assembly/AU/Dec.687 (XXX) yaliyopitishwa Januari 2017 na Januari 2018 mtawalia, kuhusu Mkutano wa Uratibu wa Nusu Mwaka;

2. **UNAAMUA** kwamba tarehe za Mkutano wa 7 wa Uratibu wa Nusu Mwaka na mikutano ya Baraza Kuu na PRC inayotangulia, zitakuwa kama ifuatavyo:

   i) Mkutano wa Kawaida wa Hamsini (50) wa PRC kuanzia tarehe 9 Juni hadi 20 Juni 2025 mjini Addis Ababa, Ethiopia;

   ii) Mkutano wa Kawaida wa Arobaini na Saba (47) wa Baraza Kuu kuanzia tarehe 10 na 11 Julai, Malabo, Equatorial Guinea

   iii) Mkutano wa Saba (7) wa Uratibu wa Nusu Mwaka wa Umoja wa Afrika na RECs tarehe 13 Julai 2025, Malabo, Equatorial Guinea;

3. **UNAIOMBA** Kamisheni kuweka hatua zote muhimu ili kuandaa Mkutano wa Saba (7) wa Uratibu wa Nusu Mwaka pamoja na mikutano ya maandalizi ya Baraza Kuu na PRC kulingana na tarehe zilizotajwa hapo juu.

## UAMUZI KUHUSU KUWA MWENYEJI WA MKUTANO WA 4 WA UBIA WA AFRIKA-UTURUKI

**Mkutano Mkuu**,

1. **UNAKARIBISHA** Taarifa ya Pamoja na Ripoti ya Pamoja ya Utekelezaji wa Mkutano wa Tatu (wa Tatu) wa Mapitio ya Mawaziri wa Afrika-Uturuki.

2. **UNAIDHINISHA** pendekezo lililotolewa na Nchi ya Libya kuandaa Mkutano wa Nne (wa Nne) wa Ubia wa Afrika na Uturuki utakaofanyika mwaka 2026.

3. **UNAIOMBA** PRC kwa ushirikiano wa karibu na Kamisheni na nchi mwenyeji kukubaliana juu ya tarehe za Mkutano wa Nne (4) wa Ubia wa Afrika na Uturuki na kuanza michakato ya maandalizi ya kufanyika kwa Mkutano huo kwa mafanikio.

## RASIMU YA UAMUZI
## KUHUSU KIWANGO CHA TATHMINI NA MICHANGO

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAZINGATIA** Uamuzi wa Mkutano wa 46 wa Kawaida wa Baraza Kuu kuhusu ripoti ya Kikao cha Pamoja cha Kamati ya Mawaziri kuhusu kiwango cha tathmini na michango na Kamati ya Mawaziri Kumi na Watano wa Fedha (F15).

   a. **Kuhusu Nchi Wanachama zinazokabiliwa na majanga yasiyotarajiwa yanayozifanya zishindwe kulipa michango yao iliyotathminiwa.**

2. **UNAREJELEA** Uamuzi wa Ext/Assembly/AU/Dec.3(XI) uliopitishwa mnamo Novemba 2018 ambapo Mkutano Mkuu uliamua kwamba unaweza kuzingatia maombi kutoka kwa Nchi Wanachama zinazokabiliwa na majanga yasiyotarajiwa yanayozifanya zishindwe kwa muda mfupi kulipa michango yao iliyotathminiwa. Nchi Wanachama kama hizo zitataarifu Mkutano Mkuu kwa maandishi na Mkutano Mkuu unaweza kuzingatia maombi hayo na kuchukua uamuzi.

3. **PIA UNAREJELEA** Uamuzi EX.CL/Dec.1071(XXXV) wa Julai 2019 ambao ulizingatia hali ya usalama na ya kisiasa ya Somalia, ulizuia kuweka vikwazo vya kutolipa michango, na kuiomba Kamisheni kushauriana na nchi kukubaliana juu ya mpango wa malipo wa kufuta malimbikizo ndani ya miaka minne (4) tangu kupitishwa kwa Uamuzi huo.

4. **UNAREJELEA ZAIDI** Uamuzi Assembly/AU/Dec.752(XXXIII) wa Februari 2020 ambao ulizingatia ombi la Jamhuri ya Burundi na changamoto ambazo nchi ilikabiliana nazo katika kukidhi michango yake ya kila mwaka kwa Umoja wa Afrika, pamoja na ombi kwa Kamisheni kushirikiana na Nchi Wanachama zinazokabiliwa na matatizo ya kulipa michango yao kwa Umoja wa Afrika na zile zenye malimbikizo kwa muda wa miaka miwili au zaidi (2) ili kukubaliana juu ya mpango wa malipo wa kufuta malimbikizo yao.

5. **UNAREJELEA** Uamuzi Assembly/AU/Dec.802(XXXIV) wa Februari 2021 ambao uliidhinisha mipango ya malipo ya Jamhuri ya Somalia na Jamhuri ya Burundi ili kufuta malimbikizo yao.

6. **UNAZINGATIA** kuwa 2024 ulikuwa mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa mipango ya malipo iliyokubaliwa na Jamhuri ya Shirikisho la Somalia na Jamhuri ya Burundi na **UNAIDHINISHA**:

   i. Mpango wa malipo unaopendekezwa uliorekebishwa wa Jamhuri ya Shirikisho la Somalia wa kulipa malimbikizo yake ya jumla ya dola za Marekani 1,722,316.95 iliyorekodiwa kufikia tarehe 1 Januari 2025, katika kipindi cha miaka mitano pamoja na michango yake ya kila mwaka iliyotathminiwa kuanzia 2025 hadi 2029.

ii. Ombi la Jamhuri ya Burundi la nyongeza ya miezi sita (6) kwenye mpango wake wa malipo hadi tarehe 30 Juni 2025 ili kulipa malimbikizo yake ya jumla ya dola za Marekani 1,306,050.97.

**b. Kuhusu uandaaji wa kiwango kipya cha tathmini**

7. **UNAZINGATIA ZAIDI** kuwa 2026 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa kiwango cha sasa cha tathmini kwa michango ya Nchi Wanachama (2024-2026) na UNAIAGIZA Kamisheni kuanza mchakato wa kuandaa kiwango kipya cha tathmini kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu mwezi Februari 2026, kwa kufuata mchakato sahihi.

## UAMUZI KUHUSU RASIMU YA SHERIA ILIYOFANYIWA MABORESHO YA TAASISI YA FEDHA YA AFRIKA (AMI)

**Mkutano mkuu**,

**1. UNAZINGATIA** uidhinishaji wa rasimu ya sharia ya AMI na Baraza la 5 Maalumu la STC kuhusu Fedha, Masuala ya Fedha, Mipango ya Kiuchumi na Utangamano na **UNAPENDEKEZA** uwasilishaji wa rasimu hiyo kwa STC ijayo kuhusu Haki na Masuala ya Kisheria kabla ya kupitishwa na Mkutano wa Kuratibu wa Mwaka wa Kati Julai 2025;

**2. UNAAGIZA** kwamba AMI ianze kufanya kazi hadi ifikapo Septemba 2025.

# UAMUZI KUHUSU USHIRIKI WA UMOJA WA AFRIKA KATIKA KUTOA MAONI KATIKA SHAURI LA MAHAKAMA YA KIMATAIFA KUHUSU PALESTINA

**Mkutano Mkuu**,

**1. UNAREJELEA** uungaji mkono thabiti wa AU kwa haki ya watu wa Palestina ya kujitawala na kuanzishwa kwa Taifa huru la Palestina, na Jerusalem Mashariki kama mji wake mkuu, kwa mujibu wa sheria za kimataifa na maazimio husika ya Umoja wa Mataifa;

**2. UNAZINGATIA** ombi la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa la kupata maoni ya ushauri kutoka kwa Mahakama ya Kimataifa (ICJ) kuhusu wajibu wa Israel kuhusu uwepo na shughuli za Umoja wa Mataifa, mashirika mengine ya kimataifa, na Mataifa mengoine katika eneo la Palestina linalokaliwa kwa mabavu, ikiwa ni pamoja na Jerusalem Mashariki;

**3. UNATAMBUA** ushiriki wa AU katika mchakato wa maoni ya ushauri, ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa yake iliyoandikwa Julai 2024 na taarifa ya mdomo yenye matokeo iliyowasilishwa mbele ya ICJ tarehe 26 Februari 2024, ambayo ilithibitisha dhamira ya Umoja wa Afrika kwa sheria za kimataifa na haki kwa watu wa Palestina;

**4. UNATAMBUA PIA** Azimio ACHPR/Res.611 (LXXXI) 2024 la Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu wakati wa Mkutano wake wa 81 wa Kawaida, ambao ulilaani ukiukwaji unaoendelea wa sheria za kimataifa katika maeneo ya Palestina inayokaliwa kwa mabavu, na Bunge la Afrika lilipitisha Azimio la Nne la Bunge la 24 Novemba 24. Mkutano huo ulidhihirisha mshikamano mkubwa na wananchi wa Palestina na kutaka kuchukuliwa hatua za dharura za kuendeleza haki na amani;

**5. UNAAMUA** kama ifuatavyo:

(i) Kuipongeza Kamisheni kupitia Ofisi ya Wanasheria (OLC) kwa kuuwakilisha Umoja wa Afrika katika mashauri ya ICJ kuhusu Matokeo ya Kisheria yatokanayo na Sera na Vitendo vya Israel katika eneo la Palestina linalokaliwa kwa mabavu, ikiwa ni pamoja na Jerusalem Mashariki, ambayo ilieleza msimamo wa kanuni na wajibu kuhusu haki za kisheria na wajibu wa Israel;

(ii) Kuiagiza Kamisheni, kupitia OLC, kuendelea kujihusisha kikamilifu katika maoni ya ushauri ya ICJ kuhusu Palestina, ikijumuisha “majukumu ya Israeli kuhusiana na uwepo na shughuli za Umoja wa Mataifa, mashirika mengine ya kimataifa na Mataifa mengine” ndani na kuhusiana na Eneo la Palestina linalokaliwa kwa mabavu;

(iii) Kuzihimiza Nchi Wanachama kutoa ushirikiano wao kamili na msaada kwa OLC kwa kuchangia data inayofaa, utaalamu, na msaada ili kuimarisha msimamo na uhamasishaji wa Umoja wa Afrika katika mashauri ya ICJ.

# UAMUZI KUHUSU KUTEULIWA KWA MHE. MOHAMED OULD CHEIKH EL GHAZOUANI, RAIS WA JAMHURI YA KIISLAMU YA MAURITANIA KAMA KINARA WA SAYANSI NA UBUNIFU

**Mkutano Mkuu**,

**1. UNATAMBUA** kuandaliwa kwa mafanikio kwa Kongamano la Elimu ya Bara chini ya mada, "Elimisha na Afrika yenye Stadi kwa Karne ya 21" na Serikali ya Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, kuanzia tarehe 9 hadi 11 Desemba 2024, mjini Nouakchott, Mauritania;

**2. UNAMPONGEZA** Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, Mhe. Mohamed Ould Cheikh El Ghazouani, kwa uongozi wake wenye maono na kujitolea katika kutumia nguvu ya elimu, sayansi, teknolojia na uvumbuzi kuelekea Afrika inayojiendesha kiteknolojia na kisayansi, na **UNAAMUA** kumteua kuwa Kinara wa Sayansi na Ubunifu.

# AZIMIO
# KUHUSU KUHARAKISHA UPATIKANAJI WA TEKNOLOJIA ZA NISHATI SAFI YA KUPIKIA BARANI AFRIKA (*Suala lilopendekezwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*)
## Doc. Assembly/AU/19(XXXVIII)

**SISI,** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tuliokutana tarehe 15 na 16 Februari 2025 katika Mkutano wetu wa Kawaida wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mjini Addis Ababa, Ethiopia;

***TUKIZINGATIA*** pendekezo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (URT) kuhusu dhamira yake ya kuendeleza Mpango wa Nishati Safi ya Kupikia, na kutambua haja ya haraka ya kuharakisha upatikanaji wa nishati na teknlojia za kupikia zilizo safi, nafuu na za uhakika kote barani Afrika;

***TUKITAMBUA*** kwamba kutegemea nishati ya asili ya kupikia kunaleta changamoto kubwa za kiafya, kimazingira, na kiuchumi, hasa kwa wanawake na watoto, na kwamba hatua ya haraka inahitajika ili kukuza teknolojia za nishati safi ya kupikia;

***TUKIREJELEA*** azimio la pamoja la Nchi Wanachama la kubadilika kuelekea katika teknolojia za kupikia endelevu, za kisasa, na zenye ufanisi kulingana na Ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), hususan SDG ya 7 kuhusu nishati nafuu na safi;

***TUKITAMBUA*** kwa kuthamini uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutoa kipaumbele kwenye suala la nishati safi ya kupikia kama kipengele muhimu cha upatikanaji wa nishati na ustahimilivu wa tabianchi barani Afrika, na juhudi za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan za kukusanya rasilimali za kitaifa na kikanda na kuhamasisha ubia ili kuongeza teknolojia za nishati safi ya kupikia katika bara zima;

***TUNATHIBITISHA*** haja ya kuongezeka kwa ufadhili, msaada wa sera, na ushirikiano wa sekta mbalimbali ili kufikia upatikanaji kwa wote wa suluhu za nishati safi ya kupikia katika bara zima;

**TUNAAZIMIA YAFUATAYO:**

1. ***KUZIHIMIZA*** sekta binafsi na taasisi za serikali, kuongeza uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za nishati safi ya kupikia na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya nishati safi ya kupikia vijijini na mijini.

2. ***KUZIHIMIZA*** Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kushirikisha wadau wa kitaifa na kimataifa katika kupata ufadhili kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya

Suluhu za Nishati safi ya Kupikia a Wanbawake wa Afrika (AWCCSP) na Programu ya Nishati Safi ya kupikia ya Afrika (ACCP).

3. ***KUSISITIZA*** kuwa ngazi zote za kitaifa na bara, mazingira ya AWCCSP na ACCP lazima yaendane na malengo ya programu hizi.

4. ***KUIMARISHA*** utafiti, mafunzo na uvumbuzi kwa kuzingatia asili ya teknolojia za nishati safi ya kupikia ili Afrika iweze kupata nishati na teknolojia safi, nafuu na za kuaminika za nishati ya kupikia.

5. ***KUIOMBA*** Kamisheni ya Umoja wa Afrika kupitia Idara ya Miundombinu na Nishati kuunda mifumo ya kufuatilia upitishaji na athari za suluhu za nishati safi ya kupikia katika ngazi ya kitaifa na kikanda kwa ajili ya kushirikiana na nchi wanachama ili kuhakikisha mbinu sanifu katika kupima maendeleo kuelekea kufikia malengo yaliyowekwa kuhusu nishati safi ya kupikia.

6. ***KUMUOMBA*** Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendeleza utetezi wake kuhusu nbishati safi ya kupikia katika bara la Afrika, kwa kuhakikisha ushiriki endelevu wa kisiasa wa ngazi ya juu, uratibu na ubia, kama kipengele muhimu cha upatikanaji wa nishati, mabadiliko ya haki ya nishati yanayozingatia jinsia katika juhudi za kukabiliana na tabianchi barani Afrika, afya ya binadamu na ustahimilivu kwa tabianchi.

7. ***KUTANGAZA*** upatikanaji wa nishtai safi ya kupikia kama kipaumbele cha kwanza kwa Afrika, kwa kutambua umuhimu wake kwa afya, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, uhakika wa nishati na mabadiliko ya kiuchumi na **TUNAZIOMBA** Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kuchukua hatua madhubuti za kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia katika sera zao husika za kitaifa.

# AZIMIO
# LA MSHIKAMANO WA UMOJA WA AFRIKA NA HAITI NA KUUNGA MKONO KUHAMISHIA MAMLAKA YA MISHENI YA MSAADA WA USALAMA WA KIMATAIFA (MSSM) YA UMOJA WA MATAIFA KWA OPERESHENI ZA AMANI ZA UMOJA WA MATAIFA – Doc. Assembly/AU/20 (XXXVIII)

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tuliokutana tarehe 16 Februari, 2025 katika Kikao chetu cha Kawaida cha 38 kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia;

**TUKIREJELEA** Mkataba wa Umoja wa Afrika unaosisitiza umuhimu wa amani, demokrasia, na usalama katika kutengeneza mazingira bora ya maendeleo na hadhi;

**PIA, TUKIREJELEA** uamuzi namba Assembly/AU/Dec.884 (XXXVII) wa Februari, 2024, ambao ulioelezea historia ya kina ya AU na zile za mtangulizi wake, OUA, ikijumuisha uhusiano wa kihistoria, kiutamaduni na kindugu unaoziunganisha nchi za Afrika na diaspora wa Afrika, na kumteua Mhe. Nana Addo Dankwa Akufo-Addo, Rais wa Jamhuri ya Ghana, kama Kiongozi wa AU katika kuharakisha Haki na Malipo ya Fidia kwa Waafrika, kwa lengo la kuimarisha utetezi wa msimamo wa pamoja kuhusu fidia barani Afrika, na kuunda umoja wa Afrika na Diaspora katika ngazi ya kimataifa.

**TUNATAMBUA** moja ya malengo manne ya msingi ya Mageuzi ya kitaasisi ya Umoja wa Afrika, kama ilivyoelezwa katika Uamuzi Assembly/AU/Dec.635 (XXVII), unaoakisi lengo la saba la Ajenda ya 2063 inayolenga "Afrika inayoshiriki kama mtendaji na mshirika madhubuti, imara, na mwenye ushawishi katika jukwaa la kimataifa."

**Tunatambua** Azimio Assembly/AU/Decl.2(XXXII) la Februari, 2019 ambalo lilisisitiza kujitolea kwa umoja wa watu wa Afrika, kujenga Afrika yenye utangamano, na kuimarisha uhusiano wa kiutamaduni, kisiasa, kijamii, na kiuchumi ambao unakuza ndoto ya muungano wa Afrika miongoni kwa watu wote wa asili ya Afrika.

**Tunarejelea** ahadi ya mshikamano inayotokana na historia ya pamoja, urithi, ubinadamu, na utamaduni ambao uliongoza uzinduzi wa Kikao cha Afrika-CARICOM mwezi Septemba 2020, kusisitiza jukumu la Afrika kwa kanda yake ya 6 na matarajio yake ya kuimarisha ushirikiano katika harakati za kufikia hatima ya pamoja.

**TUNASIKITISHWA SANA** na hali ya kisiasa isiyokuwa ya utulivu inayoendelea, vurugu za vikundi vya kihalifu, unyanyasaji wa kingono na kijinsia, na matatizo ya kibinadamu nchini Haiti, ambapo mambo yote kwa pamoja yanatishia usalama na hadhi ya watu wa Haiti, kuzuia urejeshaji wa utawala wa kidemokrasia, na kuzuia upatikanaji wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya muda mrefu, na kuhatarisha utulivu katika bara.

**TUNATAMBUA** kupitishwa kwa kauli moja kwa Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) 2699(2023) linaloruhusu Misheni ya Msaada wa Usalama ya Kimataifa (MSS) kwa Haiti na pia Azimio namba 2751 (2024), ambalo lilihuisha mamlaka haya kwa muda wa miezi 12 zaidi, kwa maombi ya Serikali ya Haiti;

**TUNAKARIBISHA** mchango wa nchi mbalimbali katika kusaidia MSSM na kwa kipekee kuisaidia Kenya kama taifa linaloongoza Misheni ya Msaada wa Usalama ya Kimataifa; na katika kuchukua hatua kwa niaba ya Afrika kuisaidia Haiti; na pia kutambua mafanikio yaliyopatikana tangu kupelekwa kwa MSS nchini Haiti;

**TUNATAMBUA** kwamba Serikali ya Haiti, kupitia Baraza lake la Mpito la Rais, limeomba mabadiliko ya Misheni ya MSS kuwa Operesheni ya Ulinzi wa Amani ya Umoja wa Mataifa (PKO) katika wasilisho la tarehe 22 Oktoba, 2024 (nyaraka za UNSC S/2024-765), ili kuchangia katika utulivu wa nchi na ujenzi wa taasisi zake za kidemokrasia;

**TUNASISITIZA** umuhimu wa msaada wa kimataifa endelevu na ulioboreshwa ili kuwezesha MSS kutimiza majukumu yake, na kusimamia mchakato wa mabadiliko unaoendelea nchini Haiti;

**TUNATAMBUA** msaada wa umma ulioonyeshwa na baadhi ya wanachama wa UNSC na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kama vile Chad, Benin, Burundi, Senegal na Algeria na wachangiaji wa misheni ya MSS, ikiwamo Kenya, kwa kuanzisha mchakato wa tafakuri na uchambuzi kulingana na ripoti na mapendekezo kuhusiana na utendaji wa misheni ya MSS, kama ilivyowekwa katika Azimio la UNSC namba 2699 (2023) na 2751 (2024), ili kuzingatia mabadiliko ya misheni ya MSS kuwa UNPKO, pamoja na umuhimu wa kuendeleza ushirikiano wa kidiplomasia na wanachama wengine wa UNSC na washirika wanaohusika ili kurahisisha mabadiliko yaliyoombwa na Haiti;

**TUNASISITIZA** kwamba jukumu kuu la kudumisha amani na usalama wa kimataifa linabaki kwa UNSC, kwa mujibu wa Mkataba, na kwamba operesheni za amani ni mojawapo ya nyenzo muhimu zinazopatikana kwa Umoja wa Mataifa kutekeleza jukumu hili;

**TUNATAMBUA** umuhimu wa kuhakikisha kwamba operesheni za ulinzi wa amani nchini Haiti zinaheshimu haki za binadamu, sheria za kimataifa, na uhuru wa kitaifa, kulingana na idhini kamili na wazi ya mamlaka za Haiti na dhamira ya watu wake, huku zikitoa msaada ulioombwa na serikali ya mpito ya Haiti wa kusaidia kurejesha utulivu na utawala wa umma, kwa kuzingatia heshima kwa misingi ya uhuru wa kitaifa, uadilifu, na uhuru wa kisiasa wa Nchi, pamoja na kanuni ya kutokuingiliwa katika masuala ambayo ni kwa msingi wa mamlaka ya ndani ya Nchi; na

**TUNATHIBITISHA** kwamba, pamoja na operesheni za ulinzi wa amani, kuna haja ya kushughulikia vyanzo vya msingi vya mizozo, na kwamba vyanzo hivi vinapaswa kushughulikiwa kwa pamoja, kupangiliwa, kuratibiwa vizuri, na kwa namna jumuishi kwa kutumia nyenzo za kisiasa, kijamii, na kimaendeleo.

**TUMEAZIMIA:**

1. ***Kuonesha*** mshikamano madhubuti na wananchi wa Haiti wakati huu mgumu na kuunga mkono wito wa Baraza la Rais la Mpito la kupata msaada wa kimataifa ili kurejesha usalama, kuwezesha mabadiliko yake ya kisiasa, na kuifanya Haiti kuwa katika hali ya usalama endelevu, utawala wa sheria, na utawala wa kidemokrasia. Kwa muktadha huu, tunapitisha maombi ya Baraza la Rais la Mpito ya kuhamasisha misheni ya MSS kuwa Operesheni za Kulinda Amani za Umoja wa Mataifa kama njia ya kupata rasilimali za uhakika za kuwezesha kufanikisha lengo hili.

2. ***Kulishukuru*** Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) kwa kuendelea kushughulikia suala la Haiti; na kutambua umuhimu na haja ya dharura ya kuwa na rasilimali zinazotosha na endelevu ili kushughulikia changamoto na ugumu unaoikabili Haiti, na kuendeleza msukumo uliopo, kuhimiza Baraza kutafakari kwa namna chanya maombi ya Haiti ya kuhamishia misheni ya MSS katika Operesheni za Kulinda Amani za Umoja wa Mataifa (UNPKO).

3. ***Kuelekeza*** A3 kuongoza kwa umakini na kuratibu kwa kushirikiana na wanachama wote wa UNSC ili kuharakisha uhamishaji wa Misheni ya MSS kuwa ya UNPKO; pia, kuhimiza wanachama wote wa UNSC kuuunga mkono kikamilifu mabadiliko hayo; na kutoa wito kwa Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa kuunga mkono na kuwezesha kikamilifu mabadiliko ya MSS kuwa UNPKO.

4. **Kutambua** msaada uliotolewa na baadhi ya nchi wanachama wa AU kwa Misheni ya MSS, hasa kujitolea kwa Kenya kama taifa linaloongoza, **kupongeza** ujasiri wa wanajeshi wa MSS ambao msaada wao kwa Polisi wa Taifa la Haiti umesababisha mafanikio makubwa na kuleta msukumo chanya nchini Haiti; na **kuhimiza** nchi nyingine wanachama wa AU kuzingatia kuungana katika juhudi za kuhakikisha kupelekwa kikamilifu kwa MSS nchini Haiti, kwa mujibu wa Azimio la UNSC 2751 (2024), na kuendelea kuratibu michango ya hali na vifaa kupitia mifumo iliyopo, ikiwa ni pamoja na Mfuko wa Umoja wa Mataifa na Kikundi cha Uratibu wa Usalama wa Kimataifa.

5. **Kutambua** michango iliyotolewa na washirika wa kikanda na kimataifa kwa Misheni ya MSS, na kusisitiza umuhimu wa kuunga mkono jitihada za Polisi wa Haiti kurejesha sheria na kurejea kwa njia ya usalama utawala wa kidemokrasia nchini humo; kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuonyesha uungaji mkono na mshikamano wao kwa watu wa Haiti na nchi yao.

6. **Kuiomba** Kenya, kama taifa linaloongoza MSS, kutoa taarifa kwa Umoja wa Afrika kupitia Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kuhusu maendeleo ya misheni; na kupendekeza kwa Kamisheniya Umoja wa Afrika kuwezesha Misheni ya Mshikamano wa Afrika kuelekea Haiti.

7. **Kuisisitiza** Umoja wa Afrika kujizatiti kusaidia Haiti katika kipindi hiki, na kuunga mkono ongezeko la rasilimali za ziada na kuweka kipaumbele katika ujenzi wa

kijamii na kiuchumi wa Haiti, kwa kuzingatia kujenga amani, utawala wa kidemokrasia, utulivu wa kisiasa, na maendeleo endelevu.

# AZIMIO JUU YA MKUTANO WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU MBOLEA NA AFYA YA UDONGO AFRIKA

**SISI** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tuliokutana tarehe 16 Februari 2025 kwenye Mkutano wa Kawaida mjini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAPITISHA** Azimio lililoambatishwa la Mkutano kuhusu Mbolea na Afya ya Udongo Afrika uliofanyika tarehe 9 Mei 2024 mjini Nairobi, Kenya.

# AZIMIO LA NAIROBI KUHUSU MKUTANO WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI KUHUSU MBOLEA NA AFYA YA UDONGO AFRIKA, NAIROBI, KENYA | 9 MEI 2024

**Sisi**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika tuliokutana mjini Nairobi, Kenya wakati wa Mkutano Mkuu kuhusu Mbolea na Afya ya Udongo Afrika;

**TUKIREJELEA** Azimio la Abuja la 2006 kuhusu Mbolea kwa ajili ya Mapinduzi ya Kijani ya Afrika lilibainisha haja muhimu ya kuongeza matumizi ya mbolea ili kuchochea ukuaji wa tija ya kilimo kwa lengo la kutokomeza njaa na umaskini barani Afrika;

**TUKIREJELEA ZAIDI** Azimio la Malabo la Programu ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) lilipitishwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Thelathini na Tatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU mjini Malabo, Equatorial Guinea mwezi Juni 2014. Katika Azimio hilo, Nchi Wanachama waliahidi kuwa na mabadiliko jumuishi ya kilimo. Azimio la Malabo la CAADP pia liliimarisha maamuzi ya awali, ikiwa ni pamoja na Azimio la Maputo la mwaka 2003 kuhusu CAADP; Azimio la Sirte la 2004 kuhusu Changamoto za Kutekeleza Maendeleo Jumuishi na Endelevu katika Kilimo na Maji barani Afrika;

**TUKITAMBUA** changamoto za kudumu na za muda mrefu katika kutekeleza ahadi katika maazimio mbalimbali na kuthamini maendeleo yaliyofikiwa tangu Azimio la Abuja, hususan ongezeko kubwa katika uzalishaji wa ndani wa mbolea za madini hadi kufikia zaidi ya dola bilioni 15 za uwekezaji wa sekta binafsi;

**TUKIWA NA WASIWASI MKUBWA** kuwa tangu kupitishwa kwa Azimio la Abuja mwaka 2006, matumizi ya mbolea barani Afrika yameongezeka tu kutoka wastani wa kg8/hekta hadi takriban kg18/hekta mwaka 2022, kiasi ambacho kiko chini ya nusu ya lengo la kg50/hekta iliyoainishwa kwenye azimio;

**TUKIREJELEA** kuwa kiwango cha wastani cha matumizi ya mbolea duniani ni takriban kg135/hekta na kuwa kiwango cha wastani cha matumizi cha 18kg/hekta ni asilimia 13 tu za kiwango cha dunia;

**TUKITAMBUA** kuwa wakati Bara sasa linazalisha takriban tani milioni 30 za mbolea ya madini kila mwaka, mbolea nyingi zinasafirishwa nje ya bara na Nchi Wanachama nyingi bado zinategemea sana mbolea ya kuagizwa kutoka nje, hususan mbolea ambazo hazina fosfati ambazo zinaiweka Afrika kwenye vishindo vya soko la nje na kubadilika kwa bei;

**TUKITAMBUA ZAIDI** kuwa janga la dunia la mbolea la hivi karibuni limeathiri Afrika kwa namna isiyo sawa, huku kukiwa na kushuka kwa 25% mwaka hadi mwaka katika matumizi ya mbolea mwaka 2022;

**TUKITAMBUA** kuwa kujikita kwenye mbolea pekee hakuwezi kusitisha uharibifu wa ardhi wala kuongeza tija ya udongo wa Afrika na mazao yake ya kilimo;

**TUKIHOFIA** utegemezi unaoendelea kwenye upanuzi wa ardhi ya kilimo ili kuongeza uzaishaji wa kilimo, kasi ndogo inayoendelea ya ongezeko la tija ya kilimo, eneo dogo lililo chini ya usimamizi endelevu wa udongo na matokeo ya kupungua kwa virutubishi vya udongo, mapato madogo ya mkulima, uharibifu mkubwa wa ardhi, uzalishaji wa hewa chafuzi ya Kaboni ($CO_2$), upoteaji mkubwa wa bayoanuwai, na gharama kubwa ya kimazingira. Upungufu huu katika afya ya udongo hupunguza kwa kiasi kikubwa mwitikio wa mazao kwenye matumizi ya pembejeo za kukuza mazao kama vile mbolea za madini na mazao mbalimbali yaliyoboreshwa, na huongeza kwa kiasi kikubwa hatari ya wakulima wadogo na jumuiya kupatwa na athari za tabianchi na vishindo vingine;

**TUKITAMBUA ZAIDI** kuwa mtazamo kuhusu uendelevu wa kilimo umekua kutoka kwenye lengo finyu la kuwa na tija na faida ya mazao hadi kwenye lengo pana kuhusu uendelevu wa kijamii, kimazingira na kiuchumi, kuendana na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, urekebishaji wa ardhi iliyoharibiwa, na urejeshaji na utengenezaji wa huduma za mfumo wa ikolojia, ikiwa ni pamoja na bayoanuwai;

**TUKITHAMINI** kuwa haja ya kuongeza matumizi ya mbolea barani Afrika bado ni suala muhimu, na linapaswa kufanyika kwa namna ambayo itasaidia afya ya udongo na ustahimilivu wa kimazingira. Kilimo cha Afrika pia kinaendelea kukabiliwa na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanatishia mustakabali wa uendelevu wa kilimo katika bara;

**TUKIFIKIRIA** kuwa siku hizi changamoto za uhaba wa chakula, lishe duni, na mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuwepo na zinahitaji hatua ya haraka. Haja ya ushirikiano wa kikanda kuhusu suala la mbolea na afya ya udongo ni kubwa kuliko ilivyokuwa hapo awali kwa vile fursa za uwekezaji na biashara kubwa za baina ya kanda na za ndani ya kanda kwa sasa zinawezeshwa kwa kiasi kikubwa na upitishaji wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA) unaofanywa na Nchi Wanachama wa AU;

**TUKITAMBUA** ukweli kuwa kuongeza matumizi ya mbolea, rasilimali zote za madini na za kikaboni, ni muhimu kwa ajili ya kuongeza tija na urejeshaji wa afya ya udongo. Ufanisi na kufaa kwa mbolea za madini na za kikaboni na pembejeo zingine za ziada vinapaswa kuimarishwa ili kuongeza tija, kuongeza faida na mapato kwenye uwekezaji, kuboresha afya ya udongo, na kuimarisha ustahimilivu kwa mabadiliko ya tabianchi;

**TUKITAMBUA** umuhimu kuwa kujenga afya ya udongo na kuzalisha upya udongo ulioharibiwa ni muhimu kwa ajili ya mabadiliko endelevu ya mifumo ya chakula na ni muhimu kwa ajili ya matumizi fanisi na yanayofaa ya mbolea na kwamba ni mchakato wa muda mrefu. Mifumo ya kusaidia na motisha ni muhimu ili kuwezesha uwekezaji wa wakulima kwenye uboreshaji wa afya ya udongo;

**TUKISISITIZA** kuwa uwekezaji katika uzalishaji wa ndani na uchanganyaji wa mbolea vinapaswa kutumiwa ipasavyo ili kutumia kwa faida rasilimali za bara na kupunguza utegemezi kwenye masoko ya kimataifa. Upatikanaji wa mbolea na gharama vinapasa

kuboreshwa. Vyombo vya ufadhili kama vile dhamana za mikopo, mitaji iliyopo, na ruzuku zinazolengwa vinapaswa kuimarishwa ili kupunguza uharibifu wa masoko, kupunguza gharama na kuimarisha minyororo ya usambazaji wa pembejeo;

**TUKITAMBUA** fursa zinazotolewa na ushirikiano, uratibu, na uoanishaji wa sera na kanuni za mbolea, uwekezaji mkubwa kuongeza uwezo wa nchi na bara wa kuzalisha mbolea, pamoja na kurahisisha biashara ya kuvuka mipaka; utafiti na maendeleo ya kushirikiana, ujenzi wa uwezo pamoja na ujifunzaji baina ya nchi na kubadilishana uzoefu mzuri;

**TUKITAMBUA ZAIDI** asili jumuishi ya sekta ndogo za kilimo (mazao, uvuvi, misitu, na mifugo) na masuala ya afya ya udongo ambayo yanahitaji kutoa kipaumbele kwa uhifadhi na usimamizi jumuishi wa udongo na maji katika bonde la maji, sura ya dunia au chanzo cha maji ili kuboresha afya ya udongo;

**TUKITAMBUA ZAIDI** kuwa mfumo wa uwasilishaji bidhaa kwenda kwa mtumiaji wa mwisho barani Afrika ni dhaifu, huku kukiwa na umbali marefu kwa wakulima kupata mbolea na pembejeo zingine muhimu za kilimo pamoja na huduma za ushauri.

***Hivyo*:**

**Tunaidhinisha** Mpango Kazi wa Mbolea na Afya ya udongo na Mfumo wa Mpango wa Udongo kwa ajili Afrika kama nyaraka muhimu elekezi ili kutumia ubia wa wadau mbalimbali na uwekezaji ili kuongoza sera, fedha, utafiti na maendeleo, masoko, na ujenzi wa uwezo kwa ajili ya mbolea na usimamizi endelevu wa afya ya udongo barani Afrika.

***Kuhusu Mbolea*:**

1. Tunaahidi kuongeza mara tatu uzalishaji wa ndani na usambazaji wa mbolea za kikaboni na zisizo za kikaboni zenye ubora uliothibitishwa ifikapo mwaka 2034 ili kuboresha upatikanaji na gharama nafuu kwa wakulima wadogo kupitia hatua zifuatazo:
    a. Kutoa kipaumbele kwenye uzalishaji wa ndani na uchanganyaji wa mbolea za madini kwa kutumia malighafi zinazopatikana ndani;
    b. Kuimarisha utafiti na maendeleo kwenye matumizi ya mbolea za kikaboni na zisizo za kaboni kwa kufufua Kituo cha Afrika cha Maendeleo ya Mbolea mjini Harare;
    c. Kutoa motisha kwa uzalishaji wa ndani, matumizi na uchakataji upya wa rasilimami za kikaboni;
    d. Kutumia fursa zinazotolewa na uzalishaji wa mbolea unaodhibitiwa na mamlaka mbalimbali, unaotumia kaboni ndogo na wa kimzunguko;
    e. Kuanzishwa kwa biashara ndogo ndogo na za kati (SME) hususan na vijana na wanawake, zinazolenga uzalishaji na usambazaji wa mbolea za kikaboni na zisizo za kaboni;

f. Kutumia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA) kuongeza maradufu biashara ya mbolea ndani ya Afrika ifikapo 2034.

2. Tunaahidi ifikapo 2034 kuwapatia, angalau 70% ya wakulima wadogo katika bara, mapendekezo yaliyolengwa kuhusu kilimo kwa ajili ya mazao mahsusi, udongo, na hali za tabianchi ili kuhakikisha ufanisi mkubwa na matumizi endelevu ya mbolea kupitia hatua zifuatao:
   a. Kuandaa mapendekezo ya ushauri wa mbolea ya muktadha mahsusi na afya ya udongo kutumia uwezo wa data na kufuata kanuni nne za usimamizi sahihi wa virutubishi (*4R Nutrient stewardship)* na Usimamizi Jumuishi wa Rutuba ya Udongo.
   b. Kuandaa na kutumia vifaa vyenye viwango na sahihi kwa ajili ya kutathmini rutuba ya udongo, afya ya udongo, na usimamizi endelevu wa udongo wa muktadha mahsusi na mahitaji ya virutubisho.
   c. Kuanzisha mfumo wa taarifa wa kidijiti kuendesha vyombo vya kusaidia maamuzi ya mbolea, mazao na tabianchi kuhusu usimamizi wa udongo katika ngazi za taifa, kanda na bara.

3. Tunaunga mkono jitihada za Nchi zinazozalisha gesi asilia katika uzalishaji wa mbolea kuongeza uzalishaji wao na kuhakikisha upatikanaji katika bei zisizobadilika badilika.

***Kuhusu Afya ya Udongo:***

4. Tunaahidi kudhibiti uharibifu wa ardhi na kurejesha afya ya udongo kwenye angalau 30% ya ardhi iliyoharibiwa ifikapo 2034 kupitia hatua zifuatazo:
   a. Kutumia mifumo ya kiuvumbuzi ya motisha - ikiwa ni pamoja na kutolea malengo upya programu zilizopo za ruzuku – ili kuhamasisha uwekezaji wa wakulima wadogo katika afya ya udongo;
   b. Kukuza uhifadhi jumuishi wa udongo na maji, mipango, na shughuli za usimamizi katika sekta ndogo za kilimo na sura ya nchi/mabonde ya maji;
   c. Kukuza uwekezaji katika umwagiliaji kama sehemu ya usimamizi jumuishi wa udongo na rasilimali maji kwa ajili ya kuwezesha ufanisi wa matumizi ya virutubisho na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi;
   d. Kuimarisha utafiti wa kiushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa na mifumo ya ugani ili kupambana na changamoto za afya ya udongo na kuboresha ubora wa msaada kwa wakulima wadogo;
   e. Kukuza mazoea ya kilimo cha kikaboni ili kuboresha afya ya udongo pamoja na kilimo cha kawaida.

***Kuhusu Ufadhili**:*

5. Tunaahidi kuendesha kikamilifu Mfumo wa Ufadhili wa Mbolea Afrika (AFFM) ili kuboresha uzalishaji, manunuzi, na usambazaji wa mbolea za kikaboni na zisizo za kaboni, na afua za afya ya udongo kupitia hatua zifuatazo:
   a. Kutanua wigo wa Mfumo huo ili kusaidia utekelezaji wa azimio hili kwa

lengo mahsusi la kuondoa hatari ya uwekezaji wa wakulima katika teknolojia za kukuza mazao na afya ya udongo ya mazao ya uhakika wa chakula ya sasa na yaliyolengwa, kufadhili miundombinu na utaratibu wa ugavi na usafirishaji ili kuboresha upatikanani wa mbolea za kikaboni na zisizo za kaboni, upatikanaji wa masoko ya chakula kwa wakulima na; kuunga mkono mageuzi ya sera ya mbolea na afya ya udongo;

b. Kuunda mfuko wa afya ya udongo unaotokana na vyanzo mbalimbali, kwa ajili ya utafiti, uvumbuzi, ujenzi wa uwezo, na biashara changa kuhusu matumizi ya mbolea na hatua za afya ya udongo. Mfuko utakuwa sehemu ya Mfumo uliopo tayari wa Ufadhili wa Mbolea Afrika (AFFM), ambao unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB);

c. Kuweka umakini kwa Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo za Afrika (SIDS), ambazo zinakumbwa na changamoto kwa sababu ya hali tete ya mifumo ya ikolojia ikiwa ni pamoja na kupata mbolea na gharama ambazo zinafaa kwa Nchi Zinazoendelea za Visiwa Vidogo.

6. Tunaomba Kamisheni ya AU kukusanya rasilimali za fedha na za kitaalamu kutekeleza ahadi hizi kwa kushirikiana kwa karibu na mifuko mbalimbali iliyopo kuhusu tabianchi

***Kuhusu Kuandaa Mazingira Wezeshi***

7. Tunaahidi kuandaa na kutekeleza sera na kanuni ili kuunda mazingira rafiki kwa ajili ya afua za mbolea na afya ya udongo kupitia hatua zifuatazo:

a. Kuandaa miongozo ya kibara, inayozingatia muktadha mahsusi kwa ajili ya uandaaji na utekelezaji wa sera muhimu na zinazofaa za mbolea na afya ya udongo;

b. Kuoanisha sera za kitaifa na kikanda na mifumo ya kiudhibiti ili kuhakikisha kuna upatanifu na kukuza biashara ya kanda na bara;

c. Kuwezesha ushirkiano na mazungumzo na sekta binafsi katika ngazi zote ;

d. Kuimarisha ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi kuimarisha uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa mbolea.

***Kuhusu kujenga Uwezo ili kusaidia Utekelezaji***

8. Tunaahidi kuandaa na kukuza ujenzi wa uwezo wa kimfumo wa kitaifa kwa ajili ya shughuli na teknolojia muhimu za ndani za usimamizi wa mbolea na afya ya udongo kupitia hatua zifuatazo:

a. Kuanzisha mitandao ya kikanda ya utafiti na maendeleo kwa ajili ya kubadilishana maarifa na teknolojia;

b. Kujenga, Kuimarisha na kusanifisha uwezo wa uchanganuzi wa mbolea na huduma za maabara kwa mujibu wa viwango vya ubora wa mbolea kwa kushirikiana na wadau wote muhimu ikiwa ni pamoja na Taasisi za Kitaalamu za Kilimo;

c. Kukiwezesha Kituo cha Afrika cha Maendeleo ya Mbolea ambacho kilianzishwa mjini Harare na Umoja wa Afrika.

9. Tunaahidi kukuza umoja wa Afrika kwa kubadilishana maarifa, mafunzo, maendeleo, na programu za kuhama kwa ajili ya mazoea bora katika rutuba ya udongo na afya ya udongo;

10. Tunaahidi zaidi kuhakikisha kuwa angalau 70% ya wakulima wadogo wanapata huduma bora za ugani na ushauri kuhusu mbolea na afya ya udongo kutoka kwenye mifumo yote ya ugani ya umma na binafsi kupitia hatua zifuatazo:
    a. Kupitia na kuboresha elimu ya msingi na programu za mafunzo ya juu kwa ajili ya sayansi ya udongo na sayansi ya uchumi wa kilimo ili kujumuisha watu ambao ni muhimu kwenye usimamizi endelevu wa udongo;
    b. Kujenga, Kuimarisha, na kuboresha huduma za uchanganuzi wa udongo ili kuhakikisha zinapatikana na ni nafuu kwa wakulima wadogo;
    c. Kuimarisha mifumo ya uwasilishaji bidhaa kwa mtumiaji wa mwisho kwa kuwasaidia wafanyabiashara wa kilimo na SMEs

***Kuhusu kutumika ndani ya nchi***

11. Tunaahidi kuingiza mapendekezo yaliyo katika Azimio hili kwenye Mipango ya Uwekezaji wa Kilimo ya Kitaifa kwa ajili ya uwekezaji ;
12. Tunatoa wito kwa Mawaziri wa Fedha kukusanya na kutenga rasilimali za kiutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyo kwenye Azimio hili.

***Wito wa Kuchukua Hatua***

***Tunaomba:***

13. AUC na AUDA-NEPAD kusaidia Nchi Wanachama kuingiza kwenye mipango ya ndani mifumo mizuri kwa ajili ya kuwapongeza wakulima wadogo kwa hatua za zilizoboreshwa za afya ya udongo, ikiwa ni pamoja na masoko ya kaboni;

14. AUC na AUDA-NEPAD kuandaa mfumo wa kimfumo wa uangalizi wa afya ya udongo unaoendana na mifumo iliyopo ya ufuatiliaji na tathmini ya CAADP, ili kufuatilia maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuandaa vipimo vya bara kwa ajili ya kupima afya ya udongo;

15. AUC na AUDA-NEPAD kuandaa mpango wa utekelezaji baada ya mkutano mkuu kwa ajili ya Mpango Kazi wa Mbolea na Afya ya Udongo na kwa kuendana na Mpango wa Udongo kwa ajili ya Afrika, na kutoa ripoti kwa Kamati Maalumu ya Kiufundi (STC) inayohusika na Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Maji na Mazingira mnamo mwezi Novemba 2025;

16. AUC na AUDA-NEPAD kuunda ubia na mikutano ya kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa azimio hili na kutoa ripoti kwa Mkutano wa KAwaida wa WAkuu wa Nchi na Serikali mwezi Februari 2026 ;.

17. AUC na AUDA-NEPAD kusaidia na kufufua Kituo cha Afrika cha Maendeleo ya Mbolea kama taasisi ya kusaidia utafiti na maendeleo ya mbolea barani Afrika na kuzingatia uwezekano wa kuanzisha vituo vya kikanda kwa ajili ya maendeleo ya mbolea na afya ya udongo ;

**Tunazihimiza**:

18. Nchi Wanachama Kuanzisha na kuimarisha Utafiti wa Mbolea wa kitaifa na Vituo vya Maendeleo ;

***Tunatoa wito kwa**:*

19. Sekta binafsi kuongeza uwekezaji katika sekta ya mbolea ya Afrika na kukuza hatua za usimamizi endelevu wa udongo;
20. Taasisi za Fedha za Bara na za Kimataifa kusaidia uwekezaji wa sekta binafsi na sekta ya umma kwenye sekta ya mbolea ya Afrika;
21. Wabia wa maendeleo kusaidia Kamisheni, AUDA-NEPAD, Jumuiya za kiuchumi za Kikanda na Nchi Wanachama katika utekelezaji wa Azimio hili.

Limeandaliwa mjini Nairobi, Kenya, tarehe 9 Mei 2024

# AZIMIO KUHUSU AZIMIO LA KAMPALA LA CAADP KUHUSU KUJENGA MIFUMO STAHIMILIVU NA ENDELEVU YA CHAKULA CHA KILIMO BARANI AFRIKA

**SISI,** Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tuliokutana tarehe 16 Februari, 2025 katika Mkutano wetu wa Kawaida wa 38 huko Addis Ababa, Ethiopia;

**TUNAIDHINISHA** Azimio lililoambatishwa la Mkutano Maalumu wa Ajenda ya Baada ya **Malabo ya CAADP** kuhusu Kujenga Mifumo Endelevu na stahimilivu ya Chakula cha Kilimo barani Afrika uliofanyika tarehe 11 Januari 2025 Kampala, Uganda.

## AZIMIO LA CAADP LA KAMPALA KUHUSU KUJENGA MIFUMO HIMILIVU NA ENDELEVU YA KILIMO BARANI AFRIKA

**Sisi**, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU), tunakutana kwenye Mkutano Maalumu mjini Kampala, Uganda, kuanzia tarehe 9 hadi 11 Januari 2025. Tunathibitisha tena dhamira yetu kuhusu Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo barani Afrika (CAADP) na kutambua uharaka wa kufanya upya juhudi zetu ili kuendeleza maendeleo ya mifumo thabiti, jumuishi, na endelevu ya kilimo barani Afrika.

**TUKIREJELEA** Shabaha 1, Lengo la 5 la Ajenda 2063, inayolenga kukifanya kilimo kuwa cha kisasa ili kuongeza tija na uzalishaji.

**TUKIREJELEA ZAIDI** Azimio la Malabo la Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo barani Afrika (CAADP), lililopitishwa wakati wa Mkutano wa Kawaida wa Ishirini na Tatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU mjini Malabo, Equatorial Guinea, mwezi Juni 2014, ambapo Nchi Wanachama ziliazimia kuleta mageuzi ya kilimo jumuishi. Azimio la CAADP la Malabo pia lilithibitisha maamuzi ya awali, ikiwa ni pamoja na Azimio la Maputo la mwaka 2003 kuhusu CAADP na Azimio la Sirte la mwaka 2004 kuhusu changamoto za utekelezaji wa maendeleo jumuishi na endelevu katika kilimo na maji barani Afrika.

**TUKITAMBUA** kwamba idadi ya watu barani Afrika inakadiriwa kufikia watu bilioni 2.5 ifikapo mwaka 2050 huku idadi ya watu duniani ikitarajiwa kufikia watu bilioni 9.8, na kwa kutambua changamoto hiyo italeta mahitaji ya chakula na hitaji la ongezeko kubwa la uzalishaji wa kilimo, uzalishaji, usindikaji na biashara ya chakula.

**TUKITAMBUA** athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya kilimo na chakula, hususani kwa idadi ya watu walio hatarini, na kusisitiza ulazima wa kuwa na majibu ya kibunifu ambayo yanahakikisha upatikanaji wa chakula salama, cha bei nafuu na chenye lishe huku ikiimarisha ushirikiano na dhamira za kimataifa kwa mifumo endelevu.

**TUKIZINGATIA** ukuaji wa haraka wa miji na tabia zinazobadilika za matumizi kuhusiana na vyakula vilivyo tayari kuliwa na vilivyosindikwa, tunaona jukumu muhimu la kuimarisha sekta ya usindikaji wa chakula ili kuunganisha wakulima wadogo na masoko yanayokua ndani ya nchi na kanda. Ingawa inakua kwa kasi, sekta ya usindikaji bado iko katika hatua zake za mwanzo. Hivyo Afrika ina fursa ya kuweka mkakati ambao unakuza teknolojia na taratibu za usindikaji wa chakula ambazo huongeza matokeo ya lishe.

**TUKITAMBUA** athari za mabadiliko ya ubunifu wa kiteknolojia, maendeleo katika kilimo cha kidijitali, bayoteknolojia, na kilimo usahihi ili kuleta mapinduzi katika mifumo ya kilimo ya Afrika, pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkonono na zana za kidijitali ambazo zinaboresha ufikiaji wa wakulima kwa taarifa muhimu, huduma za kifedha na masoko.

**TUKIZINGATIA KWA WASIWASI** changamoto kubwa zinazoletwa na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira, utoaji wa gesi chafuzi na ukosefu wa utulivu wa kijamii, Afrika inakabiliwa na masuala magumu yanayoathiri moja kwa moja uzalishaji na uzalishaji wa kilimo. Kubadilika kwa mifumo ya mvua, kuongezeka kwa joto, na hali mbaya ya hewa inayozidi kuongezeka mara kwa mara inaonyesha kuna hitaji muhimu la usimamizi endelevu wa ardhi na maji, pamoja na taratibu za kilimo kinachozingatia tabianch. Zaidi ya hayo, kushughulikia kukosekana kwa utulivu wa kijamii, hususani uhamiaji unaosababishwa na migogoro, ni muhimu wakati bara linapopambana na athari za tabianchi na upungufu wa tija.

**TUKITAMBUA** nafasi muhimu ya masuala ya kijinsia katika kilimo, kuwawezesha wanawake, vijana na makundi yaliyotengwa ni jambo la msingi kwa sababu vikundi hivi vinaunda sehemu kubwa ya nguvu kazi ya kilimo katika nchi nyingi za Afrika. Kuondoa vikwazo vya kupata rasilimali kama vile ardhi, mikopo, na pembejeo za kilimo ni muhimu ili kuongeza tija kwa kiasi kikubwa na kuboresha usalama wa chakula na lishe. Sera na afua zinaozingatia jinsia ni muhimu kwa ajili ya kubadilisha sekta ya kilimo cha chakula na kujenga jamii imara zaidi.

**TUKIBAINISHA** uwezo mkubwa wa ushiriki wa vijana, idadi ya vijana inayokua kwa kasi barani Afrika inatoa fursa ya kuendeleza ubunifu na ukuaji wa kilimo. Kwa kuwapa vijana mafunzo, ushauri, na upatikanaji wa rasilimali muhimu, tunaweza kuwawezesha kuwa mawakala wa mabadiliko katika mifumo ya kilimo cha chakula. Ushirikiano huu sio tu unashughulikia masuala muhimu kama vile ukosefu wa ajira na uhamiaji wa vijijini-mijini lakini pia huleta mitazamo na nishati mpya, na kukuza mifumo ya kilimo inayobadilika zaidi na yenye mwelekeo kwa siku za usoni.

**TUKIZINGATIA** kwamba sera za biashara na ushirikiano wa kikanda, mipango kama vile Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) ni muhimu katika kubadilisha mifumo ya kilimo ya Afrika. AfCFTA inataka kuongeza biashaŕa ya ndani ya Afŕika kwa kupunguza ushuru, kuondoa vikwazo vya biashaŕa, na kuoanisha viwango, ili kuongeza upatikanaji wa soko na kustawisha mahusiano yenye nguvu zaidi ya kiuchumi miongoni mwa mataifa ya Afŕika. Ushirikiano huu unaimarisha ushindani na uthabiti wa kilimo, na kuiweka Afrika nafasi kwa ukuaji endelevu.

**TUKITAMBUA** jukumu muhimu la ujumuishaji wa viwanda vya kilimo ili kuongeza ukuaji wa uchumi, utengenezaji wa nafasi za kazi, na ustawi wa pamojam ni muhimu kuunganisha uzalishaji wa kilimo katika minyororo mipana ya ugavi ili kukabiliana na uhaba wa chakula na kuboresha lishe. Kufanikisha hili, hata hivyo, kunahitaji uwekezaji katika mifumo ya ubunifu wa teknolojia, huduma bora, miundombinu, pamoja na sera, udhibiti na mipangilio ya kitaasisi ili kuimarisha utendaji kazi na ushindani wa sekta inayoibukia ya usindikaji wa mazao ya kilimo.

**TUKITAMBUA** uwezekano wa kuleta mabadiliko katika teknolojia zinazoibukia ili kuongeza tija na uthabiti katika mifumo ya kilimo ya Afrika, ubunifu huu hutoa suluhu zenye ufanisi kwa changamoto kubwa kama vile ukosefu wa chakula na lishe, na mabadiliko ya tabianchi kwa kuboresha mbinu za kilimo na kuboresha usimamizi wa

rasilimali. Kutumika kwa mbinu, kilimo cha kidijitali, bayoteknolojia, na maendeleo mengine ya kiteknolojia ni muhimu ili kuimarisha ufanisi, uendelevu na uthabiti katika sekta hii.

**TUKISISITIZA** kwamba usimamizi endelevu wa maji, hasa katika maeneo yenye uhaba wa maji, ni msingi wa mabadiliko ya mifumo ya kilimo ya Afrika. Utekelezaji wa mbinu bora kama vile umwagiliaji kwa njia ya matone, uvunaji wa maji ya mvua, na urejelezaji wa maji ni muhimu kwa kuongeza tija ya kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la watu. Uwekezaji katika miundombinu ya maji na mbinu za usimamizi endelevu ni muhimu ili kuimarisha uthabiti wa mifumo ya kilimo cha chakula na kuhakikisha uendelevu wao wa muda mrefu.

**TUKITAMBUA** kwamba mahitaji mbalimbali ya wakulima, kutoka kwa wakulima wadogo hadi kwa shughuli kubwa, ni muhimu katika kufikia mabadiliko endelevu ya mifumo ya kilimo. Wakulima wadogo mara nyingi wanatatizika kutokana na upatikanaji mdogo wa rasilimali, wakati wakulima wa kati na wakubwa wanakabiliwa na vikwazo vya udhibiti na vifaa. Sera na mifumo ya msaada iliyoboreshwa ni muhimu ili kushughulikia changamoto hizi tofauti, kuwawezesha wakulima wote kuimarisha uzalishaji, kuongeza ukuaji kwa usawa, na kuimarisha usalama wa chakula na lishe katika bara zima.

**TUKISISITIZA** kwamba mabadiliko kwenye mfumo wa kilimo, yatashughulikia changamoto katika mfumo mzima wa kilimo cha chakula, huku tukioanisha sera na malengo mapana ya maendeleo. Mtazamo huu wa jumla unatanguliza uendelevu wa mazingira, unaongeza milo tofauti na yenye lishe ili kukabiliana na utapiamlo, na kuhakikisha ujumuishwaji wa kiuchumi kwa wakazi wengi barani Afrika wanaotegemea kilimo. Ajenda hiyo pia inalenga kupanua upatikanaji wa masoko na kukuza biashara ya kikanda, hasa kupitia Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), kwa lengo la kuongeza kwa kiasi kikubwa biashara ya kilimo ndani ya nchi za Afrika.

**TUKITAMBUA** umuhimu wa kupunguza hasara baada ya mavuno, tunasisitiza haja ya kukuza ubunifu katika utunzaji, uhifadhi na usafirishaji baada ya kuvuna ili kupunguza upotevu wa chakula na kuboresha upatikanaji wa chakula na mapato kwa wakulima.

**TUKIPOKEA** maazimio ya Mkutano Maalumu wa Kamati Maalumu ya Kitaalamu kuhusu Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Maji na Mazingira, uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 23-25 Oktoba 2024, na kuidhinishwa na Baraza Kuu Januari 2025.

Hivyo, tunapitisha **Mkakati na Mpangokazi wa CAADP: 2026-2035** na Azimio lifuatalo la **Kampala la CAADP kuhusu Kujenga Mifumo Himilivu na Endelevu ya Kilimo barani Afrika:**

**I. Dhamira ya Kuongeza Uzalishaji Endelevu wa Chakula, Uzalishaji wa Viwanda vya Kilimo na Biashara.**

Tumedhamiria kuongeza uzalishaji kwenye kilimo cha chakula kwa 45% ifikapo mwishoni wa 2035 kupitia kutumika kwa mbinu endelevu za kilimo ili kukidhi mahitaji ya chakula barani Afrika na fursa za biashara za kimataifa, kupunguza hasara ya baada ya kuvuna kwa 50%, kuongeza mara tatu ya biashara ya kilimo katika Afrika na bidhaa za vyakula na pembejeo ifikapo mwishoni mwa 2035 kwa kuzingatia AfCFTA, na kuongeza sehemu ya chakula kilichosindikwa ndani ya nchi hadi 35% ya Pato la Taifa linalotokana na kilimo ifikapo mwishoni mwa 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kuimarisha na kuhakikisha utendakazi wa mifumo ya pembejeo za kilimo—ikiwa ni pamoja na mifumo ya mbegu, mbolea, usimamizi wa maji, na utafiti wa kilimo na huduma za ugani—huku tukihimiza kupitishwa kwa kiasi kikubwa vitendo endelevu vya kilimo vinavyohifadhi rasilimali, kulinda mifumo ya ikolojia na kuhakikisha tija ya muda mrefu na uzalishaji.

b) Kuunda sera wezeshi na mazingira ya kiudhibiti ambayo yanakuza maendeleo na ujumuishaji wa teknolojia zinazoibuka, kama vile teknolojia ya kibayolojia, akili bandia, uwekaji kidijitali na kilimo chenye usahihi.

c) Kuchochea ukuaji, ushindani, na uendelevu wa biashara zinazohusiana na uzalishaji kwa ajili ya viwanda na kilimo, kwa kuzingatia hasa biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs).

d) Kuimarisha ujumuishaji wa wakulima wadogo, wanawake na vijana katika minyororo ya thamani na masoko ya kikanda, huku tukiendeleza na kuimarisha minyororo hii ili kuchochea uongezaji thamani katika hatua zote na kuhakikisha ushiriki na faida sawa katika uzalishaji wa kilimo na biashara, huku pia tukihakikisha uzingatiaji wa viwango vya uendelevu vinavyokidhi mahitaji ya kimazingira na kijamii ili kuimarisha ukuaji wa uchumi na ufanisi.

e) Kuimarisha upatikanaji wa soko na kurahisisha biashara kwa kuondoa vikwazo vya kibiashara na kuboresha miundombinu kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa wenye ufanisi.

f) Kuwekeza katika minyororo ya thamani ya kikanda, miundombinu ya mazao baada ya mavuno, bidhaa za chakula, na shoroba za biashara, kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kuongeza biashara ili kuboresha usalama wa chakula na lishe katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika.

**II. Dhamira ya Kukuza Uwekezaji na Ufadhili kwa ajili ya Mabadiliko ya Kasi ya Mifumo ya Chakula cha Kilimo**

Tunadhamiria kukusanya jumla ya dola bilioni 100 katika uwekezaji wa umma na wa binafsi katika mifumo ya chakula cha kilimo ya Affrika ifikapo 2035, huku tukihakikisha kuwa angalau 10% ya matumizi ya umma ya kila mwaka inatengwa kwa ajili ya mifumo ya chakula cha kilimo na kwamba angalau 15% ya Pato la Taifa la chakula cha kilimo inawekezwa tena kila mwaka katika sekta hiyo. Kwa kusudi hili, tunaazimia:

a) Kuongeza uwekezaji wa sekta ya umma na binafsi katika mifumo ya chakula cha kilimo ili kuendeleza ukuaji na uvumbuzi endelevu.

b) Kupanua uwekezaji wa sekta ya umma ili kusaidia miundombinu muhimu na mipango ndani ya mifumo ya chakula cha kilimo.
c) Kuimarisha uwezo wa kuendeleza na kutekeleza programu kuu na miradi inayokidhi vigezo vya kufadhiliwa, kuhakikisha kuwa uwekezaji unaleta matokeo yenye athari na makubwa.
d) Kuboresha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mabadiliko ya mifumo ya chakula cha kilimo, kuwezesha ushiriki mkubwa wa wadau katika sekta zote kwa kuhakikisha kwamba viwango vya kutosha vya fedha za tabianchi vinawafikia wakulima na wazalishaji na wasindikaji wa chakula wadogo na wa kati.

## III. Dhamira ya Kuhakikisha Usalama wa Chakula na Lishe

Tunadhamiria kufikia njaa sifuri katika Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika ifikapo 2035 na kupunguza udumavu kwa 25%, uzito mdogo tofauti na urefu (*wasting*) kwa 25% na uzito kupita kiasi kwa 25%, na kuhakikisha kuwa 60% ya watu wanaweza kumudu lishe bora. Kwa kusudi hili, tunaazimia:

a) Kukuza mifumo ya chakula cha kilimo ambayo huongeza lishe ya binadamu na matokeo ya afya, na hivyo kukuza vyakula vinavyochangia ustawi wa jumla.
b) Kukuza uzalishaji na matumizi ya mazao ya asili yenye lishe, na asilia, wanyama, na bidhaa za samaki na uvuvi kupitia sera maalum na marekebisho ya udhibiti na mikakati ya ufadhili kwa ajili ya minyororo hiyo ya thamani.
c) Kuimarisha sera za lishe, programu, elimu, na uelewa wa watumiaji ili kutokomeza upungufu wa virutubisho vidogo.
d) Kuimarisha Hatua za Usafi na Afya ya Mimea (SPS) na kutekeleza Protokali za mbinu ya Afya Moja ili kulinda usalama wa chakula na kulinda afya ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira.
e) Kuwekeza katika ufuatiliaji na utoaji wa ripoti za magonjwa, kuimarisha maabara za mifugo, kuongeza uzalishaji wa chanjo, kuweka kipaumbele katika kutokomeza PPR ifikapo 2030, na kuboresha ushirikiano katika magonjwa ya wanyama yanayovuka mipaka.
f) Kuweka kipaumbele katika utafiti na ukuzaji wa aina bora za mazao ya malisho na kukuza vyanzo mbadala vya malisho ili kuimarisha lishe ya mifugo na kupunguza utegemezi kwenye malisho ya asili.
g) Kuimarisha minyororo ya thamani ya uvuvi na ufugaji wa samaki huku tukikuza desturi endelevu, kujenga uhimilivu, na usimamizi bora na endelevu wa rasilimali za majini.
h) Kutengeneza mitandao ya kibunifu ya usalama wa kijamii ambayo inakabiliana vizuri na utapiamlo na kukuza usalama wa chakula na lishe.

## IV. Dhamira ya Kuendeleza Ujumuishi na Shughuli za Kujikimu zenye usawa

Tunadhamiria kupunguza idadi ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kwa 50% kupunguza tofauti ya mavuno kati ya wakulima wa kiume na wa kike kwa 50%, na kuwezesha angalau 30% ya wanawake, 30% ya vijana na 30% ya makundi yaliyotengwa katika minyororo ya thamani ya chakula cha kilimo ifikapo 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kuboresha miundombinu na upatikanaji wa huduma za kijamii katika maeneo ya vijijini na jamii zilizotengwa
b) Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali salama za uzalishaji kwa wanawake, vijana na makundi yaliyotengwa
c) Kutekeleza programu jumuishi za ulinzi wa kijamii zinazoshughulikia mahitaji ya watu walio katika mazingira magumu.
(d) Kuwezesha ajira zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na zinazozingatia mazingira kwa vijana, wanawake na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kupitia mipango inayosaidia biashara zinazozingatia kilimo bora na tabianchi, nishati mbadala katika biashara ya kilimo, masoko ya kaboni na kukabiliana na tabianchi.

**V. Dhamira ya Kujenga Mifumo Himilivu ya Chakula cha Kilimo**
Tunadhamiria kuhakikisha kuwa mifumo ya kilimo cha chakula barani Afrika inastahimili majanga ya hali ya hewa, kijamii na kiuchumi na kimazingira. Tunalenga kuwa na angalau 30% ya ardhi ya kilimo iliyo chini ya usimamizi endelevu na 40% ya kaya zilizokingwa dhidi ya majanga ifikapo 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:
a) Kuongeza uwekezaji katika uwezo wa kibinadamu na kimwili kwa ajili ya utafiti wa kilimo ili kuzalisha teknolojia na uvumbuzi unaopunguza mabadiliko ya tabianchi.
(b) Kuimarisha mifumo ya tahadhari na kukabiliana na majanga mbalimbali huku ikitekeleza mikakati ya kitaifa ya uhimilivu inayojumuisha uthabiti katika mipango na sera, hatimaye kukusanya rasilimali kwa ajili ya kujenga uwezo katika mifumo ya kilimo cha mazao ya kilimo.
c) Kuimarisha uwezo wa kufyonza wa mifumo ya chakula cha kilimo wa kupunguza uharibifu, kulinda njia za kujipatia riziki, na kusaidia juhudi za kujikwamua kufuatia vishindo au usumbufu.
d) Kukuza mikakati ya kukabiliana na hali ndani ya mifumo ya chakula cha kilimo na njia za kujipatia riziki ili kupunguza uwezekano wa kuathiriwa na vishindo na shinikizo kubwa.
e) Kuongeza ukusanyaji wa fedha ya tabianchi na msaada wa kiufundi ili kuwasaidia wakulima, hususan wakulima wadogo, na kuhama kuelekea kwenye mbinu za kilimo zinazozalisha kaboni kwa kiwango kidogo.
f) Kukuza maarifa na desturi asilia, tukitambua jukumu lake katika kukuza utunzaji wa mazingira na uhimilivu.

**VI. Dhamira ya Kuimarisha Utawala wa Mifumo ya Kilimo**
Tunadhamiria kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2028, Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) zinatafsiri Azimio la CAADP la Kampala katika mipango yao ya kitaifa na ya kikanda ya uwekezaji wa kilimo cha mazao ya chakula  na kupitisha mbinu bora katika utawala wa sekta ya chakula kwa kuzingatia kanuni za CAADP. Mbali na hayo, kufikia 2030, nchi zote zitajumuisha mchakato wa Mapitio ya Kila Miaka Miwili ya CAADP katika majukwaa yao ya kitaifa ya mapitio ya pamoja ya sekta. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:
a) Kudumisha kanuni za CAADP zinazojumuisha ukuaji wa uchumi unaoongozwa na kilimo kwa maendeleo jumuishi na endelevu; kukamilishana na ushirikiano wa kikanda; na, ushirikishwaji wa wadau wote, hasa wanawake, vijana na makundi yaliyo katika mazingira magumu.

b) Kukuza ufanyaji maamuzi unaotegemea ushahidi na uwajibikaji wa pande zote, kuhakikisha kwamba utekelezaji unaongozwa na data ya kuaminika.
c ) Kuimarisha Kamisheniya Umoja wa Afrika, AUDA-NEPAD, na RECs ili kuziwezesha kutekeleza majukumu na mamlaka zilizoainishwa katika Azimio hili.
d) Kuandaa hati ya kifedha kwa lengo la kurahisisha utekelezaji bora wa Azimio hili.
e) Kuwezesha mabunge ya kitaifa, kikanda na mabara na kamati zake, kuhakikisha uoanishaji thabiti wa sheria na bajeti za kitaifa kwa malengo ya Azimio la CAADP la Kampala, na kutoa usimamizi kwa ajili ya utekelezaji bora wa sera husika.
f) Kuimarisha mashirika ya wazalishaji ili kuyawezesha kutimiza wajibu wao katika kuandaa na kutekeleza sera za kitaifa na kikanda pamoja na majukumu yaliyoainishwa katika Azimio hili.

**VII. Wito wa Kuchukua Hatua**

Sisi, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tunatambua kwamba ili kufikia malengo na shabaha zilizowekwa katika Azimio hili tutahitaji kujitolea kwa wadau mbalimbali kubadilisha maamuzi haya kuwa matokeo yanayoonekana. Ili kufanikisha hili, tunatoa wito kwa:

a) **Nchi Wanachama**:

- Kuunganisha na kutafakari Dhamira katika Azimio hili katika sera za kitaifa, mikakati na mifumo ya bajeti, kwa ajili ya utekelezaji bora kupitia Mipango ya Kitaifa ya Uwekezaji wa Mifumo ya Kilimo (NAIPs) na kuhakikisha kuwa programu na zana za utekelezaji zimewekwa ili kutekeleza NAIPs.
- Kubuni na kutekeleza sera za kina, madhubuti zinazokuza uwekezaji wa sekta binafsi katika mabadiliko ya mifumo ya kilimo huku tukihakikisha uungwaji mkono wa sekta ya umma kwa mifumo hii.
- Kuongeza uwekezaji katika miundombinu, utafiti, na huduma za ugani ili kusaidia mageuzi ya mifumo ya kilimo
- Kuhakikisha mifumo ya uratibu ifaayo iko na kuna ushirikishwaji wa jumla katika usimamizi wa mifumo ya kilimo na uangalizi maalumu kwa wanawake, vijana na makundi yaliyotengwa.
- Kuhakikisha uwezo wa kutosha na kuteua timu ya kuu ya Ufuatiliaji na Tathmini, inayoungwa mkono na mifumo ya maarifa ya Afrika nzima, wataalamu maalumu, na majukwaa thabiti ya kidijitali ili kupima ubora wa utendaji kazi na usimamizi wa data.

b) **Umoja wa Afrika (AUC na AUDA-NEPAD) na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs)**:

- Kusaidia Nchi Wanachama wa AU na RECs kujumuisha Dhamira katika Azimio hili katika Mipango ya Kitaifa na Kikanda ya Uwekezaji wa Kilimo (NAIPs na RAIPs).
- Kuwezesha ushirikiano wa kikanda, ushirikiano wa kiuchumi, na upatanishi wa sera katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuimarisha biashara ya ndani ya Afrika.
- Kuanzisha baraza la ushauri linaloongozwa na sekta binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.
- Kuendesha Mchakato wa Mapitio ya Kilimo yanayofanyika kila baada ya miaka miwili, kuanzia mwaka 2027, na kutoa ripoti ya maendeleo kwa Mkutano Mkuu wa Kawaida utakaofanyika kuanzia Januari/Februari , mwaka 2028.

- Kuimarisha matumizi ya matokeo ya ripoti ya mapitio ya kila baada ya miaka miwili ya CAADP ili kupanga na kufanya maamuzi katika ngazi za kitaifa, kikanda na bara.

c) **Wakulima na wazalishaji wa vijijini** :

- Kupitisha kanuni za kibunifu na teknolojia mpya ili kuongeza tija ya kilimo, uendelevu na uhimilivu.
- Kuwekeza katika kukuza ubunifu wa uzalishaji na ushindani wa gharama ili kupata sehemu kubwa ya masoko ya ndani na ya kikanda.

d) **Asasi za kiraia** :

- Kuunda mfumo maalumu wa kusimamia Mipango ya Kitaifa na Kikanda ya Uwekezaji wa Kilimo (NAIPs/RAIPs), kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wake.
- Kutetea ugawaji wa rasilimali kwaajili ya maendeleo ya mifumo ya kilimo, kuongeza fursa za ufadhili na msaada wa utekelezaji wa NAIPs/RAIPs.
- Kukuza kanuni za kilimo endelevu na sawa katika mabadiliko ya mifumo ya kilimo.

e) **Sekta binafsi** :

- Kuwekeza katika teknolojia, uvumbuzi, ukuzaji wa soko na ujumuishaji wa mnyororo wa thamani ili kuleta mageuzi ya mifumo ya kilimo.
- Kuongeza uwekezaji katika minyororo endelevu ya thamani ya mazao ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula, viwanda vya kilimo na biashara.

f) **Wabunge** :

- Kuhakikisha sekta ya umma inawekeza kwa usahihi katika mifumo ya kilimo ili kufikia lengo la asilimia 10 la matumizi ya kila mwaka ya umma katika mifumo ya kilimo.
- Kufuatilia na kuhakikisha matumizi bora ya fedha za umma katika mifumo ya kilimo katika ngazi ya kitaifa na kikanda .

g) **Wadau wa maendeleo na mashirika ya kimataifa** :

- Kujitolea kusaidia utekelezaji wa Mkakati na Mpango Kazi wa CAADP: 2026-2035 na Azimio la CAADP la Kampala kwa kuoanisha rasilimali zao za kitaalamu na kifedha kwa vipaumbele vya bara,
- Kusaidia AUC, AUDA-NEPAD na jumuiya za kiuchumi za kikanda ili kutoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama ili kutafsiri Azimio la Kampala CAADP katika NAIPs/RAIPs,
- Kusaidia mifumo ya data na juhudi za uwajibikaji wa pande zote katika ngazi ya bara, kikanda na kitaifa.

Azimio hili litaanza kutumika tarehe 1 Januari 2026.

***Limeandaliwa Januari 11, 2025 Kampala, Uganda.***

## AZIMIO KUHUSU MKUTANO WA 6 WA URATIBU WA NUSU MWAKA

**SISI**, Wakuu wa Nchi na Serikali, wanaowakilisha Mkutano wa Umoja wa Afrika na Wenyeviti wa Jumuiya Nane (8) za Kiuchumi za Kikanda (RECs) pamoja na Vyombo vya Kikanda vya Ulinzi wa Haki (RMs), wanaokutana Accra, Ghana tarehe 21 Julai 2024 katika Mkutano wa Sita wa Uratibu wa Nusu Mwaka, unaoongozwa na Mhe. Mohamed Cheikh El Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika;

**TUKIKUMBUKA** matokeo ya Mikutano mitano iliyotangulia ya Uratibu ya Nusu Mwaka, ambayo Azimio la karibuni la tarehe 16 Julai 2023 mjini Nairobi, Kenya likiwa katika nyaraka MYCM/AU/ Decl.(V);

**TUKISISITIZA** haja ya kukuza ushirikiano katika nyanja zote za juhudi za binadamu ili kuinua kiwango cha maisha ya watu wa Afrika, na kudumisha na kuimarisha utulivu wa kiuchumi, kukuza uhusiano wa karibu na wa amani kati ya Nchi Wanachama na kuchangia maendeleo, na ushirikiano wa kiuchumi wa Bara;

**TUKISISITIZA** haja ya kuoanisha sera za kitaifa na kikanda ili kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika bara zima;

**TUKITAMBUA** kwamba kukuza biashara ya ndani ya Afrika bado ni jambo la msingi kwa maendeleo endelevu ya kiuchumi, uzalishaji wa ajira na ushirikiano mzuri wa Afrika katika uchumi wa dunia; na

**TUKISISITIZA** kwamba utekelezaji wa Protokali ya Mahusiano kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda unaweka wajibu kwa Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda wa kuhakikisha kwamba Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda zinahakikisha kuifanikiwa kwa mchakato wa utangamano wa bara kwa njia ya ufanisi zaidi inayowezekana, na kwamba mchakato huu wa utangamano unaharakishwa ili Afrika iweze kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na utandawazi.

**TUNATAMKA KUWA:**

1. **TUNAMPONGEZA** Mwenyekiti wa AU, Mohamed Ould Cheikh El-Ghazouani, Rais wa Jamhuri ya Kiislamu ya Mauritania, kwa jitihada zake za kukuza amani, usalama na haki za binadamu ndani ya bara; na

2. **TUNATHAMINI** matarajio ya mafanikio yaliyofunguliwa kupitia ushiriki wake kamili na unaojenga na utetezi wake kwa wabia wa kimataifa kuhusu vipaumbele vya bara, hususan kwa kuhusiana na msamaha wa madeni, maendeleo endelevu ya dunia na mwitikio kwa changamoto za usalama wa jamii.

**HALI YA UTANGAMANO**

3. **TUNAZINGATIA** Ripoti ya Kamisheni kuhusu utangamano wa Bara la Afrika na **TUNAZINGATIA ZAIDI** Ripoti za Wenyeviti wa Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kuhusu hali ya Utangamano wa Kikanda kama ifuatavyo:

   i. **Mhe. Mohammad Younis Menfi**, Rais wa Baraza la Urais la Nchi ya Libya na Mwenyekiti wa sasa wa Umoja wa Arab Maghreb (AMU).
   ii. **Mhe. Mahamat Idriss Deby**, Rais wa Jamhuri ya Chad na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Nchi za Sahel-Sahara (CENSAD);
   iii. **Mhe. Hakainde Hichilema**, Rais wa Jamhuri ya Zambia na Mwenyekiti wa sasa wa Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA);
   iv. **Mhe. Salva Kiir Mayardit**, Rais wa Jamhuri ya Sudani Kusini na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC);
   v. **Mhe. Teodoro Obiang Nguema Mbasogo,** Rais wa Jamhuri ya Equatorial Guinea na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS);
   vi. **Mhe. Bola Ahmed Tinubu**, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Nigeria na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS);
   vii. **Mhe. Ismail Omar Guelleh** , Rais wa Jamhuri ya Djibouti na Mwenyekiti wa sasa wa Mamlaka ya Kiserikali kuhusu Maendeleo (IGAD);
   viii. **Mhe. João Manuel Gonçalves Lourenço,** Rais wa Jamhuri ya Angola na Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

**RIPOTI ZA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI NA VINARA WENYE KAZI MAALUM**

4. **TUNAZINGATIA** ripoti za Waheshimiwa Marais na Vinara wenye Kazi Maalum:
   i. Mhe. Dkt. **Paul Kagame**, Rais wa Jamhuri ya Rwanda na Mwenyekiti wa sasa wa Mkutano Mkuu wa Kikosi cha Dharura cha Afrika Mashariki na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake:
   ii. Mhe. Abdelmadjid Tebboune, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Algeria na Mwenyekiti wa sasa wa Jeshi la Kanda ya Afrika Kaskazini na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake:
   iii. Mhe. Abdel Fattah El-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiislam ya Misri na Mwenyekiti wa Kamati ya Maelekezo ya Wakuu wa Nchi na Serikali (HSGOC) wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Afrika (AUDA NEPAD), na **KUPITISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake.
   iv. **Mhe. Nana Addo Dankwa Akufo-Addo**, Rais wa Jamhuri ya Ghana na Mhamasishaji wa AU kuhusu Taasisi za Fedha za AU, na KUPITISHA mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti hizo mbili, ambazo ni:

- Kuanzishwa kwa Taasisi za Fedha za Umoja wa Afrika (AUFIs); na
- Kuongeza ushirikiano kwa ajili ya Utangamano wa Kiuchumi: kutumia miamala ya simu kufanya mauzo na manunuzi Barani kote;

v. Mhe. Denis Sassou Nguesso, Rais wa Jamhuri ya Kongo na Makamu Mwenyekiti wa Pili wa Ofisi (*Bureau*) ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali, na **KUIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo yanayohusiana na mahitimisho ya Mkutano wa Kwanza wa Kimataifa kuhusu Upandaji miti na upandaji upya wa miti (CIARI); **TUNAPITISHA** mapendekezo kuhusu msimamo wa pamoja wa Afrika yaliyomo kwenye ripoti yake na **TUNAIDHINISHA** zaidi kwamba Ripoti hiyo ipelekwe kwenye Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA 79) kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa kwa Muongo wa Dunia wa Upandaji miti na upandaji tena. na

vi. Mhe. Mahamadou Issoufou, Mhamasishaji wa AU kuhusu AfCFTA na **KUIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake.

**RIPOTI ZA KAMISHENI YA AU, VYOMBO VYAKE NA WABIA KUHUSU HALI YA UTANGAMANO BARANI AFRIKA**

5. **TUNATOA WITO** kwa Kamisheni, RECs na RMs, kwa kushirikiana na UNECA na AfDB, kuchapisha Ripoti ya Utangamano kila baada ya miaka miwili, kuanzia mwaka 2025, kwa misingi ya Faharasa mpya ya Ushirikiano wa Kikanda wa Afrika (ASRII);

6. **TUNAKUMBUSHIA** haja ya kuendelea kuboresha kiwango cha Utangamano ndani ya RECs na pia katika ngazi ya bara na **KUTOA WITO** kwa Nchi Wanachama, Kamisheni ya AU, RECs, RMs na AUDA-NEPAD kuimarisha ushirikiano wao katika utekelezaji wa Ajenda ya Utangamano wa Afrika;

7. **TUNAIOMBA** Kamisheni kuendelea kutetea uendelezaji wa ushirikiano baina ya REC kwa nia ya kuharakisha ajenda ya utangamano wa Afrika na KUTOA WITO KWA Nchi Wanachama kutenga rasilimali fedha za kutosha zitakazohakikisha utekelezaji mzuri wa ajenda ya utangamano;

8. **TUNAITAKA** Kamisheni, kwa kushirikiana na UNECA, RECs na taasisi zinazohusika za AU, kuendeleza uundaji wa mbinu moja ya kina na iliyowianishwa pamoja na faharasa maalumu ya kutathmini utangamano wa Afrika ambayo inatumia uwezo wa faharasa zilizopo katika Kamisheni ya AU (AMRII) na UNECA (ARII). Faharasa ya Pamoja inapaswa kuwiana na malengo ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika (Mkataba wa Abuja) na Ajenda 2063;

**MGAWANO WA KAZI KATI YA UMOJA WA AFRIKA, JUMUIYA ZA KIUCHUMI ZA KIKANDA/VYOMBO VYA KIKANDA VYA ULINZI WA HAKI NA NCHI WANACHAMA**

9. **TUNAZINGATIA** ripoti ya Mhe. Pierre Mbonjo Moukoko, Mkuu wa Kitengo cha Kamisheni cha Utekelezaji wa Mageuzi na **KUIDHINISHA** mapendekezo yaliyomo ndani yake; na

10. **TUNAIOMBA** Kamati ya Uratibu (ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Kamisheni, Makatibu Wakuu wa RECs na AUDA-NEPAD) kupeleka ripoti ya mwisho kuhusu Mgawanyo wa Kazi kwa Baraza Kuu, kwa kuendana na taratibu zilizoanzisdhwa, na ili iwasilishwe kwenye Mkutano wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa AU kwa ajili ya kupitishwa mwezi Februari 2025.

**JUKWAA LA AU LA KUBADILISHANA MAARIFA BAINA YA KANDA (I-RECKE) KWA TAHADHARI YA MAPEMA**

11. **TUNAKARIBISHA** Ripoti ya Mwaka kuhusu Shughuli za Jukwaa la Kubadilishana Maarifa baina ya Kanda (I-RECKE) kuhusu Tahadhari ya Mapema na Uzuiaji wa Migogoro;

12. **TUNAIDHINISHA** ripoti ya Kikao cha Tatu cha Sera cha Jukwaa la Kubadilishana Maarifa baina ya kanda (I-RECKE) kuhusu Tahadhari ya Mapema na Uzuiaji wa Migogoro na shughuli za I-RECKE; na **KUIPONGEZA** Kamisheni na RECs/RMs, kama wajumbe wa jukwaa la I-RECKE, kwa maendeleo makubwa yaliyopatikana katika ulimganishaji wa jitihada na uongezekaji wa athari katika eneo la ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya mipango ya amani na usalama ya kikanda na kibara.

13. **TUNASISITIZA** dhima muhimu ya I-RECKE kama jukwaa la kimkakati la kuimarisha Mfumo wa Tahadhari za Mapema wa Bara la AU; katika suala hili, na **KUTOA WITO** kwa Nchi Wanachama na washirika kuunga mkono shughuli za I-RECKE ili kuongeza uratibu na ushirikiano kati ya RECs/RMs na na Nchi Wanachama, Kamisheniya AU, kuelekea ushirikiano wa kikanda katika uwanja wa amani na usalama;

14. **TUNAPONGEZA** ushirikiano ulioimarishwa wa I-RECKE na Mtandao wa Umoja wa Afrika wa Taasisi za Sera kwa ajili ya amani (AU NeTT4Peace); na **KUKARIBISHA** maendeleo yaliyofanywa na AUNeTT4Peace kama mtandao wa taasisi za sera wa Kiafrika unaounganisha tofauti ya nadharia na sera, kama sehemu ya dira yake ya kuwa na Afrika yenye amani, usalama na mafanikio; na dhima ya kutoa muunganisho wa kimkakati kati ya jumuiya za maarifa na Umoja wa Afrika kwa ajili ya uundaji bora wa sera na utekelezaji wenye matokeo kuelekea Afrika Tunayoitaka; **na TUNAHIMIZA** jukumu la Mtandao

kushughulikia Kipaumbele kimojawapo cha AU cha kukuza mbinu ya maarifa ya hatua za amani, usalama na demokrasia za AU na kuziba pengo kati ya utafiti, sera na utendaji;na

15. **TUNAOMBA** I-RECKE, kama jukwaa la ndani ya bara, kuendelea kuzidisha juhudi zake katika kuboresha mbinu bora za kikanda kuhusu tahadhari ya mapema, uzuiaji wa migogoro, uthabiti na ujenzi wa amani kati ya AU na RECs/RMs.

**AUDA-NEPAD**

16. **TUNATHIBITISHA** jukumu kuu la uratibu la Kamisheni ya AU na AUDA-NEPAD kuhusiana na shughuli za kipaumbele zzote za maendeleo za kikanda na za bara barani Afrika, kwa mujibu wa mamlaka yake kama wakala wa maendeleo wa Umoja wa Afrika;

17. **TUNATAMBUA kazi kubwa ya Kamisheni na AUDA-NEPAD katika ripoti ya** tathmini ya Muongo wa Kwanza wa Utekelezaji wa Ajenda 2063 na uandaaji na ukadiriaji gharama uliofuatia wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi (STYIP); **TUNAHIMIZA** Nchi Wanachama wa AU, RECs, RMs na wabia kupitisha vyombo vya uingizaji kwenye mipango ya ndani na utekelezaji, kutenga rasilimali za kutosha za kiufundi na kifedha, na kushirikiana kwa karibu na Kamisheni ya AU na AUDA-NEPAD ili kuharakisha utekelezaji wa Ajenda 2063; na **KUWASIHI** kuendelea kuimarisha uwezo wa RECs na Nchi Wanachama katika kupanga mazingira (*scenarios*), uchambuzi wa maono ya mbeleni, ufuatiliaji na utoaji ripoti kuhusu Ajenda 2063;

18. **TUNAZINGATIA** dhana na kuundwa kwa Mpango Mkuu wa Timu ya Afrika *Africa Team Flagship initiative* kulikofanywa na *Kamisheni ya AU na AUDA NEPAD*, kwa ushirikiano na AfCFTA, ACDC, APRM, PAP, na RECs, kama Programu Kuu ya AU ya Ukusanyaji wa Rasilimali ili kuharakisha ukusanyaji wa rasilimali kwa mlolongo wa Programu za Uwekezaji zenye Matokeo Makubwa zinazolenga kuharakisha utekelezaji wa STYIP; na **KUIOMBA** Kamisheniya na AUDA-NEPAD kuhakikisha kwamba uzinduzi rasmi wa Programu ya Timu ya Afrika unafanyika katika Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika mnamo mwezi Februari 2025;

19. **TUNAKARIBISHA** jitihada za Kamisheni na AUDA-NEPAD katika kuandaa Dashibodi ya Ajenda 2063 ili kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa Ajenda 2063 unaofanywa na Nchi Wanachama katika ngazi za Kanda na Bara; **TUNAZIPONGEZA** Nchi Wanachama ambazo zimetumia Dashibodi kutoa ripoti kuhusu Mpango wa Kwanza wa Utekelezaji wa Miaka Kumi na **KUZIHIMIZA** Nchi Wanachama zote kutumia Dashibodi kutoa ripoti na kufuatilia maendeleo

ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Miaka Kumi wa Ajenda 2063; na

20. **TUNAZISIHI** Nchi Wanachama na RECs kuunga mkono mpango wa Dawati la Afrika la Ujuzi wa Dunia yaani *WorldSkills Africa Desk* uliozinduliwa na Kamisheni ya AU na AUDA-NEPAD mnamo Februari 2024, kama mpango mkuu wa Kaulimbiu ya Mwaka ya 2024 ya Umoja wa Afrika kuhusu Elimu, kwa lengo la kuzipa nchi za Afrika jukwaa mahususi la kuboresha ukuzaji wa ujuzi, kujenga uwezo, na kufikiria upya mifumo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) barani kote.

**MIPANGO MIKUU YA BARA YA BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AfDB)**

21. **TUNAZINGATIA** Ripoti ya Mhe. Dkt. Akinwumi A. Adesina, Rais wa Kundi la Benki ya Maendeleo ya Afrika(AfDB);
22. **TUNAPONGEZA** jitihada za AfDB katika kutetea na kutekeleza mipamgo ya bara kama inavyoamuliwa na Vyombo vya Sera vya AU ili kukusanya fedha za kufanikisha mabadiliko ya kiuchumi na ajenda ya utangamano ya bara, ikiwa ni pamoja na msaada wa kitaasisi kwa Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda;

23. **TUNATAMBUA** maendeleo makubwa yaliyofikiwa katika 5s zote za AfDB – Angaza Afrika, Lisha Afrika, Weka viwanda Afrika, unganisha Afrika na Boresha Ubora wa Maisha wa Watu wa Afrika – kama kichocheo cha utekelezaji wa Ajenda 2063, na msaada katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu ya UN;

24. **TUNAKUMBUSHA** uamuzi Assembly/AU/Dec. 817(XXXV) katika kukusanya fedha kwa ajili ya kuimarika haraka kiuchumi kwa Afrika, maendeleo na utangamano, na **TUNAKARIBISHA** maendeleo makubwa katika utekelezaji wa mipango mikuu ikiwa ni pamoja na dhamana ya *Security-Indexed Investment Bond,* uanzishwaji wa chombo cha utulivu wa Kifedha cha Afrika na kuelekeza upya mali za akiba (special Drawing Rights) za IMF kwa Afrika kupitia taasisi za maendeleo zinazohusisha nchi nyingi kama vile AfDB;

25. **TUNAKARIBISHA ZAIDI** msaada wa kiufundi wa AfDB kwa klabu ya Wakuu 12 wa Nchi na Serikali chini ya uongozi wa Mhe. Raisi Sassou Nguesso, Rais wa Jamhuri ya Kongo, katika utetezi wa GDP ya “kijani” inayojumuisha mtaji wa asili;

26. **TUNATOA WITO** wa utengaji mkubwa kwenye mzunguko wa 17 wa Mfuko wa Maendeleo wa Afrika mwaka 2025 kwa shabaha ya kukusanya dola bilioni 25 ili kuwezesha mahitaji yanayoongezeka ya bara; na

27. **TUNAISIHI** AfDB kuwasilisha taarifa juu ya maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Azimio hili kwenye Mkutano wa Kawaida wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali mwezi February 2025.

**SHUKRANI**

28. **TUNATOA SHUKRANI** kwa jitihada zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Ghana katika kufanikisha Mkutano wa Sita wa Uratibu wa Nusu Mwaka kati ya AU, RECs and RMs.

**Limeandaliwa Accra, Ghana, tarehe 21 Julai, 2024**

# AZIMIO
# KUHUSU HALI YA PALESTINA NA MASHARIKI YA KATI
# Doc. Assembly/AU/18(XXXVIII)

**SISI,** Wakuu wa Nchi na Serikali za AU, katika kikao cha Kawaida cha Thelathini na Saba cha Mkutano Mkuu wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, tarehe 17 na 18 Februari 2025;

**KWA KUZINGATIA** taarifa kuhusu hali ya Palestina na Mashariki ya Kati, **TUKITHIBITISHA** maazimio yote yaliyotangulia, pamoja na maamuzi na maazimio yaliyopitishwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika na Umoja wa Afrika kuhusu hali ya Palestina katika kuhakikisha amani ya kudumu na usalama katika ukanda wa Mashariki ya Kati;

**TUKITHIBITISHA PIA** uungaji mkono wetu kikamilifu kwa watu wa Palestina katika mapambano yao halali dhidi ya uvamizi wa kibaguzi wa Israel, unaowakilishwa na Jumuiya ya Ukombozi wa Palestina inayoongozwa na Rais Mahmoud Abbas, kurejesha haki zao za halali zisizoweza kuondolewa, haki ya kwanza kati yao ikiwa haki ya kujitawala, uhuru, na kurejea kwa wakimbizi, na kuanzisha nchi huru ya Palestina huku Jerusalem mashariki ikiwa mji mkuu, kuishi kwa amani pamoja na Nchi ya Israeli.

**TUKISISITIZA** nia na dhamira yetu ya kuunga mkono kufikia suluhu la amani na la haki kwa mzozo wa Waarabu na Israel kwa mujibu wa kanuni za sheria za kimataifa na maazimio yote muhimu ya Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa Azimio la 194 la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

**TUKIREJEA TENA** wito wetu wa kila mara wa kusitisha operesheni ya kijeshi katika Ukanda wa Gaza huku tukifuatilia kwa karibu matukio makubwa katika ardhi za Palestina na unyanyasaji wa kikatili unaofanywa na mamlaka za Israel tangu tarehe 07 Oktoba 2023.

**TUKIELEZEA** masikitiko yetu na kulaani maafa ya kibinadamu yaliyotokea katika Ukanda wa Gaza na Kusini mwa Lebanon kama matokeo ya moja kwa moja ya operesheni ya vikosi vya Israeli, idadi kubwa na ambayo bado inazidi kuwa mbaya ya vifo vya raia, uharibifu wa sekta iliyozingirwa, kuhamishwa kwa nguvu kwa wakaazi wake, na kutoheshimu utakatifu wa hospitali na maeneo ya ibada ikiwa ni ukiukwaji wa wazi wa sheria ya masuala ya kibinadamu ya kimataifa.

**TUKITHIBITISHA TENA** hadhi na kiini cha sababu ya haki ya Palestina, na msimamo wetu thabiti wa kuiunga mkono, kwa kuzingatia maadili ya uhuru na ukoloni, ukandamizaji, ubaguzi wa rangi, na ukosefu wa haki

**TUKIZITAKA** Nchi zote Wanachama wa AU kuendelea kuunga mkono dhamira ya Palestina kwa namna ambayo itahakikisha utekelezaji wa maadili na kanuni tukufu ambazo kwayo Shirika la Umoja wa Afrika/Umoja wa Afrika ulianzishwa; miongoni mwa kanuni muhimu zaidi ni kuunga mkono harakati za ukombozi na haki ya watu kujitawala, na kujiepusha na hatua au mwelekeo wowote unaoweza kudhoofisha mshikamano na Palestina na haki za watu wa Palestina.

**TUKIPINGA** ukiukwaji wa Israel, kama mamlaka inayoikalia kwa mabavu, wa haki za kimsingi na uhuru wa watu wa Palestina, na kunyimwa haki za kimsingi kabisa za maisha, na kuanzishwa kwa mfumo wa kibaguzi unaobagua watu kwa misingi ya rangi na dini, unaohakikisha uendelevu wa uvamizi wa Israel.

**Tunatamka yafuatayo:**

1. **TUNALAANI** Israeli, jeshi la uvamizi, kutokana na vita vya kikatili katika Ukanda wa Gaza tangu tarehe 7 mwezi Oktoba 2023, ambayo ililenga Wapalestina milioni 2.2 na matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya raia wasio na silaha, yakilenga makanisa, misikiti, mahospitali, nyumba za raia, miundombinu, hivyo kusababisha adhabu kwa raia, na kukatika kwa msaada wa kibinadamu kwa sekta, hivyo kupelekea vifo na majeraha kwa maelfu ya Wapalestina.

2. **TUNAKEMEA** sera za Israel, zilizodhihirishwa katika hatua za pamoja za adhabu dhidi ya raia na uvamizi wa Israel dhidi ya Ukanda wa Gaza. Sera hizi zinajumuisha uhalifu wa kivita unaothibitisha uwajibikaji wa kimataifa

3. **TUNAONESHA** kukataa kwetu kwa uthabiti na kabisa kwa pendekezo lolote au jaribio la kufuta sababu ya Palestina kwa kuwahamisha watu wa Palestina kutoka katika nchi yao, ikiwa ni pamoja na Ukanda wa Gaza, jambo ambalo ni ukiukaji wa wazi wa Sheria ya Kimataifa na msimamo thabiti wa Umoja wa Afrika unaotaka haki ya watu wa Palestina ya kujitawala.

4. **TUNATOA WITO ZAIDI** wa kuanzisha taifa la Palestina ikiwa ni msimamo wa Umoja wa Afrika usioyumba .

5. **TUNATOA WITO** kwa nchi zote za Afrika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kufanya kazi na jumuiya ya kimataifa kwa ajili ya misaada ya haraka kwa Ukanda wa Gaza ulioathirika na kukomesha maafa ya kibinadamu yaliyosababishwa na vita vya hivi majuzi vya Israel dhidi yake, na kufanya kazi kwa bidii katika kuishinikiza Israel, mamlaka inayokalia kwa mabavu, ili kuondoa kizuizi kisicho cha haki cha Israeli kwenye Ukanda huo na kuharakisha mchakato wa ujenzi mpya.

6. **TUNATHIBITISHA** uungwaji mkono wa kisiasa, kiuchumi na kifedha kwa Taifa la Palestina, na ulazima wa kuwezesha umoja wa kijiografia na kisiasa katika ardhi za Palestina kati ya Ukingo wa Magharibi (*West Bank*) na Ukanda wa Gaza.

7. **TUNASIKITISHWA na** baadhi ya nchi kuunga mkono uvamizi wa Israeli, ambao ulisababisha Israeli kufanya operesheni zake za kijeshi zinazolenga raia wa Palestina na mali zao, pamoja na kuharibu miundombinu katika eneo lililozingirwa la Ukanda wa Gaza kwa kisingizio cha "Haki ya Israel ya kujilinda yenyewe"

8. **TUNAKATAA NA KULAANI** Israeli kukiuka sheria za kibinadamu za kimataifa, hasa Mkataba wa Nne wa Geneva, kwa kulenga hospitali, vituo vya afya, miundombinu ya utoaji habari, na matumizi ya silaha zilizopigwa marufuku kimataifa, na kuunga mkono wito wa kufanya uchunguzi huru wa kimataifa kuhusu ukiukaji huu.

9. **TUNASISITIZA** haja ya dharura kuharakisha kufungua njia salama kupunguza mateso ya Watu wa Palestina na kulinda taasisi za afya na za kibinadamu.

10. **TUNALAANI PIA** sera ya utawala wa Israeli ya kuweka watu kizuizini bila kuwapeleka mahakamani na **TUNAZITAKA** mamlaka kuwaachia haraka wafungwa wa Kipalestina, hasa watoto, wanawake, wazee na wagonjwa, waliozuiliwa kwenye mazingira magumu kinyume na haki zote kwa mujibu wa sheria na mikataba iliyopo ya kimataifa.

11. **TUNASISITIZA** kuendelea kuunga mkono uthabiti wa watu wa Palestina katika kudai ardhi yao, na kuendelea kuunga mkono suluhisho la amani na usawa katika mgogoro wa Waarabu na Wapelestina kwa kuzingatia misingi ya sheria za kimataifa na maazimio yote husika ya Umoja wa Mataifa, ambayo yanasisitiza kuanzishwa kwa Dola ya Palestina yenye uhuru na mamlaka kamili ya kujitawala kwenye mipaka ya tarehe 04 mwezi Juni 1967, na makao yake makuu yakiwa Yerusalemu Mashariki.

12. **TUNASISITIZA** umuhimu wa kupata suluhu kuhusu suala la Palestina ili kupata amani kamili katika ukanda wa Mashariki ya Kati, kwa kuzingatia suluhisho la dola mbili, sheria za kimataifa, maazimio yote ya jumuiya ya kimataifa, Mpango wa Amani wa Waarabu, maamuzi ya Umoja wa Afrika, na kuongozwa na maono ya Mheshimiwa Rais Mahmoud Abbas na wito wake wa mara kwa mara wa kupata amani.

13. **TUNAUNGA MKONO** kurejeshwa kwa ombi la Dola ya Palestina kupata uanachama kamili wa Umoja wa Mataifa.

14. **TUNAZIALIKA** nchi zote za Afrika kusaidia kampeni za msaada wa haraka katika Ukanda wa Gaza katika jitihada za kukomesha majanga ya kibinadamu yanayotokana na vita vya Israeli, na kumaliza uzingiraji haramu wa Israeli katika Ukanda wa Gaza.

15. **TUNAZIOMBA** Nchi Wanachama wa AU na jumuiya ya kimataifa kuzingatia sheria za kimataifa na maazimio yanayohusika ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, na kushirikiana katika jitihada za kusitisha uvamizi wa Israeli, ambao unahujumu misingi ya sheria za kimataifa.

16. **TUNATOA WITO** kwa jumuiya ya kimataifa kuhakikisha ulinzi kwa watu wa Palestina kwa mujibu wa Azimio la Baraza la Usalama la UN namba 605 la mwaka 1987, Azimio namba 673 la mwaka 1990, na Azimio namba 904 la mwaka 1994, kwa kuzingatia Mikataba ya Geneva pamoja na maazimio yaliyopitishwa na Baraza Kuu, ikiwemo kikao chake maalum cha dharura kilichofanyika mwezi Julai mwaka 2018.

17. **TUNATHAMINI** jitihada zinazoendelea za Afrika kusaidia watu wa Palestina, hasa wasilisho lake kuhusu uchunguzi wa kisheria kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ) linaloomba maoni na ushauri wa kisheria kuhusu Israeli kuendelea kukiuka haki za watu wa Palestina kujiamulia mambo yao wenyewe, na uvamizi wa muda mrefu, makazi ya walowezi na kuendelea kuvamia maeneo ya Palestina. **HIVYO, TUNAIAGIZA** Kamisheni ya AU kupitia Ofisi ya Sheria (OLC) kuendelea na ushiriki wake katika mchakato wa maoni ya ushauri wa ICJ, ikiwa ni pamoja na kuandaa uwakilishi wowote unaohitajika kuunga mkono msimamo wa Umoja wa Afrika kwa kuzingatia kanuni zake za muda mrefu na mikataba ya kimataifa.

18. **TUNASISITIZA** uungaji mkono wetu usioyumbayumba kwa maazimio husika ya Baraza Kuu la UN kuhusu Palestina na msimamo uliotangazwa wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu ukatili unaoendelea kufanywa huko Gaza licha ya Mkataba wa Amani uliotiwa saini hivi karibuni wa kusitisha mapigano ambao bila shaka unaweza kusababisha madhara makubwa kwa hali ya amani na usalama katika Mashariki ya Kati.

19. **TUNASISITIZA** haja ya kushughulikia chanzo cha mgogoro huu wa muda mrefu, hususa Israeli kukalia, na kutaifisha ardhi ya Palestina, Makazi ya Waisrael, na ukiukwaji wa sheria za kimataifa; na mchakato wa amani uliokwama kwa makusudi na kukiuka sheria ya kimataifa na maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa:

20. **TUNASISITIZA ZAIDI** kwamba suluhisho la kisiasa kwa kuzingatia mtazamo wa mataifa mawili, ndo njia inayofaa zaidi kuhakikisha amani, utulivu na usalama kwa watu na mataifa ya ukanda huo.

**21.** **TUNATHIBITISHA TENA** msimamo wetu kwamba amani ya haki, pana na ya kudumu katika Mashariki ya Kati inahitaji uondoaji kamili wa Israel kutoka kwenye ardhi zote za Palestina na za Kiarabu zinazokaliwa kwa mabavu tangu Juni 1967, pamoja na *Syrian Golan Heights* na maeneo ambayo bado yanakaliwa kwa mabavu huko kusini mwa Lebanon, na udhihirisho wa nchi huru ya Palestina, ikiwa na Jerusalaem Mashariki kama mji mkuu wake, na kurudi kwa wakimbizi Wapalestina kwenye makazi yao.

23. **TUNAOMBA** utekelezaji wa haraka wa hatua za muda zilizoamriwa na Mahakama ya Kimataifa (ICJ) tarehe 26 Januari 2024 katika ombi lililowasilishwa na Jamhuri ya Afrika Kusini dhidi ya Israeli kuhusu mzozo unaoendelea katika ukanda wa Gaza, ambao unaathiri heshima ya ulimwengu kwa sheria za kimataifa na umuhimu kwa Israeli kutii mara moja majukumu yake chini ya Mkataba wa Kuzuia Uhalifu na Adhabu kwa mauaji ya kimbari.

## AZIMIO KUHUSU KUONDOLEWA KWA VIKWAZO VYA KIUCHUMI, BIASHARA NA FEDHA VILIVYOWEKWA NA MAREKANI DHIDI YA JAMHURI YA CUBA

**Mkutano Mkuu,**

1. **UNAELEZEA** masikitiko makubwa kuhusu vikwazo haramu vinavyoendelea vya kiuchumi, biashara na fedha vilivyowekwa dhidi ya Serikali na wananchi wa Cuba;

2. **UNATHIBITISHA** kuunga mkono azimio la UNGA "Ulazima wa kukomesha vikwazo vya kiuchumi, biashara na fedha vilivyowekwa na Marekani dhidi ya Cuba";

3. **UNASISKITIKA** kusuasua kwa mahusiano ya pande mbili baina ya Cuba na Marekani, na kwa mara nyingine, unatoa wito kwa Serikali ya Marekani kuondoa vikwazo vya muda mrefu vya kiuchumi, biashara na fedha ilivyoweka dhidi ya wananchi wa Cuban;

4. **UNASIKITISHWA PIA** na hatua zilizotekeleza na Serikali ya Marekani tangu tarehe 9 Novemba 2017, ambazo zimeimarika na **KUELEZA KUSIKITISHWA SANA** na kupanuka kwa vikwazo hivyo na kuvuka mipaka, ikiwemo utekelezaji wa Ibara ya III ya **Helms-Burton Act** (kwenye aya ya **334** ya Azimio la Mawaziri wa G-77 la mwaka **2023**, ambayo inadumisha lugha ilele iliyokubaliwa mwaka **2022**);

5. **UNAELEZA kusikitishwa sana kuhusu kujumuishwa kwa Cuba kwenye orodha ya nchi ambazo zinatuhumiwa kufadhili ugaidi, hatua ambayo imekazia zaidi vikwazo vya kifedha kwenda Cuba kutokana na vikwazo; kwa hiyo, UNATOA WITO kuondolewa kwa Cuba katika orodha hiyo**;

6. **UNAKIRI** kwamba athari hasi za vikwazo hivyo zimekuwa mbaya na kwa muktadha wa sasa, ambapo Cuba inakabiliwa na athari za kiuchumi na kijamii za COVID-19;

7. **UNAKIRI PIA** kwamba vikwazo hivyo ni kikwazo kikubwa kwa jitihada za Cuba kutekeleza Ajenda 2030 ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Maendeleo Endelevu na linashiriki masikitiko haya kutokana na umhimu ambao Umoja wa Afrika unaweka kwenye kufikia malengo ya Ajenda iliyotajwa;

8. **UNAREJELEA PIA** mshikamano wake na wananchi wa Cuba.

## AZIMIO KUHUSU ATHARI ZA VIKWAZO NA HATUA ZA KULAZIMISHA KWA NCHI WANACHAMA WA UMOJA WA AFRIKA

**SISI**, Viongozi wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika, tuliokutana tarehe 15 na 16 Februari 2025, katika Mkutano wetu wa Kawaida wa 38 wa Mkutano Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika, jijini Addis Ababa, Ethiopia;

**TUKIREJELEA** madhumuni na misingi ya Sheria ya Kuanzisha AU, ikiwamo uhuru, uadilifu wa mipaka na uhuru wa Nchi Wanachama za Umoja wa Afrika, pamoja na ahadi ya kukuza maendeleo endelevu katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, kwa bara lenye Umoja na ustawi;

**TUNASISITIZA** Azimio la Misingi ya Sheria za Kimataifa kuhusu Uhusiano wa Kirafiki na Ushirikiano kati ya Nchi kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ambao miongoni mwa mambo mengine, unaeleza, kwamba hakuna Nchi inayoruhusiwa kutumia au kuhamasisha matumizi ya vikwazo vya kiuchumi, kisiasa au aina nyingine ya vikwazo kwa nchi nyingine ili kuzuia matumizi ya haki zake.

**TUNASISITIZA** kwamba nchi moja kuweka vikwazo na sheria kwa nchi nyingine ni kinyume cha sheria za kimataifa, sheria za kimataifa za kibinadamu, Sheria iliyoanzisha Umoja wa Afrika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa na taratibu na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani baina ya nchi;

**TUNASISITIZA** maAzimio ya Azimio la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa namba 76/161 la tarehe 16 Desemba 2021; namba 78/135; na namba 78/202 la tarehe 19 Desemba 2023, na Uamuzi wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa namba 18/120 la tarehe 30 Septemba 2011 na Azimio namba 24/14 la tarehe 27 Septemba 2013, namba 27/21 la tarehe 26 Septemba 2014; namba 30/2 la tarehe 1 Oktoba 2015; namba 36/10 la tarehe 28 Septemba 2017; namba 37/21 la tarehe 23 Machi 2018; namba 40/3 la tarehe 21 Machi 2019; namba 43/15 la tarehe 22 Juni 2020; namba 46/5 la tarehe 23 Machi 2021; namba 49/6 la tarehe 31 Machi 2022; na 52/13 la tarehe 3 Aprili 2023, ambayo yanazitaka Nchi zisiweke vikwazo kwa nchi nyingine, jambo ambalo ni kinyume cha misingi inayotambuliwa ya sheria za kimataifa na kusisitiza kwamba kulazimisha nchi nyingine kutekeleza hatua au sheria ni kinyume cha sheria za kimataifa, sheria za kimataifa za kibinadamu, mikataba, taratibu na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani baina ya Nchi.

**TUNAZINGATIA** Ripoti ya Mwangalizi Maalum kuhusu athari hasi za vikwazo katika ufikiaji wa haki za binadamu, iliyochapishwa tarehe 9 Agosti 2024; **TUNAKUBALI** kwamba vikwazo vya kijamii na kiuchumi na hatua za lazima ni vikwazo

vinavyozuia utekelezaji wa Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063 na Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030;

Tukionyesha wasiwasi wetu mkubwa kuhusu athari hasi za vikwazo na hatua za lazima za nchi katika haki ya maendeleo, na kukuza uhusiano mzuri wa kimataifa, biashara, uwekezaji, ushirikiano, pamoja na amani, usalama na utulivu;

**TUNASISITIZA** kwamba hatua hizi zina athari hasi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi na maendeleo ya taifa kwa ujumla, na zinachochea matatizo ya kibinadamu na mizozo katika Nchi zinazolengwa;

**TUNASHTUSHWA** na kutokuwa na usawa na viwango na gharama kubwa, zisizo na usawa za kibinadamu za hatua za lazima, na vikwazo vya kinchi na athari hasi kwa raia, hususani wanawake na watoto, wa Nchi zinazolengwa;

**TUNASHUGHULIKIA KIKAMILIFU** na athari hasi za vikwazo na hatua za lazima za kinchi kwa upande mmoja katika maendeleo ya baada ya mizozo, ujenzi wa upya, ujenzi wa amani na katika Kaulimbiu ya Mwaka ya Umoja wa Afrika ya 2025: "**Haki kwa Waafrika na Watu wa Asili ya Afrika kupitia Fidia."**

1. **TUNALAANI VIKALI** matumizi na utekelezaji wa vikwazo katika baadhi ya nchi kama zana za shinikizo, ikiwamo shinikizo la kisiasa na kiuchumi, dhidi ya nchi yoyote, hasa dhidi ya Nchi Wanachama za Umoja wa Afrika, kwa lengo la kuzuia nchi hizi kutekeleza haki zao za uhuru wa kujitawala na kujitambua;

2. **TUNAYATAKA** Mataifa yote kuepuka kuweka hatua za lazima kwa nchi nyingine, na **TUNATOA WITO** kwa Mataifa husika kuondoa hatua hizo, kwani zinapingana na Sheria ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika, Mkataba wa Umoja wa Mataifa na taratibu na kanuni zinazosimamia uhusiano wa amani baina ya Nchi katika ngazi zote, na kuzuia utekelezaji kikamilifu wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya nchi mbalimbali, pamoja na kuathiri utekelezaji wa haki za binadamu;

3. **TUNAPINGA VIKALI** hatua hizo ambazo, pia zinatishia uhuru wa mataifa kujitawala;

4. **TUNATOA WITO** kwa Mataifa yote kutotambua vikwazo hivyo wala kuvitekeleza, na kuchukua hatua stahiki, kukabiliana na matumizi vikwazo vinavyowekwa kwa nchi.

5. **TUNAITAKA** Serikali ya Marekani kuondoa vikwazo vya muda mrefu vilivyowekwa dhidi ya Serikali na Watu wa Zimbabwe, ili kuwezesha urejeshaji wa kiuchumi wa nchi hiyo. Tunatoa wito kwa Serikali ya Uingereza kuondoa vikwazo vyote

vilivyowekwa dhidi ya Zimbabwe ambavyo vilirithiwa wakati ilipojiondoa kutoka Umoja wa Ulaya tarehe 31 Januari 2020 na vikwazo vyote vya ziada ilivyovipitisha peke yake. Tunatambua hatua zilizochukuliwa, ambazo ni pamoja na, mazungumzo ya kisiasa na ushirikiano wa ngazi za juu kati ya Zimbabwe na Umoja wa Ulaya kuelekea kuondolewa kwa vikwazo. Pia, tunasisitiza kwamba Umoja wa Ulaya uchukue hatua zinazohitajika kuhakikisha kuwa vikwazo vyote vilivyosalia vinaondolewa;

6. **TUNATOA WITO** kwa Marekani, Nchi nyingine, na Taasisi kuondoa hatua za vikwazo zilizowekwa dhidi ya Serikali, Viongozi na Watu wa Jamhuri ya Sudan Kusini kwani zinakwenda kinyume na juhudi za kukuza maendeleo baada ya mzozo, ujenzi upya na ujenzi wa amani, na tunatoa wito kwa Umoja wa Mataifa kuondoa Vikwazo vya Silaha visiyo na haki ilivyowekwa dhidi ya Sudan Kusini, pamoja na vikwazo vingine vyote na hatua za vikwazo zilizochukuliwa na mashirika mengine ili kuwezesha nchi hiyo kuchapuza utekelezaji wa mageuzi ya Usalama kwa mujibu wa Mkataba wa Makubaliano ya Utatuzi wa Mgogoro wa Jamhuri ya Sudan Kusini (R-ARCSS) uliosainiwa mwaka 2018;

7. **TUNAUTAKA** Umoja wa Ulaya na Marekani kuondoa vikwazo kwa nchi vilivyowekwa dhidi ya Nchi ya Eritrea;

8. **TUNALIAGIZA** tena Jopo la Wazee, kuwasiliana na wakuu wa nchi zilizoweka vikwazo vya kiuchumi na vinginevyo vya kisheria dhidi ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika, ili vikwazo hivyo viondolewe mara moja na bila masharti.

9. **TUNASISITIZA** mshikamano wake na Watu wa Zimbabwe, Sudani ya Kusini na Nchi ya Eritrea katika kutumia haki yao ya kujitawala na kuamua hatma yao wenyewe.

**NENO LA SHUKRANI KWA MHE. MOUSSA FAKI MAHAMAT, MWENYEKITI ALIYEMALIZA MUDA WAKE WA KAMISHENI YA UMOJA WA AFRIKA, NA UONGOZI WA JUU ULIOMALIZA MUDA WAKE WA KAMISHENI HIYO.**

**Mkutano Mkuu,**

**Ukizingatia** kumalizika kwa muda wa Mhe. Moussa Faki Mahamat kama Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, na kutambua juhudi za kupigiwa mfano na muhimu zilizofanywa na Mhe. Moussa Faki Mahamat wakati wa uenyekiti wake wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU) kwa miaka minane, ambayo ilichangia kuendeleza Ajenda ya Umoja wa Afrika yenye lengo la kukidhi mahitaji ya Bara la Afrika na kuiweka Afrika katika ngazi ya kimataifa;

**Ukizingatia** mafanikio aliyoyapata pamoja na Uongozi wa Juu wa Kamisheni katika kipindi chao cha uongozi unaomaliza muda wake kwa kudhihirisha ujitoaji, dira na dhamira ya kulinda misingi na malengo ya Umoja wa Afrika, pamoja na kujitolea kwa malengo ya Afrika na mshikamano wa Afrika; na

**Ukibainisha** hasa usimamizi wake madhubuti na mzuri wa Umoja wa Afrika wakati wa janga la UVIKO-19 na utendaji kazi wa Mfuko wa Amani:

**1. UNATOA** shukurani zake za kina kwa Mhe. Moussa Faki Mahamat, Mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Umoja wa Afrika, Mhe. Dkt. Monique Nsanzabaganwa, Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni anayemaliza muda wake, na Makamishna wafuatao wanaomaliza muda wao: Mhe. Josefa Leonel Correia Sacko, Kamishna wa Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Uchumi wa Bluu na Mazingira Endelevu, Mhe. Albert Muchanga, Kamishna wa Maendeleo ya Uchumi, Utalii, Biashara, Viwanda, Madini, Mhe. Dkt. Amani Abou-Zeid, Kamishna wa Miundombinu na Nishati, Mhe. Minata Samate Cessouma, Kamishna wa Afya, Masuala ya Kibinadamu na Maendeleo ya Jamii, Mhe. Belhocine Mohammed, Kamishna wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, na Mhe. Bankole Adegboyega Adeoye, Kamishna wa Masuala ya Kisiasa, Amani na Usalama kwa uongozi wao mahiri, wenye maono na mfano wa kuigwa wa Umoja wa Afrika katika kipindi cha uongozi wao;

**2. UNAMPONGEZA** Mhe. Moussa Faki Mahamat kwa mafanikio mengi yaliyopatikana kwa Umoja wa Afrika chini ya uongozi wake, hususan usimamizi na uzuiaji wa migogoro barani Afrika; na

**3. UNATOA TENA** shukrani zake kwa Mhe. Moussa Faki Mahamat na Uongozi Juu wa Kamisheni unaomaliza muda wake kwa mchango wao muhimu katika mchakato wa utangamano, utulivu wa kisiasa, kiuchumi na kijamii katika Bara la Afrika.